Nipashe
Jumatatu Mei 27, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579928
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Mgonjwa wa akili aua 2, auawa na wenye hasira

UKURASA 2





Nipashe Spotika
NIPASHE JUMATATU MEI 27, 2019
NIYONZIMA AKIMBIZA WAGENI UBINGWA BARA UK.18

ISIKUPITE
Kama beki wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk atafanikiwa kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] mwaka huu, atakuwa beki wa kwanza kuweza kutwaa tuzo hiyo binafsi ya juu duniani kwa upande wa wachezaji wa soka tangu Fabio Cannavaro alipoitwaa miaka 12 iliopita.

FURUKUTA...
Kiungo wa Valencia, Francis Coquelin akila sahani moja na mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi (kulia), wakati wa mechi ya fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa Del Rey'] iliyopigwa juzi na Valencia kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

UKURASA 13

# Mbunge ataka Stiegler's, bomba la gesi bungeni

**AMTAKA** waziri kesho kueleza kuhusu...*Endelea Ukurasa wa 2*



Wakazi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera wakiwa wamefurika pande mbili za daraja la mto Kanoni linalounganisha eneo la mjini na maeneo mengine likiwa limefunikwa na maji ya mvua iliyonyesha jana na kusababisha magari kutopita. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA**

## Mafuriko yazingira mji wa Bukoba

UKURASA 3

## Viwanja vya ndege vyapewa utaratibu mifuko ya plastiki

UKURASA 24

**MICHEZO** SAMATTA ATUA, AFUNGUKA MAFANIKIO UBINGWA GENK UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Mbunge ataka Stiegler's, bomba la gesi bungeni

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Kivuli wa Nishati, John Mnyika, ameitaka serikali iwasilishe bungeni mkataba wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa uzalishaji umeme wa Stiegler's Gorge pamoja na mikataba yote ya bomba la gesi Mtwara na ripoti zote zilizotokana na kamati zilizoundwa kuhusu mafuta na gesi ili Bunge iipitie.

Pia ametaka serikali iwasilishe ripoti ya tathmini ya kimazingira iliyofanyika ya utekelezaji wa mradi wa Stiegler's ili Bunge lione athari zake.

Mnyika aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa mikataba hiyo pamoja na ripoti hizo ziwasilishwe bungeni kesho wakati waziri akiwasilisha hotuba ya wizara yake.

Akizungumzia kuhusu mkataba wa Stiegler's, Mnyika ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kibamba (Chadema), alidai umekuwa na mkanganyiko wa gharama zitakazotumika, hivyo ametaka upelekwe bungeni ili waone ni miujiza gani iliyofanyika kutoka utekelezaji wake wa miaka 12 awali hadi miaka mitatu sasa.

"Binafsi nimeshaandaa rasimu ya hotuba yenye kurasa 80 na aya 145 inayozungumzia mambo mbalimbali ya sekta ya umeme, gesi na mafuta," alisema.

Mnyika aliitaka serikali ieleze kwa nini inatoa maelezo ya uongo kuhusu utekelezaji wa mradi huo.

"Serikali ilileta bungeni muswada wa sheria unaohusu sekta inayogusa rasilimali za nchi, muswada mmojawapo ukiwa na kifungu chenye kutoa wajibu na haki kwa Bunge na wajibu kwa serikali kwenye mikataba mikubwa ya nchi inayogusa rasilimali za nchi.

"Mikataba hii ilikuwa na kifungu kwamba inabidi ipelekwe bungeni kwa sababu kumeshatokea utata wa mradi wa Stiegler's Gorge, wito wangu ni kwamba tarehe 28 (Jumanne) wakati waziri anasoma hotuba yake bungeni pamoja na hotuba ya serikali, awasilishe mkataba wa ujenzi wa mradi wa Stiegler's ili mbivu na mbichi zijulikane."

Mnyika alisema serikali ilisema mkataba ambao umesainiwa na mkandarasi ni wa Sh. trilioni 6, lakini awali iliwahi kusema mradi mzima utagharimu Sh. trilioni 10.

"Uchambuzi mbalimbali ukianzia na wa serikali yenyewe ikiwamo Wizara ya Nishati na Madini wakati huo (mwaka 2016) ilifanya uchambuzi kuhusu gharama za mradi huu ambao ungetumia miaka 12 kujengwa, hii ni kwa tathmini ya wizara na tathmini ya wataalamu kuanzia mwaka 2012," alisema.

Waziri huyo kivuli alisema kwa kawaida miradi mikubwa huwa na ongezeko la gharama kadri muda unavyokwenda.

"Kama serikali imesaini mkataba wa miezi 36 (sawa na miaka mitatu) nikitumia kigezo cha uchambuzi wa nyuma wa wizara hiyo, kwamba mradi utatumia miaka tisa mpaka 12.

"Ukiingiza ongezeko la gharama kutokana na muda, halafu ukapiga hesabu badala ya miezi 36, ukachukua miaka 12 ambayo ni miezi 144 ukafanya kwa asilimia 30 kwa kila mwaka, kama

INAENDELEA UK. 8



Mwendesha pikipiki akipita karibu na zilipotundikwa kofia ngumu za mitumba ambazo zinauzwa kando ya barabara ya Azikiwe jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Dhahabu lukuki yaingia sokoni kisa masoko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI Wizara ya Madini ikiwasilisha bajeti yake leo bungeni, imeelezwa kuwa kufunguliwa kwa masoko 22 ya madini kumeingiza dhahabu nyingi sokoni kuliko wakati mwingine wowote.

Katika kipindi cha mwezi mmoja, jumla ya kilo 409.3 za dhahabu zenye thamani ya Sh. bilioni 34.3 zimeuzwa ndani kwenye masoko hayo.

Akizungumza kwenye maonyesho ya madini yaliyoandaliwa na wizara hiyo kwenye Viwanja vya Bunge jana, Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Prof. Shukrani Manya, alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa kwa wachimbaji kwenye masoko ya Chunya, Geita na Mwanza.

"Tangu kufunguliwa kwa masoko hayo ni matokeo ya dhahabu nyingi sana kuingia sokoni na kuuzwa kwa wingi kuliko wakati mwingine wowote ule."

Aliongeza: "Ndani ya mwezi mmoja kabla ya soko na baada kuanzishwa masoko tumeona kwamba bidhaa nyingi zimekuja sokoni na serikali sasa inapata halali yake kwenye tozo ya mrabaha na ada ya ushuru wa huduma ambayo ndizo zinatozwa," aliongeza.

Mei 23, mwaka huu, akihojiwa na Idara ya Habari Maelezo, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema jumla ya kilo 409.3 za dhahabu zenye thamani ya Sh. bilioni 34.3 zimeuzwa ndani kwenye masoko hayo ndani ya mwezi mmoja.

"Biashara iliyofanyika kwenye masoko haya ni kubwa kwa kipindi cha Machi 17, mwaka huu hadi 17 Aprili mwaka huu, hapo katikati jumla ya kilo 409.3 za dhahabu zenye thamani ya Sh. bilioni 34.3,"alisema.

Aidha, alisema mapato hayo yataendelea kuongezeka kutokana na masoko mengine kuendelea kufunguliwa.

Akifungua maonyesho hayo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema ameshuhudia katika siku za karibuni masoko ya madini yakifunguliwa maeneo mbalimbali nchini.

"Ndugu zangu mnaojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa za madini na biashara ya madini, yatumieni masoko hayo, jiepusheni na tabia ya kutorosha madini," alisema.

Alitaka maonyesho hayo kutumika kama uwanja wa kufundishana na kushauriana katika shughuli za uongezaji thamani madini pamoja na kutumia teknolojia sahihi ili kuondokana na athari hasi za masuala ya uchimbaji wa madini.

"Hivyo, uzoefu mtakaoupata kupitia katika maonyesho haya ukawe ni chachu ya kwenda kuongeza ufanisi katika utendaji kazi kwenye maeneo yenu," alisema.

Alieleza kuwa sekta ya madini ni mojawapo ya sekta ambazo zinatoa mchango mkubwa katika uchumi na maendeleo ya nchi.

Naye Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, alisema maonyesho hayo yamejumuisha kampuni 43, taasisi 7 na vyama vya wachimbaji madini.

# Mgonjwa wa akili aua watu 2, naye auawa

**Na Steven William,** MUHEZA

WATU wawili wakazi wa kijiji cha Kilometa Saba, Kata ya Nkumba wilayani Muheza mkoani Tanga, wameuawa na mtu anayesadikiwa kuwa ni mgonjwa wa akili anayedaiwa kutoroka kwa mganga wa kienyeji.

Tukio hilo limetokea juzi asubuhi na kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, aliyeeleza kuwa mtu huyo anadaiwa alikuwa kwenye matibabu kwa mganga wa kienyeji.

Alimtaja mtu hiyo aliyehusika na mauaji hayo kisha naye kuuawa na wananchi wenye hasira kali ni Juma Kuziwa.

Aidha, aliwataja waliouawa na mgonjwa huyo ni Omari Saidi Lugulu na Asha Mohamed, ambao ni wakazi wa kijiji cha Kilometa Saba.

Akielezea tukio hilo, alisema baada ya Kuziwa kufanya tukio hilo, wananchi wenye hasira kali walimvamia wakampiga hadi kufa.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kilometa Saba, Saidi Hasani, alisema alipelekwa kwa mganga wa kienyeji aliyejulikana kwa jina la Hamisi Kabweche ili kupatiwa tiba, lakini kwa bahati mbaya alitoroka.

Hassani alisema baada ya kutoroka alikutana na Asha Mohamed, na alimpiga fimbo sehemu ya kichwa na kupoteza fahamu na alipelekwa hospitali Teule Muheza mjini alifariki dunia.

Alisema mgonjwa huyo alikutana na Omari Lugulu ambaye nae alimpiga kwa fimbo, na alianguka chini na kupoteza maisha yake papo hapo.

Alisema baada ya kumuua mtu wa pili, wananchi wenye hasira walimkamata wakampiga hadi alivyofariki.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kilometa Saba, Rose Mdaki, walitoa taarifa polisi ambao walifika na kuchukua miili hiyo na kwamba mganga wa kienyeji alikimbilia kusikojulikana.

Diwani wa kata ya Nkumba, wilayani Muheza mkoani Tanga, Challes Mhilu, alisema kifo hicho kinasikitisha kwa kuwa wameuawa watu wasio na hatia, huku akiwataka wanafamilia kuwa watulivu wakati wa mazishi ya miili hiyo.

Katibu wa Chama cha Waganga wa Tiba Asili Wilaya ya Muheza, John Ngoda, alisema mganga huyo anafahamika kwenye chama hicho, lakini hajasajiliwa serikalini.

# HABARI KITAIFA



Kamishna wa Tume ya Madini, Prof. Abdulrahman Mruma (wapili kulia), akimwonyesha jambo Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, jiwe la madini ya almasi lenye uzito wa "ct" 512.15 likiwa na thamani ya Sh. bilioni 3,262,149,332.75 wakati wa mauzo yake yaliyofanyika katika soko la madini la mkoa wa Shinyanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: ISSA MTUWA**

## Kipindupindu chaibuka tena Dar es Salaam

**Na Mwandishi wetu**

UGONJWA wa kipindupindu umeibuka katika Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam na mgonjwa mmoja kulazwa katika Zahanati ya Vingunguti.

Aidha, limetengwa eneo maalum kwa ajili ya kupokea na kuhudumia wagonjwa hao kama wataendelea kuongezeka. Akizungumza jana na Nipashe, Kaimu Meya wa Ilala, Omari Kumbilamoto, alisema kutokana na kugundulika kwa mgonjwa huo wametenga eneo maalum la kuhudumia wagonjwa iwapo wataongezeka. Alisema hadi sasa wamebaini kuwa chanzo cha ugonjwa huo ni baadhi ya wananchi kutiririsha majitaka ambayo yanakwenda kwenye maji yanayotumiwa na wananchi.

Kumbilamoto ambaye pia ni diwani wa Vingunguti, alisema hatua za awali zilizochukuliwa ni kunyunyiza dawa kwenye maeneo ya maji machafu yaliyotuama ikiwamo kuchukua hatua kwa wanaotiririsha maji hayo kutoka kwenye vyoo.

Aidha, alisema wanawaelimisha wananchi kunyunyiza dawa, kuchemsha maji, kunawa kwa maji ya moto kabla ya kula na kuhakikisha usafi wa mazingira kila wakati.

Kwa mujibu wa Meya huyo, kwenye maeneo ya masoko wamewaelekeza wahusika kuhakikisha takataka hazikai kwa muda mrefu na usafi wa wafanyabiashara na watumiaji wengine. "Tulichobaini ni kwamba wakati wa mvua hizi, baadhi ya wananchi walikuwa wanazibua vyoo vyao na kutiririsha maji taka ovyo, hii inasababishwa na ukweli kuwa Vingunguti ni eneo la majimaji na limejengwa bila mpangilio na hivyo kushindwa kupitisha gari la kunyonya majitaka," alisema. "Tumechukua hatua kwa watu wanne tuliowakamata kwa kuwapiga faini ya Sh. 30,000 kwa kosa la kutiririsha majitaka, na wengine walikamatwa na kuwekwa ofisi za kata na kuachiwa," alibainisha.

Kuhusu athari za mafuriko, alisema baadhi ya maeneo ya manispaa hiyo yameathiriwa na mvua hiyo ikiwamo eneo la Mtambani na Miembeni, nyumba 12 kujaa maji.

# Mafuriko yazingira Bukoba

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MVUA iliyonyesha jana asubuhi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kagera ikiwamo mji wa Bukoba, imesababisha athari kubwa ikiwamo kuingia katika makazi ya watu, na madaraja kujaa maji.

Hali hiyo ilisababisha wananchi waliokuwa mjini kushindwa kwenda nje ya mji na waliokuwa nje ya mji kushindwa kuingia mjini.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakazi wa Manispaa ya Bukoba walisema kuwa mafuriko hayo yametokana na baadhi yao kujenga kandokando ya mito na kusababisha maji yasitiririke vizuri kutokana na kubana mkondo wa maji.

Kenedy January aliitupia lawama serikali kutokana na kulifumbia macho tatizo hilo ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara.

"Pia mitaro ipanuliwe na isafishwe mara kwa mara ili maji yapite kwa wepesi zaidi,"alisema January.

Mkazi mwingine wa manispaa hiyo, Mustafa Babu, alisema nchi ina viongozi kuanzia ngazi za mitaa, huku wananchi wanajenga katika maeneo yasiyofaa au yasiyoruhusiwa bila kuchukuliwa hatua, matokeo yake yanatokea madhara ikiwamo kuharibu mali na vifo.

Tumaini Barnabas, alisema serikali iwahamishe kwa nguvu wananchi waliojenga katika maeneo hatarishi ili kuepuka madhara yanayojitokeza karibu kila mwaka.

Akizungumzia tukio hilo kwa njia ya simu Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawilo, alisema wamezuia wananchi wasijaribu kuvuka kwenye madaraja yaliyojaa maji kwenda popote, na kuwa askari polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wanazunguka maeneo mbalimbali kudhibiti watu ili yasitokee maafa.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya alisema wanatafuta mitumbwi kwa ajili ya kusaidia kuvusha watu ambao wamezingirwa na maji.

Maeneo yaliyoko katika Mansipaa ya Bukoba yaliyozingirwa na maji ni Omukigusha, Kyakailabwa, Hamugembe, Buyekera na Kagondo, lakini hadi sasa hasara iliyosababishwa na mvua hiyo haijafahamika, huku mali zinazoonekana kuathirika zaidi ni nyumba na samani.

# Wiki ya Kabudi, makinikia, Stiegler's Gorge bungeni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BUNGE la Bajeti linaloendelea mjini Dodoma, leo linaingia katika juma la tisa huku utekelezaji wa mradi wa umeme wa maji katika Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge, ukitarajiwa kuendelea kuteka mijadala ya chombo hicho cha kutunga sheria.

Vilevile, katika mijadala ya wiki hii, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, anatarajiwa kujibu tuhuma ambazo zimekuwa zikielekezwa kwake na baadhi ya wabunge kwamba ametoa ushauri mbovu wa kisheria kwa serikali katika mambo mbalimbali hivi karibuni.

Katika mijadala ya Bunge wiki hii, pia kunatarajiwa kuibuka hoja ya malipo ya mabilioni ya shilingi ambayo serikali ilieleza kuahidiwa kulipwa na Barrick, Kampuni ya Uchimbaji Madini ambayo vigogo wake walilazimika kuja nchini kufanya mazungumzo na serikali baada ya Tanzania kuzuia usafirishaji wa makinikia kwenda nje kuchenjuliwa.

Ratiba iliyotolewa na Idara ya Habari na Elimu ya Bunge, inaonyesha kuwa leo, mbali

INAENDELEA UK.8


## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Yono Auction Mart and Company Ltd** Kwa idhini tuliyopewa na **AMANA BANK LTD** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa wadaiwa wote na wadhamini mlipe madeni yenu yote kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. Mnada utafanyika mahali ilipo dhamana.

### MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA NA MAHALI ILIPO

| NA | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | JINA LA MMILIKI | DHAMANA INAYOUZWA | MAHALI DHAMANA ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | JACQUELINE CHARLES KOMBA | ABUBAKARI FAMAU ABUBAKARI | License no. TMK046448<br>L.O no. TMK/MBGK/KJC20/228 | Mbagala kuu<br>Mtoni Kijichi Area<br>Dar es salaam | Tarehe 14.06.2019<br>Saa Nne (10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| 2 | ALI ABDALLAH TALIB | ALLY ABDALLAH TALIB | C.T No. 33493 LR Moshi,<br>L.O No. 251026 | Plot No 133, Block 'A'<br>Engare-Olmotonyi area<br>Arumeru District | Tarehe 21.06.2019<br>Saa Nne(10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| 3 | SLAZNA GENERAL SUPPLIES CO. | SHABANI RASHID CHANDE | Res. License No. ILA 026796<br>Parcel No. ILA/KWN/MZF7/58 | Minazi Mirefu,<br>Kiwalani<br>Ilala municipality<br>Dar es salaam | Tarehe 14.06.2019<br>Saa Nane(02:00 P.M) mchana na kuendelea |
| 4 | NGAKA IBRAHIM SOMBOKA | NGAKA IBRAHIM SOMBOKA | C.T No. 033005/40<br>L.O No. 52285 | Plot No 88, Block 'B'<br>Azimio Street area<br>Mwanza Municipality | Tarehe 22.06.2019<br>Saa Nne(10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| 5 | MF ELECTRICAL ENGINEERING LTD | ANDREW SIMON MWAIPAJA | C.T No. 130621<br>L.O No. 527629 | Plot No 2116, Block 'L'<br>Mbezi Beach area,<br>Dar es salaam City | Tarehe 15.06.2019<br>Saa Nne (10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| 6 | MAMMUT HOLDINGS INTERNATIONAL LTD | MAHMOUD ABUBAKAR AHMED | C.T No. 26387<br>L.O No. 51462 | Plot No 146, Block 'F'<br>Mikocheni area,<br>Dar es salaam City | Tarehe 15.06.2019<br>Saa Nane (02:00 P.M) Mchana na kuendelea |

Yono Auction mart Mawasiliano simu No 0767 675 168

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mnunuzi anatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki atakilipa ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
2) Ukaguzi wa dhamana utafanyika siku nne kabla ya mnada kuanzia saa Nne(10:00 A.M) asubuhi hadi saa Nane (02:00 P.M) mchana.
3) Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4) Dhamana itauzwa "kama **ilivyo**"

215247602

MAHOJIANO MAALUM

# Mbunge amwonesha Magufuli rushwa iliko

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Serengeti, Marwa Ryoba (CCM) (pichani), amempongeza Rais John Magufuli kwa utekelezaji wa miradi mikubwa na kuchukua hatua dhidi ya wanaojihusisha na rushwa.

Hata hivyo, mbunge huyo amesema licha ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali ya awamu ya tano kukabiliana na changamoto ya rushwa, bado kuna maeneo ambayo vitendo hivyo vinaendelea kutokana na wahusika kutoonekana kirahisi kwa Rais Magufuli.

Katika mahojiano maalum na Nipashe, mbali na kuzungumzia changamoto ya rushwa, Ryoba pia aliishauri serikali kufumua mfumo wa elimu, akieleza kuwa umepitwa na wakati.

Katika mahojiano hayo, mbunge huyo pia alitaja sababu za kukihama Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na kueleza kuwa haoni mbunge kutoka upinzani ambaye atarejea bungeni baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mwalimu huyo wa masomo ya Kemia na Baiolojia:-

**SWALI:** Ukipata nafasi ya dakika moja leo kuzungumza na Rais Magufuli, utamshauri jambo gani muhimu kwa taifa?

**RYOBA:** Kwanza nitampongeza kwa sababu anaendelea vizuri. Kwa kweli kuna vitu anafanya kimsingi hakuna mtu mwingine wa kawaida angeweza kufanya. Kuna maamuzi magumu anafanya hakuna mtu mwingine wa kawaida angeweza kufanya.

Mfano, jiulize leo katika hali ya kawaida nani angetekeleza mradi wa Stiegler's Gorge ambao unapingwa na watu wengi.

Lakini kwa manufaa ya taifa, ili tupate umeme mwingi wa kutosha utakaopunguza bei ya umeme, kwa kila mwananchi, mradi ambao utasaidia viwanda vya ndani kupata umeme wa bei nafuu, ameamua kuutekeleza.

Jambo lingine analofanya ni vita dhidi ya rushwa. Ilikuwa imefika mahali kila Mtanzania akipata nafasi ya kuwa sehemu, anatafuta namna ya kula, kwamba utakula kwa urefu wa kamba yako. Kwa hiyo, ukiwa na nafasi unaitumia. Nchi ilikuwa imeharibika.

Rais Magufuli amejitahidi sana lakini bado ninaona kuna mianya, kuna watendaji wake wa huku chini hawajakaa sawasawa.

Kwa hiyo ningemshauri atie nguvu zaidi kuchungulia watendaji wa chini huku, mfano wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya. Kuna watendaji huku chini bado hawajamwelewa zaidi. Huku chini bado hali si shwari sana.

Rais amefanya kazi kubwa sana na amejipambanua kuwa ni mpambanaji dhidi ya wala rushwa na watu wanaogopa. Tatizo wanamwogopa yeye, wanapopata nafasi pale ambapo yeye hawezi kuona, wanapiga.

Kwa hiyo, aandae mfumo ambao



utamsaidia kupata taarifa na kukabidhi majukumu hayo kwa watu wake waweze kumsaidia kubaini nani mla rushwa na kuanza kushughulika nao.

Unajua bila kiboko mambo hayawezi kwenda. Kama kuna mtu anakula rushwa, tumbua, kutumbua tu ndiyo dawa. Eeeh! Wewe umepewa nafasi, tumika, heshimu fedha za umma, hutaki kuheshimu, tumbuliwa.

**SWALI:** Wewe ni mwalimu. Chamgamoto kubwa ya sekta ya elimu nchini kwa sasa ni nini?

**RYOBA:** Elimu yoyote lazima ijibu matatizo ya nchi au ya watu husika. Mfumo wa elimu tulionao ni wa kizamani sana. Mfano, zamani mtu ulikuwa unasoma ukitegemea kuajiriwa na kwa kweli zamani ulikuwa ukihitimu tu unapata ajira.

Lakini sasa hivi wanaomaliza vyuo vikuu, wanaomaliza diploma, wanaomaliza astashahada ni wengi sana kiasi kwamba haitawezekana na haitakaa iwezekane serikali ikawaajiri wote. Zamani ilikuwa mkihitimu tu wote mnachukuliwa na serikali.

Sasa vyuo vimekuwa vingi na wanaohitimu ni wengi, wenye shahada ya uzamili ni wengi, wenye PhD ni wengi na hata maprofesa sasa ni wengi.

Mimi nadhani lazima kama nchi tufanye mabadiliko katika mfumo wetu wa elimu. Kwa mfano, iwe ni lazima kuanzia shule ya msingi vijana wetu wafundishwe masomo ya ujasiriamali, ufugaji, kilimo na usindikaji ili wakimaliza masomo wawe na uwezo wa kwenda kujitegemea huko. Wapo wanamaliza darasa la saba hawaendelei na sekondari. Wale wanakwenda kufanya nini? Hatutaki wawe tegemezi lakini wawe na ABCD za usindikaji, ujasiriamali, kilimo na ufugaji.

Na ukiangalia wakulima wengi darasa la saba, wafugaji wengi darasa la saba, watu wanaojishughulisha na biashara ndogo ndogo darasa la saba.

Lakini pia tufike wakati tubadili lugha ya kufundishia. Ukiangalia duniani kote, wanasaikolojia wote, wataalamu wote wamefanya utafiti na kugundua lugha inajifunzwa kuanzia utotoni. Mtoto anapozaliwa hadi umri wa miaka 10, ndo kipindi cha kujifunza lugha.

Sisi Tanzania tunasubiri mtoto afike sekondari akiwa na miaka 14 ndo aanze kujifunza Kiingereza. Kujifunza lugha ukiwa na zaidi ya miaka 10 ni ngumu sana ndiyo maana unaona Watanzania hata kwenye kuongea Kiingereza hatuko vizuri, ni kwa sababu hatukujifunza Kiingereza utotoni.

Kwa hiyo ifikie sehemu tuamue maana kiukweli dunia Inazungumza Kiingereza. Wachina wanapata shida kwenye biashara, inabidi ajue Kiingereza ili aweze kuwasiliana na Afrika na mabara mengine. Kichina tu hakitoshi.

Mimi naona ni vyema tukatumia Kiingereza kwa watoto wetu kujifunza. Watoto wangu wako English Medium School, watoto wa wabunge, mawaziri na watu wengi wenye fedha wamewapeleka watoto wao English Medium School kwa sababu ya Kiingereza. Kiingereza kaka ndiyo lugha ya dunia kwa sasa.

Kwa hiyo, ifike sehemu kama nchi tuamue, lakini si kwamba tuachane kabisa na Kiswahili, 'no' (hapana) -- Kiswahili kiwapo, kiendelee kuwa somo na lugha ya taifa, lakini Kiingereza iwe lugha ya kujifunzia.

Hata 'innovation' (ubunifu) italetwa pia na lugha. Kama hatuelewi lugha tutabaki na vyeti hapo, mtu ana vyeti vingi lakini hana ubunifu wowote. Ukiangalia kwenye nchi kama Nigeria watu wanakuwa wavumbuzi, Rwanda hapa, Kenya hapa kuna uvumbuzi kwa sababu wanaelewa wanachofundishwa.

Sisi unaanza kufundishwa Kiingereza una miaka 14. Ndiyo maana hata Kiingereza chetu ni cha ajabu. Kwa hiyo mimi naona kwenye mfumo wetu wa elimu tuufumue utusaidie watu wetu kwenda kujiajiri huko duniani.

Kwa mfano, tuna wabunge wengi ukiangalia hapa na mbunge anaweza kupata fedha, lakini akaenda kufanya biashara ikafa. Inakufa kwa sababu hana 'skills' za ujasiriamali, za kufanya biashara. Leo anapata fedha inakwisha yote.

**SWALI:** Huoni kwamba kukifanya Kiingereza kuwa lugha ya kufundishia nchini ni kwenda kinyume cha mtazamo wa Mwalimu Nyerere wa kukikuza Kiswahili?

**RYOBA:** Tujiulize tunataka kufanya biashara na nani? Nenda Uganda tu hapa -- hata bodaboda wanaongea Kiingereza. Kila mtu anaongea Kiingereza. Nchi zinazoongea Kiswahili kwa asilimia 100 ni ngapi? Tunataka kwenda haraka. Utakwenda haraka? Lazima Kiingereza kaka. Nenda Uganda, nenda Kenya, nenda Rwanda utabaini hilo.

Sisi inafikia kipindi hata kwenye kushawishi mambo fulani inakuwa shida. Lugha kaka, lugha ni tatizo. mtu asikudanganye, mimi ni mwalimu, naelewa nachokisema. Watanzania bado kwenye hili eneo. Sawa kuna Watanzania wachache wamesoma nje ya nchi, wamepata bahati ya kusoma English Medium School, lakini nakwambia hii ya Kiswahili inaturudisha nyuma.

**SWALI:** Jimbo la Serengeti linakabiliwa na changamoto ipi kubwa kwa sasa na hatua gani zimechukuliwa kuitatua?

**RYOBA:** changamoto ya kwanza ni barabara. Ukitamka Serengeti, dunia yote wanaijua ni urithi wa kimataifa. Hifadhi ya Taifa Serengeti iko Wilaya ya Serengeti, Mkoa wa Mara. Ukienda makao makuu ya Wilaya ya Serengeti, hayajaunganishwa na barabara ya lami. Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha hatujaunganishwa na barabara ya lami. Hatujawapa hizi faida za utalii watu wa Mara ndo maana utakuta utalii umejikita kaskazini huko Arusha.

Kule Mara watalii wanapata shida kwa sababu ya miundombinu, barabara ni mbovu. Tukiunganishwa kwa barabara ya lami, Mkoa wa Mara utaanza kung'ara kwa uchumi kiutalii kutokana na mbuga ya Serengeti, angalia wanyama wote wale.

Tuna changamoto nyingine ambayo ni ugumu wa upatikanaji wa maji. Najua mipango ya serikali, mimi ni kuihimiza tu serikali yangu ya CCM itekeleze miradi. Nimeona mwaka ujao tumetengewa Sh. bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa barabara, kipande cha Sanzate-Mugumu na tumepata fedha pia kutoka Serikali ya India kwa ajili ya mradi wa maji.

**SWALI:** Yalisemwa mengi baada ya kutangaza kujiunga na CCM. Hebu tuambie nini hasa kilichokutoa Chadema?

**RYOBA:** Mimi ni mtu mzima na maisha nayaona. Hakuna mtu aliyeniambia 'nenda Chadema'. ni nafsi yangu. Nilijiunga na Chadema mwaka 2007. Kabla ya hapo sikuwahi kuwa mwanachama wa chama chochote.

Kujiunga na chama chochote cha siasa si dhambi kwa mujibu wa Katiba ya nchi, si dhambi kwa mujibu wa sheria na kanuni za vyama vya siasa. Kila Mtanzania ana haki ya kujiunga na chama chochote cha siasa wakati wowote. Na Biblia pia inaruhusu. Kwa hiyo ni uhuru.

Niliamua kuja CCM baada ya kuona Chadema imekosa mwelekeo. Kulikuwa na Bunge la Katiba ambalo lingetusaidia kupata Katiba nzuri. Wakaunda Ukawa (Umoja wa Katiba ya Wananchi), wakaondoka kwa sababu ya hoja ya serikali tatu, lakini mle ndani kulikuwa na mambo mengi mazuri ikiwamo Tume huru ya Uchaguzi, wakaondoka.

Sasa unajiuliza unaona, mbora kila mtu afanye mambo yake. Mimi nimeamua kujiunga na CCM kwa sababu nimeona kwa mtazamo wangu ndiyo chama kinachoweza kutufikisha. Huku kwingine ni kutwanga maji kwenye kinu.

Hivi vyama vingine, kitaenda, kitafika mahali pazuri lakini kitaporomoka. Chadema ilikuwa ichukue nchi mwaka 2015, baada ya hapo si unajua wananchi wameshakata tamaa na Chadema 'brother' (kaka).

Chadema imeisha, unadhani Chadema itainuka tena? Imeshakwisha! Sasa unaona ACT inaanza kunyanyuka, na yenyewe itafika mahali itaporomoka. Kwa hiyo, kila mtu afanye mambo yake.

Mimi nimeamua kujiunga na CCM baada ya kuona angalau kina mwelekeo. Kwa kweli mwaka 2015 kurudi nyuma CCM ilikuwa imeharibika, nadhani hata wewe utakuwa unalifahamu hilo, lakini sasa CCM imenyooka, imenyooka, wakisema ni hivi, ni hivi. Mwenyekiti wa CCM, Mheshimiwa Rais Magufuli, akisema jambo linatekelezeka.

'So what do you want' (unataka nini)? 'If you can't fight them join them' (kama huwezi kuwashinda ungana nao). Mimi nimeona Chadema haiwezi kuishinda CCM, acha niungane nao.

**SWALI:** Matumaini ni makubwa kiasi gani kwamba utarejea bungeni baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani?

**RYOBA:** Mimi ni mkristo na katika ukristo tuna kitu tinakiita imani. Imani ni kuwa na uhakika na mambo yatarajiwayo. Ninaamini kwa imani kwamba 2020 'I will be there' (nitakuwapo). Naamini kwa sababu Biblia inasema 'mwenye haki wangu ataishi kwa imani'.

Imani ni ya moyoni. Kwa hiyo mimi naamini nitakuwapo kwa sababu baada ya kuja CCM, chama kimeonyesha imani kwangu. Kwa hiyo, bado naamini ndani ya chama watanichagua. Naamini, si kwamba ni lazima.

Lakini hata nisipochaguliwa, maisha si yapo tu nje ya siasa. Si lazima niwe mbunge. Kwani wangapi ni wabunge? Wewe ni mbunge? Ni nafasi unapata, ni neema ya Mungu, si lazima maana hujui kesho yako. Mungu ndo anapanga. Lakini Mungu anatuwazia mema.

**SWALI:** Kwa hali ya kisiasa iliyopo nchini, unatarajia upinzani kufanya vizuri katika Uchaguzi Mkuu ujao?

**RYOBA:** ... (kicheko) Sasa si unaona hivi vyama vya upinzani vimepoteza mwelekeo 'brother' (kaka). Yaani kuna mbunge gani wa kushinda kwa mfano? Mimi sijaona mbunge wa upinzani atakayeshinda mwakani. Nani kwa mfano?

Si unaona hapa bungeni wamepoteana kaka. Kwani unamwona hata kiongozi wao (Freeman) Mbowe bungeni? Mimi nakuhakikishia hakuna mbunge wa upinzani atakayerudi, sioni! Kama watarudi, wachache sana kwa neema ya Mungu.

**SWALI:** Unatarajia kurejea kufundisha baada ya ubunge?

**RYOBA:** Mimi bado nafundisha. Mimi ni miongoni mwa wabunge wachache wanaoishi jimboni. Sina nyumba sehemu yoyote Tanzania nje ya Wilaya ya Serengeti. Familia yangu iko Serengeti, Bunge likiisha, narudi jimboni napiga mzigo ikiwamo kufundisha.

Mimi nafurahia kufindisha. Hata kwenye siasa ujue nafundisha. Kwenye mikutano yangu jimboni nafundisha. Kufundisha hakukomi, ni taaluma. Inategemeana sasa uko kiwango gani. Masomo rasmi ya darasani, bado uwezo huo ninao, nikipata nafasi nafundisha, lakini pia kwenye mikutano yangu jimboni nafundisha. Mwalimu ni mwalimu tu.

## HABARI KITAIFA




Meneja Bidhaa za Simu kutoka Tigo, Mkumbo Myonga (kulia) pamoja na Meneja wa Samsung Tanzania Suleiman Mohammed (kushoto) wakitoa maelezo kwa waandishi wa habari (hawapo pichani) juu ya matoleo mapya simu za Samsung aina ya Galaxy A Series ambazo zinakuja na ofa ya hadi GB96 za intaneti wakati wa uzinguzi wa simu hizo uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu 400 wasomeshwa Udom kujua KKK

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

SERIKALI mkoani Mwanza, imewasomesha Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), zaidi ya walimu 400 wa shule za msingi watakaofundisha wanafunzi wa awali hadi darasa la tatu kujua kutumia alama za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

Akizungumza ofisini kwake jijini hapa, Ofisa Elimu Taaluma mkoani Mwanza, Ngoseki Joseph, alisema kuwa walimu hao waliosomeshwa ni kutoka katika wilaya nane za mkoa huo. "Walimu zaidi ya 400 wamesomeshwa na serikali, Chuo Kikuu cha Dodoma, kwa ajili ya kufundisha watoto hao shule za msingi kuanzia darasa la awali hadi la tatu kujua kutumia alama za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKKk) kutoka wilaya nane, alisema Ngoseki.

Alizitaja wilaya hizo kuwa ni Nyamagana, Sengerema, Magu, Ukerewe, Misungwi, Buchosa, Kwimba pamoja na Ilemela ambao watasaidia kuondoa tatizo la wanafunzi wanaofika darasa la nne hadi la saba wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Alisema walimu waliopata elimu hiyo chuo kikuu watakuwa rasmi katika ufundishaji wa masomo ya alama hizo, kuliko ambao hajasomea na kwamba walimu hao wataongeza ufaulu wa wanafunzi shuleni hasa wa darasa la saba kwenda sekondari. Aidha, alisema changamoto zilizopo katika shule za msingi ni pamoja na ufundishaji hafifu wa walimu wa masomo mbalimbali kutokana na kutokuwa na uwezo wa kufundisha, uzembe wa kufundisha vipindi darasani, wengine kuwa watoro shuleni wakifanya shughuli zao binafsi. Ngoseki alisema kuwa serikali imekuwa ikiwahimiza walimu kufuata maadili ya kazi, ikiwamo kuwafukuza kazi wasiofuata wajibu wao ili kuleta ufanisi na tija katika sekta ya elimu mkoani humo.

# Tawla yakerwa kesi dhuluma ya ardhi kumalizwa kifamilia

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wanasheria Wanawake (Tawla), kimesema changamoto wanayokabiliana nayo katika miaka 30 ya kutoa msaada wa kisheria nchini ni kesi nyingi za kudhulumiwa ardhi na mirathi kumalizwa kifamilia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tawla, Tike Mwambipile, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam, katika Mkutano Mkuu wa Tawla na kusema kuwa kesi za ardhi hazifiki mwisho kwa sababu si wavumilivu wa kusubiri haki kwa mujibu wa sheria.

"Miaka 30 ya Tawla changamoto bado nyingi hasa kwa wanawake wanaokuja kutaka msaada wa kisheria, tunawasaidia kwa nia njema lakini wengine wanamalizana kifamilia, mwisho tunaonekana wabaya na kuonekana sisi tunamshawishi, kuchukua hatua," alisema Mwambipile.

Alisema chama hicho ambacho kinatimiza miaka 30 tangu kuanzishwa kwake, kinaendelea kutoa misaada mbalimbali ya kisheria kwa wanawake na vijana kujua haki zao.

Naye Mwanasheria Naseku Kisambu, aliwataka wanawake kuonyesha mfano katika kuwania nyanja mbalimbali za uongozi ili kusukuma mbele gurudumu la kumkomboa mwanamke na mtoto wa kike.

Kisambu alisema inashangaza wanasheria wanawake licha ya kujua sheria na mikataba mbalimbali ya haki za binadamu, lakini wamekuwa wazito kujitokeza kuwania nafasi za uongozi.

"Sisi kama wanasheria tunafaida kubwa, tunajua sheria, tunajua mikataba mbalimbali ya kisheria, lakini je, tunatumiaje hizo nafasi zinapokuja? Lazima tujiulize," Kisambu alihoji na kuongeza:

"Wanawake ambao hawakupata nafasi ya kusoma na wale wa ngazi za chini tunasema mfumo dume na kutojua sheria inawakandamiza, sasa sisi tunaoijua tunaitumiaje, tunaonyesha mfano gani, tunafanya nini kama wanasheria?" alihoji.

Jaji wa Mahakama Kuu, ambaye pia ni miongoni mwa waanzilishi wa Tawla, Joaquine De Mello, alisema anafurahi kushuhudia miaka 30 ya Tawla ikiwa imepiga hatua kubwa na inajiuza, haijawahi kuyumba wala kutoka nje ya lengo la kuanzishwa kwake.

# Watanzania 2 washinda tuzo ya kimataifa Qur'an

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA wa Kitanzania, Zakaria Sheha Ally na Shamsi Mwalimu Said, wamechukua nafasi ya kwanza na ya tatu kwenye fainali za 27 za tuzo ya kimataifa ya kuhifadhi Qur'an tukufu.Zakaria Sheha Ally (16), kutoka Tanzania Bara na Shamsi Mwalimu Said (19), kutoka Zanzibar wameibuka na kitita cha dola za Marekani 5,000 na dola 3,000 kila mmoja baada ya kuwashinda wenzao wanane waliofanikiwa kuingia fainali hizo ambao walitoka Afrika Kusini, Sudan, Malaysia, Uturuki, Yemen, Kenya, Burundi na Uingereza.

Nafasi ya pili imechukuliwa na Gaffari Mohammed (14), kutoka Uingereza ambaye ameibuka na kitita cha dola za Marekani 4,000. Mashindano hayo yaliyoandaliwa na Jumuiya ya Kuhifadhisha Quran Tanzania, mwaka huu yalishirikisha vijana 10 kutoka nchi 10 duniani.

Tuzo hizo zimetolewa jana wakati wa kilele cha mashindano ya 27 ya Kimataifa ya Kuhifadhi na Kusoma Qur'an tukufu na

INAENDELEA UK.8



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF tatueni kasoro hizi kabla ya msimu kuanza

**BAADA** ya miezi tisa migumu ya mshikemshike wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hatimaye ligi hiyo itafikia ukingoni kesho, Jumanne kwa timu zote 20 kushuka dimbani katika viwanja 10 tofauti.

Ligi hiyo inafikia ukingoni kesho wakati Simba ikiwa tayari imetwaa ubingwa huo kufuatia Jumanne iliyopita kujihakikishia kombe hilo kwa kuifunga Singida United na kufikisha alama 91 ambazo zisingeweza kufikiwa na timu yoyote ile kabla ya Jumamosi kuongeza pointi moja na kuwa 92 baada ya kutoka sare ya bao 1-1 na Biashara United katika Uwanja wa Taifa.

Simba ilitwaa ubingwa huo ikiwa na mechi mbili mkononi, lakini pia wakijihakikishia taji hilo kwa mara ya pili mfululizo katika Uwanja wa Namfua kwa kuifunga Singida United.

Aidha, katika ligi hiyo ambayo kwa mara ya pili mfululizo pia Yanga imemaliza nafasi ya pili, African Lyon tayari imeshuka daraja, huku kesho hatima ya timu moja itakayoungana nayo na mbili zitakazocheza mechi za mchujo (play off) kujua ama zitashuka au kubakia Ligi Kuu msimu ujao zikitarajiwa kujulikana. Hata hivyo, tumeshuhudia ligi ngumu na iliyomalizika ikiwa na changamoto nyingi moja kubwa ikiwa ni kukosekana kwa mdhamini mkuu pamoja na pangua pangua ya ratiba na 'gonjwa' la kuvurunda kwa waamuzi.

Kwa upande wa ratiba, tumeishuhudia Simba pamoja na kukabiliwa na mechi za kimataifa kwa kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikibaki nyuma kwa kuwa na viporo takriban 10.

Lakini wakati huo huo ilipotolewa kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), ikilazimika kucheza baadhi ya mechi zake za viporo ndani ya saa 48 kinyume cha kanuni za Fifa zinazotaka kuwapo na tofauti ya saa 72 kati ya mchezo mmoja hadi mwingine.

Pia, pamoja na changamoto za hali ngumu kifedha kwa klabu nyingi, bado Shirikisho la Soka nchini (TFF), likashindwa kuandaa ratiba rafiki kwa klabu ili kuzirahisishia gharama za usafiri na malazi. Mfano Yanga ilitoka Kagera na kwenda kucheza na Alliance CCM Kirumba Mwanza na kurejea kucheza Dar es Salaam kabla ya baadaye kwenda Musoma kuivaa Biashara United.

Huo ni moja ya mfano kati ya mingi kwenye ratiba mbovu isiyojali maslahi ya timu ambazo zinajiendesha kwa kujikongoja, kwani Yanga baada ya kucheza na Alliance ingeweza kuunganisha kuifuata Biashara United mjini Musoma kabla ya kurejea Dar es Salaam. Tunatambua si zaidi ya timu tatu zinazoshiriki Ligi Kuu kati ya 20 zenye uwezo wa kutumia usafiri wa ndege, hivyo ukichangia na umbali kutoka Kituo A hadi B, ni wazi kwa usafiri wa basi ratiba haikuwa rafiki kabisa kwa wachezaji na klabu. Kwa upande wa waamuzi, Nipashe tunaamini tatizo hili mbali na semina za mara kwa mara kwa ajili ya kuwapiga msasa kwa kukumbushana sheria 17 za soka, lakini kuboreshewa maslahi yao kunaweza kuwa suluhisho. Ni wazi kutokana na posho ndogo wanazozipata, waamuzi ni rahisi kushawishiwa na klabu zinazohitaji matokeo na kisha kuzifinyanga sheria 17 za soka kwa makusudi kabisa.

Hivyo, kinachotakiwa kwa TFF ni kutizama upya maslahi ya waamuzi ili kuweza kupunguza ushawishi wa rushwa katika ligi hiyo pamoja na ile ya Ligi Daraja la Kwanza ambayo inaonekana kusahaulika kwa kumulikwa mara kwa mara.

Tunahitaji kuona soka la kuvutia na ushindani ukiongezeka, hivyo ni wakati sasa kwa TFF kujipanga upya na kutizama wapi ilikosea hususan suala la ratiba, mdhamini na gonjwa hili sugu la kuvurunda kwa waamuzi. Hatutarajii kuona tena katika msimu mpya wa 2019/20 matatizo ama kasoro kama hizo zikijitokeza na kuzifanya baadhi ya klabu, makocha, wachezaji, wadau wa soka na zaidi mashabiki kuamini kwamba zipo baadhi ya timu zinabebwa ama zimeshaandaliwa kuwa bingwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# Wasiojua ndio wanaomshangaa Salamba

Na Adam Fungamwango

**AMA** kweli ukishangaa ya Mussa utayaona ya Firauni. Kwenye dunia hii tunayoishi kuna kizazi kiliwahi kuishi bila kuona teknolojia ya televisheni wala simu za mkononi.

Hapa Tanzania Bara tu, kwenye miaka ya 80' hakukuwapo na televisheni wala simu za mkononi, hivyo walioishi miaka hiyo kwenda nyuma walikufa bila kukutana na teknolojia hiyo.

Kuna kizazi kingine, ambacho ndicho hiki chetu. Hiki kimewahi kuishi wakati hakukuwa na televisheni wala simu, lakini teknolojia hii imewakuta.

Kizazi hiki ndicho kilichopata bahati ya kuishi kwenye mazingira yote mawili, kipindi hicho ambacho hakukuwa na mambo hayo, lakini kipindi hiki ambacho kuna utandawazi na kuangalia TV, pia kumiliki au kuwa kwenye dunia ya watu wanaomiliki simu za mkononi.

Pia kipo kizazi cha sasa ambacho chenyewe kimezaliwa moja kwa moja na kukuta teknolojia hii.

Na hawa ukiwaambia jinsi watu walivyokuwa wakiishi zamani bila kuangalia TV wala kuwa na simu wa mkononi wanashangaa na kuona hawa watu walikuwa wanaishije? Pia wanaona kama maisha ya watu hao yalikuwa magumu bila vitu hivyo.

Cha ajabu ni kwamba kuna baadhi wa kizazi hiki hiki cha teknolojia wana mawazo kama ya wale ambao waliishi enzi ambazo hakuna TV wala simu.

Baada ya mechi ya kirafiki kati ya Simba na Sevilla ya Hispania, kuna kitendo kilifanywa na mchezaji wa Simba, Adam Salamba kumuomba mchezaji nyota kabisa nchini Argentina anayeichezea klabu hiyo, Ever Banega kiatu alichochezea mechi hiyo, kimefanywa kama ndiyo tukio kubwa kuliko mechi yenyewe.

Hapa sina hata haja ya kufafanua ni kwa nini Salamba inaeleweka kabisa kuwa alicheza na mchezaji mkubwa kabisa duniani na kwake ni ndoto kucheza na mtu kama huyo, hivyo alihitaji kumbukumbu yake na hata kuwawekea wajukuu zake wapate tambua kuwa babu yao alikuwa mchezaji wa kiwango kikubwa kiasi cha kucheza na mchezaji huyo.

Ninachoshangaa mimi ni kwa nini baadhi ya mashabiki wa kizazi hiki wameifanya inshu hiyo imekuwa kubwa wakati wao kila wiki wanaangalia mechi za Ligi Kuu mbalimbali nchini Ulaya na Dunia kwa ujumla wakati vitu hivi ni vya kawaida sana na vinaonekana huko kwa wenzetu?

Nisingepata shida kama wangekuwa wanajadili hili ni wale ambao waliishi enzi ambazo hakuna TV wala simu za mkononi, lakini kwa kizazi cha sasa ni aibu kubwa kujadili kitu au kumsema vibaya Salamba kwa kufanya alivyofanya kwa sababu ni jambo ambalo tunaliona hata huko kwenye nchi zilizoendelea.

Nilitegemea baada ya mechi hiyo kitakachojadiliwa, achilia mbali matokeo ya mechi ni kuwauliza wachezaji wa Simba kama wameshafanya mazungumzo na wachezaji wa Sevilla kuwauliza kama wao wanafanyaje ili kuwa kwenye ubora walionao, kuanzia mazoezi yao, chakula na vitu vingine vinavyowafanya wenzetu wacheze soka kwa muda mrefu, huku viwango vyao vikiwa pale pale.

Badala yake watu wanakwenda kujadiliana au kuzungumzia suala ambalo hata wale wa kizazi cha miaka ya 60', 70' hadi 80' ambako nchini kulikuwa hakuna TV wala simu za mkononi wasingeweza kukaa na kulifuatilia kama ni jambo la ajabu sana.

Nina uhakika kama kuna Mhispania mmoja akafuatilia mijadala hii na kutafsiriwa kwa Kiswahili angeshangaa sana na kutuona kuwa ama baadhi ya mashabiki wa soka nchini wamechelewa sana, au ni washamba wa masuala ya soka.

Suala hili la kubadilishana jezi, viatu na vitu vingine vya kimichezo ni utamaduni wa wanamichezo, hasa wachezaji na mashabiki ambao wao wanachofanya ni kwenda kuweka kumbukumbu kwenye maisha yao ya soka. Sijajua tatizo hasa ni nini? Utani, ushabiki, wivu, au kufuata mkumbo, kwa sababu hakuna cha ajabu ama kigeni chochote ambacho Salamba amekifanya.

Wamemuandama kijana wa watu mpaka ameomba radhi kwa kitu ambacho kilifaa apongezwe kwa kuwa muungwana yaani 'fair play'. Ningeungana nao kama Salamba angemchezea rafu mbaya isiyokuwa na sababu yoyote mchezaji huyo kwa sababu angekuwa si muungwana, lakini kwa hili hapana.

Kizazi cha teknolojia, kinachoona mambo yote laivu yanayofanyika Ulaya hadi huku Bongo, leo kushangaa jambo hilo ni ajabu na kweli ni aibu pia. Je, hilo lingetokea kwa wachezaji wa wa Simba kugombea viatu hivyo kama ambavyo wachezaji wa Raja Casabalanca ya Morocco walivyogombea na kugawana kiatu kimoja kimoja cha Ronaldinho, pindi walipocheza na Barcelona mechi ya kirafiki miaka iliyopita, sijui ingekuwaje? Mashabiki tubadilike.

## BARUA/MJADALA

# Nakumbushia juu ya pensheni ya wazee wote

**Mhariri**

*SERIKALI iliahidi kuwaenzi wazee wote wenye umri wa zaidi ya miaka 60 kwa kuwalipa pensheni ya Sh. 45,000 kwa mwezi kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012.*

*Kauli hiyo ilitolewa na Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda na kutangazwa na vyombo vya habari yakiwamo magazeti.*

*Wazee walifurahi jinsi serikali inavyowaandalia maisha bora uzeeni na wengine wakajawa na furaha iliyopitiliza na kuimba wimbo wa taifa na kuitukuza nchi.*

*Wakati ulipofika, wazee walikwenda kuuliza kwenye ofisi za vijiji, za kata na hata wilayani na za mkoa na kuambulia kuwa hakuna taarifa yoyote kuhusu malipo hayo.*

*Wakati wazee wakiendelea kufuatilia walichokuwa wameahidiwa mwaka wa fedha 2011/2012, serikali ikatangaza tena kupitia kwa Waziri wa Kazi na Ajira wa wakati huo, Gaudensia Kabaka kwamba wazee wa miaka 60 na zaidi nchi nzima watalipwa pensheni kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014.*


*Ahadi hii imezidi kuwaacha wazee 'solemba' maana hakuna maelekezo kwamba watalipwa lini, kiasi gani wala na mamlaka zipi?*

*Baada ya wazee kuahidiwa mara mbili bila utekelezaji, serikali ikatangaza tena kwa mara ya tatu kupitia kwa Naibu Waziri wa Fedha, Dk. Ashatu Kajaji kwamba serikali itatenga bajeti maalum na itaanza kuwalipa pensheni wazee wa umri wa zaidi ya miaka 60 kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017.*

*Ahadi hii ilitangazwa na vyombo vya habari likiwamo gazeti la Nipashe la Februari 15, 2016. Hapa tena hakuna utaratibu uliotolewa kwamba ni wapi watalipwa na kiasi gani.*

*Pamoja na hayo, bado wazee wanayo imani kubwa kwa serikali yao na wanaiunga mkono kwa dhati; hivyo ili kudumisha hiyo imani ni vizuri kutimiza ahadi hii muhimu kwa kundi hili la watu waliolifanyia kazi kubwa taifa hili enzi za ujana wao.*

*Wako*
**Samson Kissenge**
**Usangi, Mwanga**
**Maoni: 0784- 227 487**




# Nafasi tatu Ligi Kuu ziwe za kimataifa msimu ujao

**Na Adam Fungamwango**

FAIDA ambayo Tanzania imeipata msimu huu kwenye nyanja za michezo ni timu ya Taifa, Taifa Stars kutinga Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), na vile vile timu ya Simba kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba imesababisha Tanzania kupata nafasi nne za uwakilishi mechi za kimataifa msimu wa 2020/2021. Na washindi hao watapatikana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kuanzia msimu ujao wa 2019/2020.

Timu mbili zinatakiwa zicheze Ligi ya Mabingwa Afrika na nyingine mbili Kombe la Shirikisho Barani Afrika (Caf).

Hata hivyo, itategemea na Shirikisho la Soka nchini (TFF), itatumia mfumo gani kuwapata wawakilishi hao wanne. Rais wa TFF, Wallace Karia, alikaririwa akisema kuwa hadi sasa hawajakaa kuangalia ni vipi watatengeneza mfumo wa kupata timu nne ambazo zitaiwakilisha Tanzania kwenye mechi za kimataifa.

Kwa sasa mfumo uliopo ni kwamba bingwa ndiye anaiwakilisha Bongo kwenye Ligi ya Mabingwa na Mshindi au bingwa wa Kombe la Shirikisho nchini (TFF), maarufu kama Kombe la FA, ndiye anayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (Caf).

Hii ni kwa sababu mpaka sasa Tanzania inapeleka timu mbili tu, yaani moja Ligi ya Mabingwa na moja Shirikisho.

Kwenye mjadala huu natoa ushauri kwa TFF kutokaa na kumiza kichwa sana jinsi gani ya kuwapata wawakilishi wanne, badala yake waipe thamani Ligi Kuu Tanzania Bara itoe wawakilishi watatu kwenda kwenye mechi za kimataifa.

Nina maana kuwa Bingwa wa Ligi Kuu na mshindi wa pili wawakilishe Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na mshindi wa tatu moja kwa moja aiwakilishe nchi kwenye Kombe la Shirikisho, aungane na Bingwa wa Kombe la FA naye acheze Shirikisho. Hapa tayari nchi itakuwa imepata wawakilishi wake wanne kwenye michuano hiyo.

TFF isitafute michuano mingine au kutengeneza vitu ambavyo vitazidi kuifanya ligi isiwe na mvuto wala thamani.

Kwa sasa Ligi Kuu ina timu 20 ambazo ni nyingi, lakini anayetafutwa ni bingwa mmoja tu na tumeona timu moja au mbili zikishakuwa na pointi nyingi kuliko zingine, msisimko unapotea.


Kwa maana hiyo, zikitafutwa nafasi tatu kati ya timu 20 zinazocheza Ligi Kuu, nadhani itakuwa na mvuto wa hali ya juu kwani hata kama kuna timu ambayo itakuwa na pointi nyingi na kukaribia ubingwa, bado kutakuwa na timu zinapambana ili kupata nafasi ya pili na ya tatu kwa ajili ya kuiwakilisha nchi, hivyo ligi kuendelea kuwa ngumu na bora zaidi.

Hapo hata timu inayosaka ubingwa inaweza kuwa na wakati mgumu ikipambana na timu ambayo inatafuta nafasi angalau ya tatu kwa ajili ya kucheza Kombe la Shirikisho.

Mifano tunaona kwenye Ligi Kuu ya England ambapo mbali na vita ya ubingwa, lakini kuna nyingine ya nne bora maarufu kama 'top four' na hiyo inaifanya kuwa ngumu na isiyotabirika.

Kuanzia msimu ujao ambapo zitaanza kutafutwa timu nne, nashauri Ligi Kuu sasa iwe ya 'top three', yaani timu tatu za juu ziende kucheza mechi za kimataifa, mbili Ligi ya Mabingwa na moja Shirikisho, hapo hata TFF yenyewe itaona jinsi gani ligi itakavyokuwa ya ushindani, na inaweza kabisa kusababisha hata kupata wadhamini na klabu zikaanza kunufaika.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Watanzania 2 washinda tuzo ya kimataifa Qur'an

INATOKA UK. 5

utoaji tuzo yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na mamia ya waumini wa Kiislamu waliofurika kushuhudia kilele cha Tuzo ya Kimataifa ya Quran iliyoandaliwa na Jumuiya ya Kuhifadhisha Quran nchini, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesema kuhifadhisha Quran kunapaswa kuwa msingi imara katika kujenga jamii bora.

Aliwataka wazazi wa Kiislamu wahakikishe wanawasimamia vema watoto wao na kuwahifadhisha Qur'an badala ya kutoa msukumo pekee kwenye elimu ya kimazingira. "Sote ni mashahidi kwamba vijana wetu wanao uwezo wa kuhifadhi Qur'an na wakati huohuo wakasoma na kuhitimu fani mbalimbali katika elimu ya mazingira."

Alisema njia mojawapo ya kuwasaidia vijana kukabiliana na hali ya sasa ya dunia ya utandawazi ni kuwasomesha na kuwahifadhisha Qur'an. "Vijana waliosoma na kuhifadhi ni vigumu kuenenda kinyume na maadili kwani ndiyo njia pekee ya kuwachunga na kuwafanya waonyeke dhidi ya vitendo vinavyokwenda kinyume na uadilifu."

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameipongeza Jumuiya ya Kuhifadhisha Qur'an nchini kwa kuendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mwongozo na msingi wa maisha yao kupitia kitabu hicho kwa kuwa kufanya hivyo wanakuwa wanawaongezea vijana hao uelewa sahihi wa dini yao na elimu ya kutosha ya mazingira (yaani circular education).

Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir bin Ali, alisema tuzo za jana zimethibitisha kuwa kusoma elimu ya mazingira hakuharibu elimu ya dini. "Iwe changamoto kwa Waislamu kwamba msingi wa elimu ya dini hauchafui elimu ya dini, kwani kuna watu hawataki kusoma elimu ya mazingira kwa kisingizio kuwa Mtume hakusoma, sasa Mtume atasoma kila kitu?" Alihoji.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kuhifadhisha Qur'an Tanzania, Sheikh Othman Ali Kaporo, alisema walilazimika kuanzisha taasisi ili kuwafundisha vijana maadili mema kwa kuwa miaka ya 80 - 90 ilikuwa shida kumpata kijana mwenye uwezo wa kuhifadhi hata juzuu tatu tu.



Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Idara ya M-Commerce, Epimack Mbeteni (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Amana Bank, Dk. Muhsin Masoud, wakizindua huduma mpya ya Halal Pesa ambayo inaambatana na sheria za Kiislam jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na mtandao wa M-Pesa ili kuleta faida kwa wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Wiki ya Kabudi, makinikia, Stiegler's Gorge bungeni

INATOKA UK. 3

na mambo mengine, bungeni kutakuwa na mjadala wa siku moja wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Katika mjadala huo, tuhuma dhidi ya Waziri Kabudi kwamba ameishauri vibaya serikali katika utungaji wa Sheria ya Takwimu na kushughulikia suala la makinikia, zinatarajiwa kuendelea kuelekezwa kwake na baadhi ya wabunge, huku waziri huyo akitarajiwa kuzijibu baadaye leo jioni.

Tuhuma hizo ziliibuka wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka ujao wa fedha na ziliendelea wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikimtaka Waziri Kabudi kujiuzulu kwa kile inachodai ameishauri vibaya serikali katika utungaji wa Sheria ya Takwimu na wakati wa kushughulikia masuala mbalimbali ya kisheria likiwamo sakata la makinikia na uingiaji wa mkataba kati ya serikali na Kampuni ya Indo Power Solutions ya Kenya kununua korosho zilizokusanywa na serikali kutoka kwa wakulima. Ratiba ya vikao vya mkutano wa Bunge la Bajeti inaonyesha kuwa kesho na keshokutwa, kutakuwa na mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nishati. Mradi wa Stiegler's Gorge unatarajiwa 'kuuteka' mjadala huo kutokana na utekelezwaji wake kutoungwa mkono na upinzani.

Wiki iliyopita, Mbunge wa Viti Maalum, Catherine Ruge (Chadema), aliingia matatani bungeni baada ya kupinga utekelezaji wa mradi huo.

Wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka ujao wa fedha, Ruge alijikuta akitakiwa kuwasilisha ushahidi kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Jumatano (keshokutwa) baada ya kupinga mradi huo na serikali kudai kwamba hoja zake hazina ukweli.

Katika mjadala huo, alisema Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauona mradi wa Stiegler's Gorge kama diwani ya 'Songs of Lawino and Okol', akisisitiza kuwa Watanzania wanapaswa kutambua una madhara na hautawanufaisha.

Ruge alisema gharama za utekelezaji wake hazielezeki huku akinukuu taarifa ya msomi aitwaye Jorge Hitman, ambaye alisema utatekelezwa kwa gharama ya Sh. trilioni 21 wakati serikali ikieleza kuwa utagharimu takribani Sh. trilioni 10.

Aliongeza utekelezaji wa mradi huo pia utaathiri watu zaidi ya 500,000 wanaoishi pembezoni mwa Bonde la Mto Rufiji na Hifadhi ya Selous.

Wakati Ruge anaendelea kuwasilisha mchango wake bungeni, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisimama na kuomba kutoa taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 64 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayoelekeza kuwa mbunge hatatoa bungeni taarifa yoyote ya uongo.

Mgalu alisema Ruge ametoa taarifa ya uongo wakati anachangia kuhusu Stieger's Gorge kwa kuwa mradi huo ulifanyiwa tathmini, tenda ilitangazwa na makandarasi waliomba kuutekeleza.

Ruge amekuwa mbunge wa pili kutakiwa kuwasilisha ushahidi wa hoja zake tangu kuanza kwa Bunge la Bajeti Aprili 2, mwaka huu, akiungana na Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe (Chadema), ambaye wiki iiyopita aliwasilisha ushahidi kwa Kamati ya Maadili kuhusu madai yake kwamba Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, amekuwa akiwaomba rushwa wawekezaji.

Ikiwa ushahidi wa wabunge hao hautairidhisha Kamati ya Maadili, watakuwa hatarini kufungiwa kuhudhuria vikao kuanzia vitatu hadi 10 vya Bunge kwa mujibu wa kanuni za chombo hicho.

Mbunge aliyefungiwa, hutakiwa kutokanyaga kwenye maeneo ya Bunge jijini Dodoma na ofisi za taasisi hiyo zilizoko jijini Dar es Salaam, huku akilipwa nusu posho na mshahara kwa kipindi chote cha kifungo chake.

Ratiba ya mkutano wa Bunge la Bajeti inaonyesha Alhamisi kutakuwa na mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Madini. Katika mjadala huo, serikali inatarajiwa kulieleza Bunge manufaa yaliyopatikana kutokana na hatua mbalimbali ilizozichukua hivi karibuni kuimarisha udhibiti wa sekta ya madini nchini.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Ijumaa kutakuwa na mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Katika mjadala huo, serikali inatarajiwa kulieleza Bunge mafanikio ya mkakati wa wizara kukabiliana na migogoro ya ardhi, huku wabunge wakitarajiwa kuhoji uamuzi wa serikali kupoka mashamba makubwa yaliyokuwa yakimilikiwa na wafanyabiashara wakubwa na viongozi wakiwamo Mohamed Dewji 'Mo' na Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye.

Ratiba ya vikao vya Bunge la Bajeti inaonyesha mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara hiyo inayoongozwa na Waziri William Lukuvi, utahitimishwa Jumatatu ijayo.

# Mbunge ataka gesi bungeni

INATOKA UK. 2

mradi huu utatekelezwa kwa miaka 12 au tisa gharama zingekwenda mpaka Sh. trilioni 22.95.

Aliongeza: "Ni vizuri mkataba ukaletwa bungeni ili tujue ni miujiza gani iliyowekwa sasa hivi kwenye mkataba ambao unafanya mradi ambao serikali awali ilisema ungetekelezwa kwa miaka tisa awamu ya kwanza, miaka mitatu na awamu ya pili na kufanya jumla kuwa miaka 12.

"Tunataka hii siri ijulikane bungeni, tunataka kuuona mkataba wa mradi huu na kuupitia kipengele kwa kipengele, miaka ya nyuma walipenda mikataba ipelekwe bungeni, lakini kutokana na kutokuwa na sheria haikuwezekana, wametunga sheria wenyewe yenye kuruhusu mikataba mikubwa inayohusu rasilimali za nchi ije bungeni," alisema.

Kuhusu uwekaji jiwe mwezi Julai, mwaka huu, ili kuruhusu utekelezaji wake, Mnyika katika hotuba ya waziri ya mwaka jana iliahidi uzinduzi ungefanyika mwezi Julai mwaka huo na ziliwekwa Sh. bilioni 700 ili mkandarasi alipwe asilimia 15 ya mradi mzima ili kazi ianze. Mnyika alisema wanataka pia ripoti ya tathmini za kimazingira iliyofanyika, iwasilishwe bungeni ili Bunge lione athari.

Kuhusu gesi, Mnyika alisema serikali iliingia kwenye gharama za ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam kwa gharama ya dola za kimarekani bilioni 1.283 (Sh. trilioni 2.5) ambapo sehemu ya fedha hizo, dola za kimarekani bilioni 1.225 zilikopwa benki ya Exim ya China.

Mnyika alitaka serikali kesho iwasilishe bungeni mikataba yote ya bomba la mafuta ili bunge iipitie na kujua athari ambazo taifa inazipata kutokana na mikataba hiyo.

Alisema mpaka sasa kiwango cha gesi kinachopita kwenye bomba hilo ambalo limejengwa kwa gharama kubwa ni asilimia 6 kinachotumiwa na Tanesco na asilimia ndogo kwa maeneo mengine huku sehemu kubwa ya gesi haipiti.

Mnyika aliitaka serikali ieleze kwa nini imeachana na uchumi wa gesi na kuitaka iwasilishe bungeni mikataba yote ya ujenzi wa bomba la mafuta, mikopo na iliyoambatana nalo.

Kuhusu sintofahamu iliyojitokeza kipindi kile gesi iliyosababisha Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda, kuunda kamati iliyokwenda Mtwara kuchunguza na baadaye kuiwasilisha serikalini, Mnyika alitaka nayo iwasilishwe siku hiyo.

"Kuna kamati zilizoundwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai kupitia mikataba mbalimbali ya mafuta na gesi ambayo nayo tunataka iwasilishwe bungeni.

"Serikali itakaposoma bajeti yake bungeni ieleze pendekezo kwa pendekezo yaliyokuwa kwenye ripoti ya uchunguzi iliyoundwa na Spika kuhusu gesi na Spika Ndugai awezeshe tupewe nakala ya hiyo ripoti ili tupime kati ya maelezo ya serikali na utekelezaji halisi uliofanywa na serikali tupo katika hatua gani kuhusu gesi," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Vijiji 226 vyatangaziwa neema bomba la mafuta

**Na Mwandishi Wetu,** NZEGA

WANANCHI wanaoishi vijiji linakopita bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanzania, watanufaika na mradi huo kufuatia serikali kutangaza mradi wa kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji 226 linapopita bomba hilo.

Aidha, imeelezwa kuwa wakati wa utekelezaji mradi wa kupanga matumizi bora ya ardhi mwananchi hawatatozwa gharama yoyote na wale ambao maeneo yao yametwaliwa watalipwa fidia.

Hayo yalibainishwa juzi katika kijiji cha Sojo, kata ya Igusule, Wilaya ya Nzega mkoani Tabora na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, wakati wa uzinduzi mradi wa upangaji matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinavyopitiwa na bomba la kusafirisha mafuta ghafi -EACOP alipozungumza na wananchi wa kijiji hicho kuwaelezea mpango wa wizara yake kupanga matumizi bora ya ardhi ili kuendana na fursa za kiuchumi.

"Vijiji vyote 226 ambavyo bomba la mafuta linapita ardhi yao itafanyiwa matumizi bora ya ardhi ili kutoa fursa za kiuchumi kwa wananchi wanaoishi katika vijiji hivyo," alisema Lukuvi.

Akiwa na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na baadhi ya wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi na Maliasili, Waziri Lukuvi, alisema, uzinduzi uliofanyika ni kwa niaba ya vijiii 226 na wilaya 24 zilizoko katika mikoa nane inapopita bomba hilo na kubainisha kuwa fedha kwa ajili ya mpango huo zishatengwa.

Waziri Lukuvi alitoa onyo kwa wananchi watakaojipenyeza au kufanya maendeleo katika eneo la ekari 144 lililotwaliwa na serikali na kusema picha ya anga imechukuliwa katika eneo lote litakalojengwa kituo wezeshi cha kuunganisha mabomba ya mradi.

Kwa mijibu wa Lukuvi, mradi wa upangaji matumizi ya ardhi katika vijiji vinavyopitiwa na bomba la mafuta utakuwa shirikishi kwa kuwahusisha wananchi wanaoishi maeneo hayo.

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Dk. Stephen Nindi, alisema kazi ya upangaji matumizi bora ya ardhi imeanza katika vijiji, miji na miji midogo inayopitiwa na bomba la kusafirisha mafuta ghafi ambapo kazi hiyo imeanza katika wilaya 13 kati ya 24 zilizopangwa kufanyiwa matumizi bora ya ardhi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Coca-Cola Kwanza, Basil Gadzios, akiwaongoza wafanyakazi wa kampuni hiyo pamoja na wateja kwenye futari iliyoandaliwa na Coca-Cola Kwanza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kwa ajili ya wateja wake. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wachimba visima vya maji wapewa angalizo

**Na Frank Monyo**

OFISA wa Maji Bonde la Wami/Ruvu, Simon Ngonyani, ameeleza kuwa kufuatia agizo la serikali la kufuta tozo ya visima vya maji kwa watumiaji binafsi kwa matumizi ya majumbani, hakuhalalishi watu kuchimba visima ovyo bila kufuata sheria kwa kuwa ni hatari kwa afya zao.

Aidha, amewatahadharisha wamiliki wa visima vya maji kwa ajili ya biashara kulipa ada ya matumizi ya maji chini ya ardhi na kuacha kutumia katazo la serikali kuleta usumbufu kwa sababu agizo hilo haliwahusu.

Alitoa kauli hiyo jana, jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa wao kama wasimamizi wa maji chini ya ardhi, wamepokea agizo la serikali na kwamba wanawashauri wamiliki wa visima na ambao wanataka kuchimba k ufika katika ofisi za bonde kwa ajili ya kupewa ushauri na kukutana na wataalamu ambao watawaonyesha sehemu sahihi ya kuchimba. "Sisi kama wataalamu tunawashauri kwamba bado wafuate utaratibu kwa kuwa kuchimba visima kiholelea si jambo zuri kwa afya zao... hata kama wakichimba hawalipi, lakini hii ya kutolipa haiwaondolei kwamba ni salama waje waombe vibali ili tufahamu nani anachimba wapi, vinginevyo tutachimba hadi kwenye mashimo ya choo na matokeo yake ni hatari kwa afya zao pia," alisema Ngonyani.

Alisema watu ambao wanachimba visima kiholela hasa kipindi hiki cha mvua, wanakuwa katika hatari za kupata magojwa ya mlipuko kwa kuwa uchafu unaosombwa na maji ya mvua unaweza kupelekwa hadi kwenye visima kutokana na kutochimbwa kitaalamu.

Aliongeza kuwa wapo watu ambao wanafanya biashara ya maji kutoka chini ya ardhi, baadhi yao wamekuwa wasumbufu kulipa ada ya matumizi ya maji hayo, hivyo sheria itafuata mkondo wake ikiwano kufikishwa mahakamani.

"Kuna watu wamechimba visima kwenye nyumba zao ambao wanafanya biashara ya kuuza maji, tozo iliyofutwa na serikali haiwahusu kabisa nyie ni wafanyabiashara, mnatakiwa kulipa tozo na niwatake tu msitumie mgongo huu wa watumiaji wa maji majumbani kukwepa kulipa tozo hatutawaelewa," alisema Ngonyani alisema kuwa kwa wale wamiliki wa hotel, vituo vya mafuta, nyumba za kulala wageni, ambao hawajalipa tozo za maji wanapaswa kulipa ili kuepuka kupelekwa mahakamani.

# Ajinyonga kisa ugomvi na mke

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MWANAUME aliyefahamika kwa jina la Anthony Masala (49), mkazi wa kitongoji cha Mang'o B kijiji cha Kanazi kata Ntatumbila wilayani Nkasi mkoani Rukwa, amekufa kwa kujinyonga kwa kamba kutokana na hofu ya kukamatwa na polisi baada ya ugomvi na mkewe.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ntatumbila, Given Kisantola, tukio hilo lilibainika jana asubuhi baada ya kukutwa maiti ya mtu huyo ikining'inia juu ya mti kwa kamba ya katani.

Alisema chanzo cha kujinyonga hakijajulikani ila inaelezwa na ndugu za marehemu siku moja kabla ya tukio hilo ugomvi kati yake na mkewe ugomvi ulioanzia kilabuni walipokuwa wakinywa pombe.

Alidai wanandoa hao walianzia ugomvi wao kilabuni ambapo mwanaume alikuwa akimtuhumu mkewe kuwa amekuwa akimsaliti, ugomvi ambao uliendelea hadi nyumbani kwao na ndipo mwanamke alipoamua kukimbia na kwenda kwao.

Kwamba kutokana na kudhani mkewe amekwenda kutoa taarifa polisi kuwa anafanyiwa fujo ikizingatiwa kuwa mwanamke huyo alikua ni mjamzito, ndipo alipoamua kujinyonga.

Diwani wa kata hiyo, Leonard Maasai, alisema marehemu huyo alijinyonga kwenye mti uliopo umbali wa mita 100 kutoka nyumbani kwake na kuwa licha ya kuwa hakuacha ujumbe wowote isipokuwa majirani wanasema alifikia maamuzi hayo ili kukwepa kukamatwa na polisi.

Katibu Tawala wa Wilaya Nkasi, Cosmas Kuyela, alithibitisha kupokea taarifa hizo.

Jeshi la Polisi limethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kushauri kuwa migogoro iwe inatafutiwa ufumbuzi haraka kabla ya kugharimu maisha ya watu.

# TGNP yapigania hedhi salama kwa wanawake, wasichana

**Na Yasmine Protace**

MATATIZO mengi ya wanawake kuhusiana na uzazi, yanasababishwa na kushindwa kukabiliana na hedhi kwa njia salama haswa walipokuwa katika umri mdogo.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, wakati wa ufunguzi wa mdahalo wa maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama, ambao ulifanyika jijini Dar es Salaam.

Mdahalo huo wa siku moja ulihudhuriwa na madiwani, maofisa kutoka halmashauri, walimu wa shule za msingi na sekondari, wadau kutoka asasi za kiraia na wanafunzi.

Liundi alisema siku ya hedhi ni siku ya kimataifa ya kujenga uelewa na kupasa sauti juu ya upatikanaji wa huduma nzuri za kusaidia wanawake kuwa salama wanapokuwa kwenye hedhi.

"Siku hii inatupa fursa kujadili na kutafakari juu ya mifumo yetu kama nchi tunavyosimamia masuala ya hedhi salama, ambapo kaulimbiu ya mwaka huu ni wakati ni huu chukua hatua," alisema.

Aliongeza kuwa TGNP Mtandao katika kutekeleza kauli mbiu ya mwaka ya kimataifa, wanasisitiza na kaulimbiu yao inayosema tenga bajeti kugharamikia mahitaji ya hedhi salama shuleni.

Alisema wanaamini kwamba kama halmashauri na serikali kuu watalipa kipaumbele jambo hilo, changamoto zinazowakumba wasichana shuleni na wanawake juu ya ukosefu wa nyenzo za hedhi salama zitapungua.

Liundi aliongeza kuwa Umoja wa Mataifa uliipa uzito wa kipekee siku hiyo, baada ya kuona kwamba nchi zinazoendelea mwanamke akiwa katika hedhi anapata tabu zaidi kwa sababu vifaa vya kujisitili vina gharama kubwa ambazo hawawezi kumudu.

Alisema lengo la TGNP Mtandao kukutana na wadau ni kujenga utamaduni wa kuvunja ukimya, kuondoa woga wa kusema wazi wazi juu ya changamoto zinazowakabili wanawake wakiwa kwenye hedhi hasa watoto wa shule za msingi na sekondari.

Anaongeza kuwa TGNP Mtandao inaendelea na kampeni yao ya wape mabawa ambayo lengo lake ni kuhakikisha wasichana wanapata mazingira salama ya kupata elimu, ambayo ni kuvunja ukimya, ushawishi watunga sera watenge bajeti za kutosha kuwezesha upatikanaji wa taulo za kike na vifaa vingine kama matundu ya kutosha ya vyoo, upatikanaji wa majisafi na salama.



Meneja Mkazi wa Kampuni ya Shell Tanzania, Axel Knospe (wanne kulia), akimkabidhi kadi ya gari la kubebea wagonjwa Mkuu wa Wilaya ya Lindi Mjini, Shaidi Ndemanga aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi kwa ajili ya Hospitali ya Mkoa mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Shell yapiga jeki gari la wagonjwa hospitali mkoa

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

KAMPUNI ya gesi ya Shell Tanzania, jana ilikabidhi gari ya kubebea wagonjwa kwa Hospitali ya Sokoine, ambayo ni ya Mkoa wa Lindi.

Akipokea gari hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, aliishukuru Kampuni ya Shell na kueleza kwamba kampuni hiyo imefanya jambo kubwa linaloweza kusaidia kuokoa maisha ya wakazi wa Mkoa wa Lindi.

"Tulikuwa na uhitaji mkubwa wa gari ya kubebea wagonjwa katika hospitali hii ya mkoa. Sasa gari tumeipata. Tunawashukuru sana," alisema Ndemanga na kuahidi kulitunza gari hilo.

"Tutahakikisha gari hili linatunzwa na linafanya tu kazi iliyokusudiwa," aliongeza.

Amesema serikali inatambua mchango wa Shell katika kuisaidia jamii na kuongeza kwamba kampuni hiyo iko mstari wa mbele katika kufikisha kwa Watanzania aina mbalimbali za nishati mbadala. Katika hafla hiyo, Meneja Mawasiliano wa Shell Tanzania, Patricia Mhondo, alisema Mkoa wa Lindi unaendelea kuwa na ongezeko la watu, pia mahitaji ya kiafya yanaongezeka. "Tumetoa gari hii kwa kuzingatia haya yote," aliongeza Mhondo. Alisema Hospitali ya Sokoine inahudumia wagonjwa wengi na kwa hiyo mahitaji ya gari la kubebea wagonjwa ni dhahiri.

# NEMC yajipanga mazingira duniani

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku chache kabla ya kusherehekea Siku ya Mazingira Duniani, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), linatarajia kukutana na wadau wa mazingira ili kuleta maana ya siku hiyo nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema wataitumia siku hiyo kwa kushirikiana na wadau kuweka mazingira katika hali ya usafi na salama.

"NEMC tumejipanga kukutana na wadau wote ili kuweka mikakati na kuona maeneo gani yapewe kipaumbele katika kuhakikisha mazingira yetu yanaendelea kuwa rafiki nchi nzima," alisema Dk. Gwamaka.

Mbali na wadau, uongozi wa NEMC kwa kushirikiana na wafanyakazi wa baraza hilo, wamejipanga kuitumia siku hiyo kwa kufanya usafi katika maeneo ya pembezoni mwa bahari, hospitalini pamoja na katika shule mbalimbali.

"Uongozi kwa kushirikiana na wafanyakazi wa NEMC tumedharia kuitumia siku hiyo kwa kuwaongoza Watanzania kwa kufanya usafi katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye fukwe za bahari, hospitalini na katika shule mbalimbali," alisema Dk. Gwamaka.

Alieleza namna NEMC ilivyojipanga kuitumia siku hiyo katika kutoa elimu ya mazingira katika shule za msingi na sekondari ili kuwajengea wanafunzi uelewa mpana wa masuala ya mazingira

"Tutaitumia siku hiyo kutoa elimu katika shule zetu nchini kuhusu faida ya kutunza mazingira kwa vizazi vilivyopo na vijavyo ili nao kwa kupata uelewa huo wataenda kuwa mabalozi wazuri kwa jamii pana ya Watanzania, alisema na kuongeza: "Elimu ni njia pekee katika kuyafanya mazingira yetu yawe bora na yenye kuleta tija kwa viumbe vinavyoishi katika mazingira hayo wakiwamo binadamu."

Dk. Gwamaka alitoa wito kwa wadau wote wa mazingira wapende mazingira ili nayo yaweza kuwatunza.

"Mazingira ni sekta mtambuka, hivyo nitumie nafasi hii kuwaomba wadau wote kuyatunza mazingira na kwa kufanya hivyo nayo yatatunza na kutuletea tija kubwa leo na siku za baadaye," alisisitiza.

Siku ya Mazingira Duniani husherehekewa Juni 5 ya kila mwaka na kwa mara ya kwanza maadhimisho hayo yalifanyika mwaka 1974 Marekani na tangu hapo mataifa mengi yamekuwa yakiadhimisha siku hiyo kila mwaka, huku kukiwa na kauli mbiu tofauti tofauti na kwa mwaka huu yanatarajia kufanyika China na kauli mbiu ni 'Air Pollution' (uchafuzi wa hewa).

# Ole Nasha asafishiwa njia kuelekea uchaguzi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewataka wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro kutoyumba katika uchaguzi mkuu mwakani, kwa sababu mbunge wanaye anayejali matatizo yao ambaye ni Willium Ole Nasha.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akiwasha umeme kwa mara ya kwanza wilayani humo, wakati alipokuwa akiongea na wananchi wa Kata ya Samunge na Digodigo, wilayani humo.

Dk. Kalemani alisema Ole Nasha ambaye pia ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia amekuwa mstari wa mbele tangu kuchaguliwa kwake jimboni humo katika kutetea wananchi wake juu ya maendeleo.

"Mnajua tuna vijiji na wilaya nyingi nchini, lakini leo nimekuja kwanza kwenu kuwasha umeme, sababu mbunge wenu amekuwa akinisumbua kila wakati juu ya kuleta umeme jimboni mwake ili mkafanye maendeleo, sasa msiyumbe na wengine watakaokuja kujipitisha," alisema.

Alisema Ole Nasha ataingia uchaguzi kama ilivyo ada na vyama vingine vitaruhusiwa kuchukua fomu, lakini wananchi wanafahamu mbunge anayejali shida zao ni yupi.

Pia aliwafikishia salamu zao kwa Rais John Magufuli kuwa anawajali na kuwathamini wananchi wa huko na wasione kama wametengwa, ndio sababu anawapelekea maendeleo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, akihutubia mkutano huo wa hadhara, alimshukuru Waziri Dk. Kalemani kuwaletea umeme wilayani humo ambao tangu Uhuru haujawahi kuwaka.

Alisema jambo la msingi kwa wananchi ni kuhakikisha wakati ukifika wa uchaguzi kumkumbuka aliyewaletea maendeleo hayo na kuachana na wale wanaojipitisha pitisha kutaka madaraka.

"Nyie mmemaliza uchaguzi katika jimbo lenu, sababu Ole Nasha amekuwa mstari wa mbele kuwapigania kuhakikisha maji, umeme na kila mahitaji muhimu ya mwanadamu yanafika jimboni mwake, sasa mnatafuta nini tena," alisema.

Akizungumza jimboni mwake, Naibu Waziri Willium Ole Nasha na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, aliishukuru serikali kuwaletea umeme wananchi wake na kuwataka kutumia katika uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo ili waweze kujikomboa na umaskini.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. Joseph Nyamhanga (katikati), akizungumza baada ya kukagua majengo mapya ya Kituo cha Afya Magugu wilayani Babati, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake, vijana wanolewa kuelekea uchaguzi

**Novatus Makunga,** ARUSHA

WANAWAKE na vijana wanaojipanga kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu mkuu mwakani katika mkoa wa Arusha, wametakiwa kujipanga katika kukabiliana na changamoto mbalimbali, zikiwamo za rushwa ya ngono, jamii kukosa imani nao kutokana na kutokuwa na makazi ya kudumu na kutokujiamini.

Hayo yamebainishwa na Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Mkoa wa Arusha, Anna Msuya, katika mafunzo ya kukuza ushiriki wa wanawake na vijana kwenye uongozi kutoka katika wilaya za mkoa huo, yaliyoandaliwa na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA).

Msuya alisema endapo kama kweli makundi hayo mawili yana nia ya dhati ya kushika nafasi za uongozi hususani udiwani, hawana budi kuwa na ujasiri, wajiamini na kuacha kabisa uoga, kwa kuwa wasitegemee kwamba uchaguzi huo utakuwa mwepesi.

"Lazima muwe na mkakati na mbinu za kupambana katika kupata uongozi kwenye uchaguzi huo na kwa vyovyote mtakutana na makundi ambayo yatawatisha na mengine kuwakatisha tamaa, lakini pia mtakutana na watu wenye uzoefu katika siasa," alisema.

Msuya aliwasisitiza kuwa katika kuelekea kuwania uongozi, ni vyema wakazingatia maadili na kuepuka makundi maovu na pia kuachana na tabia ambazo hazikubaliki katika jamii ikiwamo ya ulevi wa kupindukia na uzinzi.

Alisema wanawake wana changamoto kubwa zaidi kuliko vijana, kwa kuwa licha ya kuingia katika uongozi bado watalazimika kutekeleza majukumu yao ya asili ambayo aliyataja kuwa ni pamoja na kutumikia taifa, mume, watoto na jamii.

"Ni vyema kuiandaa familia kabla ya kuingia katika uongozi, tuna mifano mingi tu ya baadhi ya wanawake walioingia katika uongozi, baadaye familia zao zilivurugika na kusambaratika kabisa," alisema.

Naye mkufunzi wa mafunzo hayo ambaye ni mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Arusha, Firmin Nnko, alisema kupitia mafunzo hayo anaamini vijana na wanawake hao wameiva na hivyo katika maeneo wanayotoka kutapatikana viongozi bora ambao wataitumikia vyema jamii.

Nnko alisema vijana na wanawake hao wanaandaliwa bila kujali itikadi ya vyama vya siasa wanakotoka na akafafanua kwa kueleza kuwa katika kuhudumia jamii hahiitaji vyama, bali cha msingi ni kwa vijana na wanawake, kubeba makundi makubwa ya kuwaongoza.

Kwa upande wake mratibu wa mafunzo hayo kutoka TAWLA Mkoa wa Arusha, Silvia Mwanga, alisema mafunzo hayo yanafanyika kupitia mradi wa kukuza ushiriki wa vijana na wanawake katika uongozi (WYPRE).

"Kupitia mradi huu tumeandaa mafunzo kwa vijana na wanawake wanaoonyesha nia ya kutaka kugombea nafasi za uongozi na tumeanza kwa ngazi za udiwani na baadhi walishawahi kugombea katika chaguzi zilizopita," alifafanua.

Mwanga alisema katika mafunzo hayo wanajengewa uwezo wa jinsi ya kujiamini, kuongea na kujenga ushawishi kwa wapiga kura, ili waweze kuchaguliwa kutegemeana na mchango wao katika jamii.

Alizitaja changamoto kubwa walizobaini kwa wanawake ni pamoja na kutokujiamini, rushwa ya ngono na familia zao kutokupendezwa na wao kujitosa katika siasa, pamoja na vita iliyopo miongoni mwa wanawake wenyewe.

Kwa upande wa vijana, alisema changamoto kubwa ni kukosa maadili ya uongozi, kutumika zaidi kama wapiga kampeni na siyo wawania uongozi, pamoja na jamii kutowaamini kutokana na kutokuwa na maisha ya kudumu kwa kukosa familia na makazi.

Mafunzo hayo yamewashirikisha viongozi watarajiwa wa makundi ya wanawake na vijana kutoka katika Halmashauri za Wilaya ya Longido, Arusha-Wilaya, Meru, Monduli, Karatu na Arusha Jiji.

# Mbegu za mbuzi wa asili hatarini kutoweka

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAFUGAJI nchini wapo hatarini kupoteza mbegu za mbuzi wa kienyeji, baada ya wengi kuhamia kwenye ufugaji wa kisasa na kuacha ufugaji wa asili.

Hayo yalisemwa jana na Mratibu Mkuu wa mradi wa kuboresha, kuhifadhi na kuendeleza mbuzi wa asili, ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya utafiti wa mifugo Tanzania, kituo cha Tanga, Dk. Zabron Nziku, wakati akizungumza na kikundi cha wafugaji wa mbuzi weupe wa Kipare, waliotembelea kituo cha utafiti wa mifugo (TALIRI) kilichopo West Kilimanjaro kujionea shughuli za ufugaji.

Dk. Nziku alisema utafiti uliofanywa na watafiti wa mifugo wamebaini kuwapo kwa upotevu wa mbuzi wa asili ya kienyeji, kutokana na wafugaji wengi kuhamia kwenye ufugaji wa kisasa na kusahau wa asili.

Alisema lengo la mradi huo wa mwaka mmoja ni kutoa elimu na kuhamasisha ufugaji huo wa mbuzi weupe wa Kipare, ambao wana uwezo wa kuishi mazingira yote, huku wakistahimili ukame na hata magonjwa tofauti na mbuzi wengine wa kisasa."Ukifuga mbuzi hawa wa asili hutaingia gharama kubwa kama mfugaji au kama wale wanaofuga mbuzi wa kisasa," alisema.

Dk. Nziku alisema tangu kuanza kwa mradi huo, Januari mwaka huu zaidi ya wafugaji 100 wa mbuzi wamenufaika na mafunzo ya mbinu bora za ufugaji wa mbuzi hao weupe wa asili na namna ya kuhifadhi mbegu bora.

Aliushukuru Umoja wa nchi za Afrika na Umoja wa nchi za Ulaya kwa ufadhili, pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kukubali mradi huo kufanyika nchini.

Mkurugenzi wa Kituo cha utafiti wa mifugo (TALIRI) West Kilimanjaro, Dk. Athumani Nguluma, alisema kutokana na hali hiyo wafugaji wa mbuzi, wameshauriwa kutumia ufugaji wa mbuzi wa asili, ambao wapo hatarini kutoweka ili kurejesha asili iliyokuwapo hapo awali.

Aliwashauri pia kuwa na utaratibu wa kuchagua madume na majike ya mbegu yaliyo bora, wakati wa kupandisha mifugo ili vizazi vijavyo viwe bora zaidi.

# Kasi ya mafundi jamii yakuna DC

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

KASI ya mafundi jamii kutii kiu ya serikali ya kumalizwa kwa wakati kandarasi ya ujenzi wa madarasa mawili na madawati 40 ya Shule ya Msingi Sinai iliyopo Kata ya Ormelili katika Wilaya ya Siha 'umeiteka' furaha ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu.

Kiasi cha Sh. milioni 46.6 kilichotengwa kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya sekta ya elimu kimetolewa kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Akikabidhi madarasa hayo mwishoni mwa wiki pamoja na madawati 40, Buswelu alisema: "Nimeridhishwa sana na kiwango bora cha ujenzi wa madarasa haya, matundu sita ya vyoo na madawati 40. Natoa wito kwa kila shule kuiga mfano huu wa Shule ya Msingi Sinai."

"Nafikiri tunaenda vizuri, quality of work (ubora wa kazi) unanifurahisha na niwahakikishieni viongozi wenzangu na wataalamu katika wilaya yetu, mmenipa faraja sana kwa kasi hii ya ujenzi ambayo imetii kiu ya serikali. Mmesimamia vilivyo kwa kuhakikisha fedha za serikali zinatumika vizuri."

Kufuatia kauli hiyo, Ofisa Elimu ya Msingi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Rose Sandi, alimhakikishia Mkuu huyo wa Wilaya kwamba hakuna noti iliyotengwa na serikali inaweza kutumika ndivyo sivyo katika idara yake ambayo anaisimamia yeye.

Serikali ina jukumu kubwa la kuhakikisha kunakuwa na mazingira bora katika utoaji wa elimu, ambapo miradi ya namna hiyo inatekelezwa katika halmashauri nchi nzima.

Wilaya ya Siha ina shule za sekondari za kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na kidato cha tano na sita, ambazo zinawika hivi sasa katika Mkoa wa Kilimanjaro zikitishia nafasi na majina ya shule zinazosifika kitaifa, kwa kuongoza kwa ufaulu katika mitihani ya kitaifa.

Shule hizo ni Magadini, Visitation, Magnificant, Faraja Seminari, Oshara, Sanya Juu na Nuru.

# Soko la kimataifa nafaka kutumia bil. 11/-

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MCHAKATO wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa kimkakati wa ujenzi wa soko la kimataifa la nafaka ambalo uwekezaji wake utagharimu Sh. bilioni 11 katika eneo la Kwa Sadala, Wilaya ya Hai, umepewa jina la 'The Magufuli International Complex Centre' (MICC-Hai).

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amesema mchakato huo umeiva na kwamba soko hilo litajengwa karibu na kiwanda cha Arsho au karibu na njia panda ya kwenda Masama.

Ole Sabaya alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki na watumishi wa halmashauri wa wilaya hiyo, madiwani, viongozi wa dini, taasisi za fedha na wadau wa maendeleo ambao wamekubali kutoa fedha hizo.

"Soko hili litakuwa na kazi ya kuongeza thamani ya mazao, kuchochea pato la mkulima na kuingizia serikali kodi, litakuwa na eneo maalum la viwanda vya usindikaji, eneo la utalii zikiwamo hoteli, kituo cha habari za utalii, migahawa ya kisasa na maeneo ya huduma za kibenki, bima, kumbi za kisasa za mikutano na maduka makubwa. Muda ambao mradi huu utatekelezwa ni miaka miwili na utagawanyika katika awamu tatu," alieleza.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, mradi huo unafadhiliwa na serikali ya Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Hai na wabia wa maendeleo yakiwamo mashirika binafsi na kampuni binafsi.

Karibu asilimia 70 ya wakulima wadogo katika wilaya hiyo, wanajishughulisha na kilimo cha ndizi na kilimo cha mbogamboga kwa mwaka mzima.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi huo wa kimkakati, utakaotumia miezi 12 kufanya vipimo, michoro, kuandaa eneo la kuweka vifaa vya ujenzi wa mradi na kufanya mapitio ya kiasi cha uhitaji wa mitambo.

Awamu ya pili, itahusisha usimikaji, kujenga uwezo kwa wasimamizi, wataalamu na majaribio ya mitambo. Awamu ya tatu, itahusisha manunuzi, usimikaji na uendeshaji wa mitambo kwa ujumla wake.

Ujenzi wa soko la kimataifa litakalokuwa na viwanda vya usindikaji wa nyanya, ndizi, kahawa, matunda na mboga, utatumia kiasi cha Sh. bilioni 8, wakati ujenzi wa kituo cha habari za utalii na maeneo ya huduma mbalimbali za kijamii, utagharimu Sh.bilioni 2 na manunuzi, usimikaji na majaribio ya mitambo na uendeshaji wa viwanda utaigharimu Sh. bilioni 1.



Diwani wa Kata ya Bomambuzi katika Manispaa ya Moshi, Juma Raibu, akikabidhi kadi ya pikipiki kwa mmoja ya vijana wa kata yake, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake aliyoitoa kipindi cha uchaguzi, zenye thamani ya Sh. milioni 23.2 zilizotolewa kwa vijana wa bodaboda na diwani huyo ili waweze kujikwamua kiuchumi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Tathmini ya ajali moto ya shuleni Ashira kuanza leo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), Seleman Jafo, akihisi ajali ya moto iliyoteketeza mabweni mawili ya ghorofa ya Shule kongwe ya Sekondari ya Wasichana ya Ashira, imesababishwa na hujuma, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetangaza kuanza kwa tathmini kuanzia leo.

Jana, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Avemaria Semakafu, alithibitisha kuwa serikali itapeleka katika shule hiyo kiasi cha Sh. milioni 750 kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo.

"Kutokana na janga la moto lililotokea siku tano zilizopita, wizara ina mpango wa kuongeza kiasi cha pesa kwa ajili ya ukarabati wa shule hii. Nimeelekeza mabweni yaliyoungua yapewe kipaumbele katika ukarabati huo.

"Mhandisi wa ujenzi wa wilaya, atashauriana na timu maalumu ya serikali kuu niliyoiunda, kuona kama majengo yaliyoungua kwa moto yanafaa kwa ukarabati na kuendelea kutumika au kuanza ujenzi upya. Ukarabati wa majengo na miundombinu ni lazima, haukwepeki."

Aidha, licha ya serikali kuanza kazi ya tathmini ya uharibifu na kuchunguza chanzo cha moto huo, Waziri Jafo alisema kuwa moto uliotketeza mabweni hayo mawili ya ghorofa ya shule hiyo kongwe umesababishwa na hujuma.

Kutokana na hujuma hizo, Jafo amevitaka vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi wa kina na kwa haraka na watakaobainika kuhusika na tukio hilo wachukuliwe hatua za kisheria.

Mei 23 mwaka huu, moto huo ambao chanzo chake hakijajulikana uliteketeza mabweni ya shule hiyo na vifaa vya wanafunzi 224 ambao kati yao wanafunzi 73 wamepoteza kila kitu. Moto huo unadaiwa ulitokea saa 2:00 asubuhi wakati wanafunzi wakiwa madarasani.

Kwa mujibu wa Waziri Jafo, wataalamu kutoka ofisi yake watafika katika shule hiyo kufanya tathmini na kutoa taarifa nini ambacho kinapaswa kufanywa katika mabweni hayo.

Sekondari ya Wasichana ya Ashira, imo katika kundi la shule kongwe za kitaifa za wasichana zilizowika miaka ya nyuma kwa kutoa wanafunzi wenye vipaji maalum, zikiwamo pia Sekondari ya Wasichana ya Weruweru, Kilakala, Msalato, Machame, Sekondari ya Wasichana Tabora na Nganza ya Mwanza.

# Nipashe Spotika



## NIYONZIMA AKIMBIZA WAGENI UBINGWA BARA UK.18




### ISIKUPITE

Kama beki wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk atafanikiwa kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] mwaka huu, atakuwa beki wa kwanza kuweza kutwaa tuzo hiyo binafsi ya juu duniani kwa upande wa wachezaji wa soka tangu Fabio Cannavaro alipoitwaa miaka 12 iliopita.




# FURUKUTA...

Kiungo wa Valencia, Francis Coquelin akila sahani moja na mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi (kulia), wakati wa mechi ya fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa Del Rey'] iliyopigwa juzi na Valencia kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**




Samuel Umtiti

# WA3 WAKUMRITHI KOMPANY MAN CITY

**MANCHESTER, England**

BAADA ya kutumia misimu 11 akiwa na Manchester City, nahodha na beki Vincent Kompany ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Baada ya kuifumua Watford kwenye fainali ya Kombe la FA, Manchester City haitakuwa naye tena, kwani tayari Kompany amecheza mchezo wake wa mwisho na klabu hiyo.

Kompany amekuwa na mchango mkubwa wa kuchomoza kwa Manchester City katika soka la dunia na raia huyo wa Ubelgiji ameshinda idadi kubwa ya mataji. Ushindi mara mbili mfululizo wa Kombe la Ligi Kuu yanaweza kuwa moja ya mafanikio makubwa zaidi kwake katika kipindi cha uchezaji soka pale City. Ingawa Kompany hakuwa na mafanikio kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini ukweli unabaki kuwa na mafanikio makubwa kwake pale Manchester City.

**Kompany amekuwa na nyakati bora za kukumbukwa akiwa na City. Kwenye Ligi Kuu bao la Kompany dhidi ya Newcastle United lilisaidia ushindi wa 1-0 na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutetea taji la ubingwa wa Ligi Kuu.**

Itakuwa kazi ngumu kwa Pep Guardiola kupata mrithi wa raia huyo Mbelgiji. Ingawa kuna vipaji vya kutosha kwenye kikosi hicho, na sasa Manchester City inaweza kutafuta mrithi wake kipindi hiki cha majira ya joto.

Kwa upande mwingine, hapa tunaangalia uwezekano wa wachezaji watatu ambao wanaweza kurithi mikoba ya Vincent Kompany pale Manchester City.

**3. Samuel Umtiti**

Samuel Umtiti amekabiliwa na majeraha kwa kipindi kirefu msimu huu, kitu kilichochangia kutokuwa na mechi nyingi za kucheza pale Barcelona. Baada ya kuwa na kiwango kizuri kwenye michuano ya Kombe la Dunia, Mfaransa huyo hajawa kwenye wakati mzuri na kuna uwezekano mkubwa sasa akalazimika kubadili klabu.

Huku Kompany akiwa anaondoka, Manchester City inahitaji beki mwenye nguvu na akili ya kucheza kama yeye, na Umtiti anaonekana kufiti kwenye nafasi hiyo. Kwa uwezo wake dimbani na kiwango cha mchezaji kama Kompany, anaweza kuwa mchezaji bora zaidi wa kurithi mikoba yake.

**2. Matthijs de Ligt**

Matthijs de Ligt, ni mchezaji mwenye kipaji cha ukweli pale Ajax na kila shabiki wa soka ameshuhudia jinsi alivyozawadiwa kipaji cha kucheza soka. Katika umri wake wa miaka 19, amekuwa nahodha wa kikosi hicho na kuifikisha timu yake kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na walikuwa wanajiandaa kutinga fainali kabla ya kutolewa na Tottenham Hotspurs.

Kijana huyo amekuwa ni beki mwenye akili na kiwango bora kabisa dimbani. Pia amekuwa na uwezo wa kufunga mabao na hivyo anafaa kumrithi Kompany pale Manchester City.

Katika mashindano yote kwa msimu wa 2018-19, De Ligt amefunga mabao saba kwenye mechi 55, kitu ambacho ni bora zaidi kwa beki. Beki huyo pia anashikilia rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwa nahodha kuiongoza timu kwenye hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, ukiacha kuwa mchezaji wa Uholanzi mwenye umri mdogo zaidi kufunga kwenye hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ingawa uhamisho wake unaweza kuwa ghali, Manchester City inatakiwa kujipanga ili kumsajili kuweza kuziba vizuri pengo la Kompany.

**1. Kalidou Koulibaly**

Beki huyu wa Napoli amekuwa katika kiwango bora kwa misimu kadhaa iliyopita na kuisaidia timu yake kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A. Ana ubora sawa na Kompany, na kama Pep Guardiola akikaa chini na kuamua kutafuta mrithi wa mchezaji wake wa kimataifa wa Ublegiji, kwa uhakika kabisa Koulibaly anafaa kuchukua nafasi hiyo.

Beki huyo kutoka Senegal amecheza zaidi ya mechi 150 katika klabu yake ya Napoli kwa kipindi cha misimu mitano iliyopita kwenye Serie A, ingawa amekuwa sio mfungaji mzuri, kwani amefunga mabao 10 tu kwenye ligi.

Amekuwa na mchango mkubwa kwenye kikosi chake na Manchester City wakimsajili mchezaji huyo anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwao kwa kipindi hiki cha majira ya joto na ataweza kuwasaidia vilivyo.

**JE, WAJUA?**



MABAO mawili ya kipindi cha pili kupitia kwa Odsonne Edouard, wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Hearts kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Scotland ['Scottish Cup'], yameifanya Celtic kutwaa mataji matatu msimu huu kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo. Kabla ya juzi, tayari Celtic ilishatwaa Kombe la Ligi na Ubingwa wa Ligi Kuu, na kwa mafanikio hayo, kocha wa muda, Neil Lennon akatangazwa kuwa wa kudumu.

# MICHEZO




Timu ya African Lyon ambayo imekuwa ya kwanza kushuka daraja msimu huu.

## NJE YA UWANJA

### Messi anavyomtesa Ronaldo Kiatu Ulaya

Lionel Messi ametwaa Kiatu cha Dhahabu Ulaya kwa mara ya sita shukrani kwa mabao yake 36 kwenye La Liga aliyowafungia mabingwa wa Hispania, Barcelona msimu huu.

Kutwaa kwa Messi kiatu hicho, kunamfanya sasa kuwa kinara wa ufungaji kwenye ligi tano bora barani Ulaya kwa mwaka wa tatu mfululizo, msimu huu akimpiku Kylian Mbappe kwa mabao matatu kufuatia Paris Saint-Germain kupokea kipigo cha 3-1 dhidi ya Reims Ijumaa iliyopita wakati straika huyo akitupia moja.

Messi pia kwa sasa ana Viatu vya Dhahabu viwili zaidi ya nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo, ambaye mara ya mwisho alitwaa tuzo hiyo msimu wa 2014-15.

Nyota huyo wa Kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 31, Messi ameiongoza Barca kutwaa taji la La Liga mara mbili mfululizo ['back-to-back'] mbele ya Atletico Madrid na Real Madrid msimu huu.

Hata hivyo, juzi Jumamosi Messi alishindwa kuipa Barcelona Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] kufuatia kukubali kipigo cha mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali dhidi ya Valencia.




# LIGI KUU KABLA YA MECHI ZA MWISHO KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

KILA timu kwa sasa imebakisha mechi moja tu kabla ya kufunga dimba la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2018/19, unaotarajiwa kumalizika kesho kwenye viwanja mbalimbali nchini.

Baada ya safari ndefu, hatimaye kila timu imevuna ilichokipanda. Ni msimu ambao ulizikutanisha timu 20 ambazo zilipambana kiume kutafuta ubingwa wa Tanzania Bara, lakini pia kuna timu hadi kwenye mechi za kesho, zinahangaika kubaki Ligi Kuu.

Mpaka sasa timu ya Simba ndiyo inayoonekana imemaliza kila kitu kwani imetwaa ubingwa, huku African Lyon nayo imeshajijua kuwa imeshuka daraja.

Baada ya mechi za kesho zitajulikana timu mbili ambazo zitashuka moja kwa moja na timu mbili ambazo zitakwenda kucheza mechi za mchujo maarufu kama 'play off' ambazo zitazikutanisha timu hizo pamoja na timu zilizoshika nafasi za pili kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara kwenye Kundi A na B. Ikumbukwe kuwa washindi wa kwanza wa makundi hayo, Namungo na Polisi Tanzania zimepanda moja kwa moja Ligi Kuu.

Timu mbili zitakazoshinda mechi hizo za 'play off', kutoka Ligi Kuu na Daraja la Kwanza nazo zitapanda moja kwa moja Ligi Kuu.

Kwa maana hiyo huenda timu moja au mbili zilizoshika nafasi ya 17 na 18 zikarejea tena Ligi Kuu, au pia ikawa kinyume chake, timu nyingine za Daraja la Kwanza zikachukua nafasi.

Mwandishi wa makala haya amekusanya rekodi na takwimu mbalimbali za timu za Ligi Kuu ikiwa imesalia raundi moja tu kufikia tamati...

**92-** Ni idadi ya pointi ambazo Simba imekusanya kabla ya mechi ya kesho dhidi ya Mtibwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

**86-** Hizi ni pointi zinazomilikiwa na Yanga mpaka sasa ambayo nayo imebakisha mechi moja dhidi ya Azam FC, ikiwa imeshika nafasi ya pili msimu huu, huku pointi hizo zikiilinda kwa kutofikiwa na timu yoyote ile zaidi ya Simba ambayo imezipita.

**77-** Timu ya Simba imefunga idadi hii ya mabao kwenye Ligi Kuu kabla ya mechi ya kesho, na mpaka sasa ndiyo timu iliyofunga mabao mengi zaidi kuliko timu nyingine yoyote ile. Pia kiuhalisia hakuna uwezekano wowote wa timu yoyote kesho kufikia idadi hiyo.

**72-** Hii ni idadi ya pointi za Azam FC ambazo inazo mpaka sasa. Imebakisha mechi moja tu dhidi ya Yanga hapo kesho, lakini pointi hizo imefanya kujihakikisha nafasi ya tatu ambazo hazitofikiwa na timu yoyote ile.

**44-** Kivumbi kiko hapa, kwani idadi hizi za pointi zinamilikiwa na timu nne kila mmoja. Timu hizo ni Biashara United, JKT Tanzania, Stand United na Mbao FC.

Timu hizi zote haziko salama, kwani Biashara iko kwenye nafasi ya 12, JKT Tanzania 13, Stand United 14 na Mbao FC ikiwa kwenye nafasi ya 15. Mechi za kesho ndizo zitaamua hatima yao.

**43-** Kagera Sugar na Prisons, kila moja ina idadi hii ya pointi, Prisons ikiwa kwenye nafasi ya 16 na Kagera Sugar 17. Kwa vyovyote lazima zishinde mechi za kesho, lakini hapo hapo zikiangalia matokeo ya mechi za mwenzao ili kuikwepa 'play off' au kushuka kabisa.

**41-** Mwadui FC, ndiyo timu iliyo kwenye hatari zaidi ya kushuka daraja kuliko timu nyingine yoyote ile zinazopigania kujinasua. Hizi ndizo idadi ya pointi ilizonazo, ikikamata nafasi ya 19. Ni ushindi tu ndiyo utaifanya ifikishe pointi 44 na kama ikiwa hivyo, basi itakuwa ikiombea timu za Kagera Sugar, Prisons zenye pointi 43 na Ruvu Shooting yenye pointi 42 zipoteze mechi zao, ili yenyewe itoke kwenye shimo hilo.

**38-** Ni idadi ya magoli yaliyofungwa na timu za KMC ya Kinondoni, Mbeya City na Stand United kila moja kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**29-** Simba imeshinda idadi hii ya mechi na kuwa timu iliyoshinda mechi nyingi zaidi kuliko timu yoyote ile kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**23-** Hizi ni idadi ya pointi ilizonazo African Lyon, timu ambayo imekuwa ya kwanza kushuka daraja msimu huu, ikikamata nafasi ya 20 kwenye msimamo wa Ligi Kuu. 22- African Lyon ndiyo timu iliyopoteza mechi nyingi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu. Namba hii inaonyesha idadi ya mechi ambazo tayari imepoteza.

**14-** JKT Tanzania na Coastal Union ndiyo timu zinazoongoza mpaka sasa kwa kutoa sare nyingi kwenye Ligi Kuu. Namba hii ndiyo idadi ya sare ambazo timu hizo imepata kila moja.

**10-** Timu za JKT Tanzania, Prisons, Ruvu Shooting na Kagera Sugar, kila moja imeshinda idadi hii ya mechi.

**5-** Inasimama kama ni idadi ya sare kwa timu ya Simba, idadi ya sare na mechi zilizopotezwa na Yanga, pia ni idadi ya mechi zilizopotezwa na Azam FC.

**3-** Simba imepoteza idadi hii ya mechi kati ya michezo 37 ambayo imecheza mpaka sasa.

**2-** Namba hii inasimama kwa Yanga, inayokamata nafasi hiyo kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**1-** Ni namba inayosimama kwa Simba inayoshika nafasi ya kwanza kwenye Ligi Kuu, lakini pia ndiyo bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

# NYOTA HAWA, KAMATA EURO MIL. 100 MKONONI




David De Gea

**LONDON, England**

HUKU msimu wa 2018-19 ukiwa umefikia ukingoni, kwa sasa macho ya wapenzi wengi wa mpira wa miguu yapo kwenye kuangalia majina ya wachezaji ambao watasajiliwa na klabu zao.

Klabu kwa sasa zinaingia sokoni kwa ajili ya kufanya usajili wa wachezaji wakubwa ili kuimarisha vikosi vyao tayari kwa msimu ujao.

Idadi kubwa ya wachezaji wenye majina makubwa wanatarajia kupamba kwenye usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto.

Makala haya yanakuchambuliaji wachezaji watano ambao wanaweza kusajili kwa zaidi ya euro milioni 100 kwa kipindi cha majira ya joto, twende sasa...

**5. Paulo Dybala (Juventus)**

Nyota wa Juventus, Paulo Dybala ni mmoja wa wachezaji wengi ambao wanavumishiwa kwa mengi kipindi hiki cha majira ya joto. Kaka wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, Gustavo Dybala amebainisha wazi kwamba, mdogo wake mwenye umri wa miaka 25, anafikiria kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ili kutafuta changamoto nyingine.

Uwapo wa Cristiano Ronaldo pia umekuwa moja ya sababu ya Dybala kuondoka kwenye klabu hiyo. Tangu kuwasili kwa mwamba huo wa Ureno, amekuwa na wakati mzuri na kufunga mabao mengi katika klabu hiyo.

**Mchezaji huyo wa Argentina alikuwa nyota kwa kibibi kizee hicho cha pale Turin msimu wa 2017/18, akifunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho tano. Hata hivyo, uwapo wa Ronaldo katika kikosi cha kwanza, kumemfanya Dybala kufunga mabao matano tu na pasi za mwisho nne katika mechi 28 alizowachezea 'Bianconeri' hao msimu huu.**

Kwa uhakika kabisa Dybala ambaye anavaa jezi namba 10 ataondoka kipindi cha majira ya joto. Klabu za Manchester United na Paris Saint Germain ndizo zinatajwa kuwania saini yake.

Dybala kwa sasa thamani yake inatajwa kuwa pauni milioni 90 (sawa na zaidi ya euro milioni 102).

**4. Antoine Griezmann (Atletico Madrid)**

Kwa zaidi ya mwaka mmoja uvumi kuhusu hatima yake pale Atletico Madrid ulikuwa ukisambaa. Antoine Griezmann hatimaye sasa amebainisha kwamba anajiandaa kuondoka Atletico Madrid. Mfaransa huyu ni mmoja wa wafungaji bora kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na klabu yake na ni vigumu kupata mrithi wake akiondoka hapo 'Rojiblancos'.

Kwa mujibu wa vyanzo kadhaa, Griezmann tayari amekubaliana na mabingwa wa Hispania, FC Barcelona, ambao kipindi cha majira ya joto kilichopita walijaribu kumsajili. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 28, anaonekana kuwa tayari kurithi mikoba ya mchezaji wa kimataifa wa Uruguay, Luis Suarez, ambaye anaonekana kuwa sasa anaelekea mwisho.

Habari njema kwa kocha Ernesto Valverde ni kwamba Paris Saint Germain na Manchester City zimejiondoa kwenye mbio za kumsajili mshambuliaji huyo na sasa ni wazi kwamba 'Blaugrana' watakuwa na uhakika wa kumsajili. Thamani ya Griezmann ni kati ya euro milioni 200 hadi 120 na Julai Mosi, mwaka huu miamba hao wa Catalunya watakamilisha usajili wake.

**3. Paul Pogba (Manchester United)**

Ole Gunnar Solskjaer anatajwa kuwa yupo bize kwenye kuhakikisha anakijenga upya kikosi chake cha Manchester United kipindi hiki cha majira ya joto. Kwa uhakika Paul Pogba ni mmoja wa wachezaji ambao anataka kuwakumbatia wabaki hapo katika dimba la Old Trafford.

Majaliwa ya Mfaransa huyo yapo shakani kwani anaonekana kuwa anaweza kuondoka, huku United ikiwa haipo tayari kumuachia aondoke.

Pogba amekuwa kwenye wakati mgumu tangu alipowasili hapo akitokea Juventus mwaka 2016. Kwa kukoleza moto, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alitamka wazi kwamba anataka kuondoka hapo Old Trafford.

Zinedine Zidane kocha wa Real Madrid mara kadhaa ametamka kuwa mshindi huyo wa Kombe la Dunia anataka kuona akicheza kwenye dimba la Santiago Barnabeu msimu ujao. Barcelona pia inatajwa kuwa kwenye mipango ya kumtaka kiungo huyo.

Kwa mujibu wa ripoti, 'Mashetani Wekundu' hawatakuwa tayati kumuachia nyota wao huyo bila euro milioni 130.

**2. David De Gea (Manchester United)**

Manchester United inapanga kufanya marekebisho makubwa ya kikosi chake kipindi hiki cha majira ya joto na huku wachezaji wengi wakionekana kutaka kuondoka hapo kwenye dimba la Old Trafford. Bahati mbaya, golikipa wao, David De Gea pia yupo kwenye harakati za kutaka kuondoka.

Raia huyo wa Hispania alitua hapo kwa 'Mashetani Wekundu' mwaka 2011. Amekuwa kwenye wakati mzuri na klabu hiyo. Hata hivyo, sasa ameonyesha wazi kuwa anataka kuondoka.

De Gea bado hajakubali kusaini mkataba mpya hapo Old Trafford, huku mkataba wake wa sasa ukifikia mwisho. Ripoti zinasema kwamba, raia huyo wa Hispania anataka kuondoka hapo United kwa ajili ya kutafuta klabu itakayomwezesha kushinda mataji. Na sasa Mashetani Wekundu wameripotiwa kutaka kumsajili Jasper Cillesen kama mrithi wake.

Manchester United watapigana kuhakikisha wanambakisha kipa huyo, lakini kama wakishindwa itawalazimu kumuuza na thamani yake inatajwa kuwa ni zaidi ya euro milioni 120.

**1. Eden Hazard (Chelsea)**

Sawa, hatuhitaji kujua ni klabu gani Eden Hazard atajiunga nayo? Ni rahisi kuijua.

Pengine mchezaji huyu wa kimataifa wa Ubelgiji atacheza mchezo wake wa mwisho kwa Chelsea dhidi ya Arsenal kwenye fainali ya Kombe la Europa Jumatano, na inaonekana kuwa ndio atafunga rasmi ukurasa wake wa kukaa kwenye Ligi Kuu ya Soka ya England.

Kwa mujibu wa ripoti, Hazard tayari ameshafikia uamuzi wake wa mwisho kuhusu kuondoka hapo Chelsea na sasa imebakia tu kwa Blues hao kama wataweza kumbakisha. Baadhi ya ripoti zinabainisha kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, atatangazwa kuwa ni mchezaji wa Real Madrid Mei 29, mwaka huu na kumaliza kipindi chake pale England. Zinedine Zidane pia anatajwa kuwa amekuwa akivutiwa mno na kiwango cha mchezaji huyo wa Ubelgiji.

'Los Blancos' wameripotiwa kwamba wamekubaliana na Chelsea kulipa kiasi cha euro milioni 100 kama ada kwa ajili ya kumsajili Hazard. Inabakia kuwa suala la muda tu kwa mchezaji huyo kuondoka hapo Chelsea kwa sasa.

## Nukuu

"Nimecheza soka bora katika wasifu wangu kisoka msimu huu na kwa Arsenal, na si kwa sababu ya kufunga mabao, lakini katika mchezo wangu - ukweli nimejizatiti. Tuzo binafsi ukweli si muhimu kabisa. Mara zote ni furaha, bila shaka, kupokea vitu kama hivi, lakini si kitu cha kwanza ninachowaza wakati ninacheza soka. Ninataka kushinda kombe, kama Europa League," **Straika wa Arsenal, Alexandre Lacazette.**



"Nimegundua mengi hapa, na ninahisi labda ni wakati wa kuwa na majukumu zaidi. Ninatumai kwamba pengine inaweza kuwa hapa Paris Saint-Germain, hiyo itakuwa furaha kubwa ama pengine sehemu nyingine na mradi mpya," **alisema Kylian Mbappe ambaye anawindwa na Real Madrid, baada ya kutwaa tuzo mbili ya Mchezaji Bora wa Mwaka Ligue 1 na ile ya Kinda Bora wa Mwaka.**



"Uchaguzi mara nyingine ni mgumu. Siwezi kusema kila wakati, hata kama ungependa. Wachezaji wengine wanastahili pia na Aymeric [Laporte] wa Manchester City ni kati yao. Kama nisingemchagua Clement [Lenglet] wa Barcelona, angestahili hilo pia. Ni fursa kwangu nina wachezaji wengi kwa kila nafasi ambao ni wagombea wa timu ya Ufaransa," **Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps akijitetea kumuita Lenglet na kumwacha Laporte katika kikosi chake.**





# NIYONZIMA AKIMBIZA WAGENI UBINGWA BARA

**Na Adam Fungamwango**

KAMA kuna wachezaji wenye bahati duniani, basi kiungo wa Kinyarwanda, Haruna Niyonzima (pichani) atakuwa mmojawapo.

Jumanne iliyopita wakati Simba ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya pili mfululizo, yeye alikuwa akisherehekea kubeba taji hilo kwa mara ya tano mfululizo.

Niyonzima tangu alipojiunga na Simba msimu uliopita ni kama vile yeye ndiyo amekuja na taji hilo kwani ni mara ya pili sasa anatwaa akiwa na Wekundu wa Msimbazi hao.

Kabla ya hapo, Niyonzima alikuwa Klabu ya Yanga alikotoka huko akiwa ametwaa taji hilo mara tatu mfululizo.

Kwa maana hiyo, Niyonzima ametimiza mataji matano mfululizo, matatu akiwa na Yanga, na mawili akiwa na Simba. Huyu unaweza kusema kuwa ni mchezaji wa mataji.

**"Naweza kusema kuwa mimi ni mtu mwenye bahati, tena ya kipekee kabisa. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo. Kwa sababu hili kwangu ni jambo kubwa sana. Tangu nije Tanzania hakuna mchezaji yeyote wa kigeni aliyeweza kupata bahati kama hii na kuweka rekodi hii niliyoiweka mimi," anasema Niyonzima na kuongeza:**

"Pia nawashukuru wachezaji wenzangu kwa ushirikiano waliouonyesha kwangu kwa kuwa sikuuanza msimu vizuri kwa sababu mbalimbali ikiwamo majeraha na nyingine ambazo sitazisema hapa, lakini kwa sasa mambo yamekwenda vizuri."

Niyonzima alitua Tanzania kwa mara ya kwanza mwaka 2011 na kusajiliwa na Klabu ya Yanga na amekuwa hapa nchini kwa kipindi chote hicho.

Ifuatayo ni misimu ambayo Niyonzima aliweka rekodi ambayo baadhi ya wachezaji hata wa Bongo wameshindwa kuipata na kuonekana kama vile wanapishana na ubingwa, teleza nayo hapa...

**1. Msimu wa 2014/15- Yanga**

Niyonzima alikuwa mmoja wa wachezaji waliokuwa kwenye kikosi cha Yanga kilichotwaa ubingwa msimu wa 2014/15.

Ni msimu ambao Yanga ilimaliza ligi ikiwa na pointi 55 kwa mechi 26 ilizocheza, ikishinda mechi 17, sare nne na kupoteza mechi tano. Timu hiyo ilifunga mabao 52 na kufungwa mabao 18, akifunga bao moja tu msimu mzima.

**2. Msimu wa 2015/16- Yanga**

Niyonzima akiwa na Yanga alitwaa tena taji la ubingwa wa Ligi Kuu, akiwa na kikosi ambacho kilicheza mechi 30 msimu huo na kushinda 12, sare saba na kufungwa mechi moja tu.

Ni msimu ambao Yanga ilifunga mabao 70 na kufungwa 19 tu, huku ikikusanya pointi 73. Na msimu huu pia alifunga bao tu.

**3. Msimu wa 2016/17- Yanga**

Alikuwa kwa mara nyingine tena kwenye kikosi cha Yanga kilichotwaa ubingwa msimu wa 2016/17 na ilikuwa ni mara ya tatu mfululizo.

Ilicheza mechi 20, ikishinda mechezo 21, sare tano, na kupoteza mechi tano, ikimaliza mechi zake 30 ikiwa na pointi 68. Hakufunga bao lolote msimu huo.

**4. Msimu wa 2017/18- Simba**

Ulikuwa ni msimu wa kwanza kwa Niyonzima akiwa na klabu yake mpya ya Simba. Huu ni msimu wa 2017/18. Yaani msimu uliopita.

Ni msimu ambao Niyonzima pia alifunga bao moja, Simba ikicheza mechi 30, ikishinda mechi 20, sare tisa na kufungwa mechi moja. Ilimaliza ikiwa na pointi 69 na kutwaa ubingwa wa kwanza baada ya misimu mitano, lakini kwa Niyonzima ukiwa ni wa nne mfululizo kwake. Ni kama alihama nao kutoka Yanga. Pia katika msimu huo alifunga bao moja.

**5. Msimu wa 2018/19- Simba**

Niyonzima ametwaa tena ubingwa msimu huu akiwa na kikosi cha Simba na kuwa sasa ni mara ya tano mfululizo. Simba ilitwaa ubingwa ilipofikisha jumla ya pointi 91 ambazo hazitafikiwa na timu yoyote ile kwenye Ligi Kuu, lakini pia kiungo huyo akiwa amefunga bao moja mpaka sasa.

**Maisha ya soka**


Kiungo huyo mwenye uwezo mkubwa wa kumiliki mpira, chenga za maudhi na pasi za mwisho zenye 'macho', aliyezaliwa Gisenyi, Kusini mwa Ziwa Kivu nchini Rwanda mwaka 1990, anasema alianza kuupenda mchezo wa soka baada ya kuona kaka zake wakicheza, lakini shemeji yake mmoja aliyemtaja kwa jina la Athumani ndiye aliyempa moyo zaidi wa kufanya vizuri.

"Kaka zangu walikuwa wachezaji wazuri, lakini pia makosa ya eneo hilo la nyumbani walinishawishi nizidi kuendelea na soka, na shemeji yangu Athumani ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kuninunulia viatu vya kuchezea," anasema.

Safari yake ya soka ilianza mwaka 2005 alipoanza kuchezea Klabu ya Etincelles, kabla ya kutua Rayon Sport mwaka 2006 na 2007 akajiunga na Klabu ya APR zote za nchini Rwanda.

Safari yake ya soka la kulipwa nje ya nchi ilikuwa ni mwaka 2011 alipoondoka nchini kwao na kujiunga na Yanga ya Tanzania na hajahama nchini hapa kisoka hadi leo hii akiwa na Klabu ya Simba.

**NAJUA WAJUA**



PAMOJA na Haruna Niyonzima kuweka historia ya kuwa mchezaji wa kwanza wa kigeni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara mara nyingi kufuatia kulibeba taji hilo mara tano, katika kila msimu alioutwaa hadi sasa amekuwa akifunga bao moja kila msimu.

## SOKA



# VITU VI5 VYA KUJIFUNZA MAN CITY MSIMU HUU

**LONDON, England**

MANCHESTER City imekuwa ikicheza kwa tofauti kabisa ikilinganishwa na klabu nyingine za Ligi Kuu England kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita. Licha ya kupata changamoto kubwa kutoka kwa Liverpool, Pep Guardiola na timu yake waliweza kutetea ubingwa huo kwa tofauti ya pointi moja na kufanya kuwa moja ya mbio bora zaidi za Ligi Kuu kuwahi kutokea.

Ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Watford kwenye fainali ya FA, kuliifanya City kumaliza msimu kwa kutwaa mataji matatu msimu huu. Ingawa umekuwa wakati bora zaidi wa mafanikio kwa timu.

Kiukweli Man United imeshindwa kutamba Ulaya baada ya kutolewa na Tottenham Hotspur kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na hivyo kumaliza ndoto za City katika mashindano hayo.

Hata hivyo, kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hakuwafanyi wao kutokuwa bora. Lakini huu ulikuwa msimu bora zaidi kwa Man City na hapa tunaangalia vitu vitano vya kujifunza kutoka kwa Manchester City.

**5. Kiwango cha dhahabu**

EPL chini ya Guardiola

Tangu kuchukua mikoba ya kuinoa Manchester City, hamasa ya Pep Guardiola na mbinu zake zimekuwa ni za kuvutia zaidi. Chini ya zama za Guardiola falsafa ya soka yao imebadilika kabisa. Muhimu zaidi, wachezaji wamepewa mbinu mpya na pia kuwa na kiwango tofauti kabisa.

Chini ya kocha huyo raia huyo wa Hispania, City imetwaa mara mbili mfululizo taji la Ligi Kuu ya England. Huku wakikaribia kufikia mabao 200 katika misimu miwili na safu ya ushambuliaji ya City imekuwa bora zaidi.

Kitu kimoja muhimu kwenye safu ya ushambuliaji ya City ni kwamba hawakubadilisha staili yao mara kwa mara. Na ubora wao huo ukaifanya City kuwa kwenye kiwango bora cha daraja la dhahabu.

**4. Ederson Moraes amethibitisha thamani yake**

Misimu miwili iliyopita, Ederson Moraes alipamba vichwa vya habari wakati alipokamilisha usajili wa fedha nyingi kutua hapo kwenye dimba la Etihad. Golikipa huyu na mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, ameonyesha thamani yake kuwa ni moja ya usajili bora zaidi katika zama za City. Tangu hapo amekuwa kwenye kazi ya kuzuia mabao kwenye lango la Man City.

Huku City ikiwa inapenda kucheza kwa kushambulia kutoka nyuma, Ederson ameonekana kuelewa vizuri zaidi mfumo huo na kuhakikisha kwamba anazuia nyavu zake kutikiswa.

Ubora aliouonyesha Ederson umemfanya kuwa mmoja wa magolikipa bora kwenye ligi hiyo. Mbrazil huyo amethibitisha kwamba City walikuwa sawa kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kumsajili yeye.

**3. Uwezo wa Aymeric Laporte**

Ingawa Klabu za Ligi Kuu ya England mara nyingi huwa hazitumii kiasi kikubwa cha fedha wakati wa usajili wa kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari, Manchester City ilivunja mwiko huo kwa ajili ya kumsajili Aymeric Laporte Januari mwaka 2018. Hata hivyo, mwaka mmoja baadaye, kila mmoja ameona kwa nini Guardiola aliamua kumsajili beki huyo wa kati wa Ufaransa.

Nguvu yote ya ushambuliaji ya Man City msimu huu, ilikuwa imechangia kwa kiasi kikubwa na Laporte. Uwezo wa Laporte kuusoma mchezo kwa kuijenga vizuri safu ya ulinzi lilikuwa jambo lililoimarisha zaidi timu hiyo. Kwa nyongeza mchezaji huyo wa zamani wa Athletic Bilbao pia amethibitisha uwezo wake wa kuchangia kwenye ufungaji, kwani alitoa pasi za mwisho tatu kwa kipindi chote cha msimu huu wa 2018-19.

**2. Bernardo Silva njiani kuwa mchezaji bora duniani**

Msimu wa 2018-19, umemalizika kwa kuwa bora zaidi kwa Bernardo Silva akiwa katika rangi za jezi ya Manchester City. Huku Kevin De Bruyne akikosa sehemu kubwa ya msimu kutokana kwa majeruhi, raia huyu wa Ureno aliweza kuimiliki vizuri safu ya kiungo ya City na kufanya wengi wamsahau Bruyne raia wa Ubelgiji.

Silva ameonekana kuwa mrithi sahihi wa David Silva. Silva alikuwa na kipindi bora hapo City, lakini sasa muda wake unaoonekana kuelekea ukingoni na yeye ndiye anayeonekana haswa kuwa mrithi wake.

Akiwa na mabao 13 na pasi za mwisho 13 kwenye mashindano yote msimu huu, Silva amejipambanua yeye mwenyewe kama ana miaka mingi zaidi ya kuendelea kuwa bora zaidi.

**1. Man City itaendelea kunyatia ubingwa wa Uefa msimu ujao**

Kwa ligi zote za nyumbani Manchester City imetawala tangu ujio wa Guardiola, lakini jambo moja ni kwamba wameshindwa kutamba Ulaya. Msimu huu walijipanga kufika mbali, lakini wakaishia mikononi mwaka Tottenham Hotspur kwenye hatua ya robo fainali.

Hata hivyo, staili ya uchezaji ya City chini ya Guardiola, inaonekana ni wazi kwamba msimu ujao wanaweza kulibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kama wataendelea na falsafa ile ile ya uchezaji.

Ingawa kwa sasa wanakabiliwa na uwezekano wa kufungiwa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kutokana na kuvunja sheria ya haki ya usajili, wanaweza kuwa moja ya washindani wa taji hilo msimu ujao.

%%%%%%

NDANI YA 18




LICHA ya kuhitimisha msimu wa Ligue 1 kwa kichapo cha mabao 3-1 dhidi ya Reims wiki iliyopita, bao lao pekee kupitia kwa Kylian Mbappe katika dakika ya 59, linawafanya mabingwa Paris Saint-Germain kuwa timu ya kwanza Ligi Kuu Ufaransa kuweza kucheka na nyavu katika mechi zote 38.

Nipashe
Spotika



HUKU msimu wa 2018-19 ukiwa umefikia ukingoni, kwa sasa macho ya wapenzi wengi wa mpira wa miguu yapo kwenye kuangalia majina ya wachezaji ambao watasajiliwa na klabu zao. Klabu kwa sasa zinaingia sokoni kwa...

**Uk. 16-17**



Van Dijk

# KWA NINI NI MWAKA WA VAN DIJK BALLON D'OR

**LONDON, England**

HUKU mismu wa 2018/19 ukifikia mwisho, mazungumzo yote kwa sasa ni nani atakuwa mchezaji bora msimu huu. Inaonekana wachezaji kwa sasa wanafikiri kutwaa Ballon d'Or na wote wamekuwa kwenye kiwango bora kabisa na timu zao. Messi amekuwa katika moja ya msimu wake bora kabisa, huku Virgil van Dijk akiifanya safu yake ya ulinzi kuwa kwenye kiwango cha kuvutia pale Liverpool.

Messi amekuwa hazuiliki mbele ya goli, lakini Van Dijk amekuwa mzuri zaidi kwenye kulinda lango. Hakuna mchezaji yeyote aliyempiga chenga kirahisi msimu huu!

Ingawa kutakuwa na mshangao mkubwa kama Messi atashinda tuzo yake ya sita ya Ballon d'Or msimu huu, lakini kiwango cha Van Dijk sio cha kukipuuzia. Hapa tunaangalia sababu tatu kwa nini Van Dijk atakuwa na nafasi kubwa ya kushinda tuzo hiyo msimu huu na kuwa beki wa kwanza tangu Fabio Cannavaro alipoitwaa miaka 12 iliyopita:

**1. Amekuwa kwenye kiwango kisichoshuka kwa klabu na nchi**

Katika mechi zake 59 ambazo Van Dijk ameichezea klabu yake na nchi msimu huu, ni vigumu kushuhudia kwamba amekuwa kwenye kiwango kibovu. Kiwango chake kwa kutoshuka msimu huu kimemfanya kuwa mmoja wa mabeki bora zaidi wa kati.

Amecheza mechi zote za Ligi Kuu kwa Liverpool na kiwango chake kimemfanya kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu ya England. Katika mechi zote, Van Dijk amekuwa beki bora, akizuia mipira kwa kichwa pia. Hakuna hata mchezaji mmoja aliyeweza kumpiga chenga kirahisi Mholanzi huyo msimu huu!

Amekuwa pia asiyeshuka kiwango katika mechi zake za kimataifa kwa nchi yake. Baada ya Uholanzi kushindwa kufuzu kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, Van Dijk amekuwa sehemu ya mafanikio kwa kikosi hicho cha Uholanzi. Sasa wapo kwenye nafasi nzuri ya kufuzu Euro 2020 na pia wako kwenye nusu fainali ya Kombe la Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Yeye na De Ligt wametengeneza safu imara zaidi ya ulinzi kwa nchi yao. Kama Van Dijk ataweza kushinda Kombe la Ligi ya Mataifa ya Uefa na Messi akashindwa kuibeba Argentina kwenye Copa America, hivyo Van Dijk anaweza kuwa na nafasi nzuri ya kushinda tuzo hii.

**2. Beki bora wa kati**

Siyo tu Van Dijk anajulikana kwa uwezo wake wa kuwazuia washambuliaji wakali, lakini pia anajulikana kwa uwezo wake wa kucheza pasi nzuri. Ana uwezo mzuri kwenye kucheza soka kwa ulinzi wa kisasa.

Anaweza kutengeneza pasi na kupandisha mashambulizi kwa timu yake. Alitoa pasi ya mwisho kwenye mchezo wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Bayern Munich msimu uliopita. Amekuwa ni beki sio wa kuzuia mashambulizi bali pia kutengeneza mashambulizi.

Amekuwa akitengeneza safu imara ya ulinzi kwa Liverpool msimu huu. Kama ukiilinganisha safu ya ulinzi ya Liverpool na timu nyingine, basi tangu kuwasili kwa Van Dijk kuimeifanya kuwa katika wakati mzuri zaidi msimu huu. Ameitengeneza safu imara zaidi ya ulinzi kwa upande wa Liverpool. Na pia ameisaidia timu yake ya Liverpool kucheza mechi 21 bila kuruhusu bao kwenye Ligi Kuu.

Pia ameweza kuiimarisha safu ya ulinzi ya Liverpool kwa 'upatina' wake mzuri na mabeki Lovren na Matip. Uchezaji wao wa pamoja umeifanya klabu hiyo kuwa kwenye kiwango bora zaidi barani Ulaya.

**3. Ameisaidia Liverpool kutinga fainali Uefa kwa mara ya pili**

Tangu kuwasili kwa Van Dijk, Liverpool imeweza kufuzu kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa mara mbili na kumaliza nafasi ya pili kwenye mbio za Ligi Kuu ya England ikipitwa kwa pointi moja tu dhidi ya mabingwa Manchester City. Pengine wanaweza kuwa wafalme wa Ulaya kama wakiifunga Spurs kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pale jijini Madrid Juni Mosi, mwaka huu.

Van Dijk amecheza kama nguzo kuu ya mafanikio ya kikosi cha Kocha Jurgen Klopp. Alisimama kama nguzo muhimu kwa kikosi hicho msimu huu. Kwa uwapo wake, wameonyesha kuwa na safu imara zaidi ya ulinzi pamoja na uwapo wa Robertson, Alexander Arnold na Allison pale golini.

Kama Liverpool itafanikiwa kuifunga Spurs kwenye fainali, watashinda taji lao la sita la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kwa uhakika kabisa Van Dijk atakuwa na nafasi kubwa ya kushinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa dunia.

## USILOLIJUA

MABAO mawili ya Robert Lewandowski na moja la Kingsley Coman katika ushindi wa 3-0 kwenye mechi ya fainali ya Kombe la DFB-Pokal dhidi ya RB Leipzig juzi, yamemfanya Kocha wa Bayern Munich, Niko Kovac kuwa kocha wa kwanza kutwaa taji hili mara mbili mfululizo ['back-to-back'], baada ya mwaka jana kulibeba kwa kuichapa Eintracht Frankfurt mabao 3-1 kwenye mechi ya fainali.



# Ma-DC Nyanda za Juu kujadili utunzaji misitu

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKUU wa wilaya kutoka mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na watumishi kutoka Wizara za Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) wamekutana jijini Mbeya kujadili na kuweka utaratibu utakaosaidia utunzaji wa rasilimali za misitu.

Majadiliano hayo yalifanyika juzi jijini Mbeya ikiwa ni utekelezaji wa randama ya makubaliano ya usimamizi wa rasilimali za misitu, pamoja na utawala bora yaliyofanyika mwezi Mei, 2016.

Majadiliano hayo yalikuwa na lengo la kuweka ushirikiano mzuri kwenye rasiliamli za misitu nchini ili kuondoa changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya misitu ikiwamo ukataji holela wa miti na uchomaji.

Mgeni rasmi katika majadiliano hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kila mmoja akitimiza wajibu wake changamoto ya uharibifu wa mazingira itakwisha na rasilimali za misitu zitatunzwa.

Alisema baadhi ya wananchi wanavamia misitu kwa sababu ya usimamizi mdogo wa utunzaji misitu, aliwataka watumishi na wadau wote wa misitu kusimamia vyema sheria zinazokataza uharibifu wa misitu.

"Nawaomba watumishi na wakuu wa wilaya na wadau wengine wa misitu kuendelea kutoa elimu ya utunzaji misitu hasa kwa jamii za wafugaji na wakulima ambao mara nyingine wamekuwa wakivamia misitu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye," alisema Chalamila.

Meneja wa Wakala wa Misitu Tanzania, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Ebrantino Mgiye, alisema Tanzania ina jumla ya hekta milioni 48 za misitu.

Alisema ili kutunza hekta hizo milioni 48 serikali iliamua kuwashirikisha viongozi na idara nyingine ili kuongeza nguvu ya pamoja katika utunzaji misitu nchini.

Alisema idadi hiyo ya hekta za misitu ni kubwa, lakini ushirikiano unahitaji ili kila mmoja kwa nafasi yake ahakikishe hakuna uvamizi wa misitu wala uchomaji.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akiwa kwenye harambee ya uchangiaji wa ujenzi wa jengo la ofisi ya chama hicho, Wilaya ya Tanga iliyoendeshwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa, Humphrey Polepole, Sh. milioni 18.5 zilikusanywa. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Chalamila awaonya wanunuzi tumbaku holela

**Na Grace Mwakalinga,**
CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameagiza watumishi wa umma ambao wananunua tumbaku kwa njia za panya na wakulima wanaouza wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ili kudhibiti hujuma dhidi ya taasisi za kifedha, vyama vya msingi pamoja na kampuni zinazonunua zao hilo kisheria katika Wilaya ya Chunya.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua soko la pamoja la zao la tumbaku lilipo katika Kijiji cha Mtande, Kata ya Mamba, wilayani Chunya na kuagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, kuchukua hatua za kisheria kwa watumishi na wakulima wanaolalamikiwa kuzihujumu taasisi za kifedha kutolipa madeni.

Alisema wakulima hao hulazimika kuuza tumbaku zao kwa njia ya panya ili kukwepa kulipa madeni kwenye taasisi za kifedha na matokeo yake kuziingizia hasara kutokana na kushindwa kujiendeleza na kukopesha watu wengine na mwanya huo hutumia watumishi wa umma kununua tumbaku hizo kwa bei wanazotaka wao.

"Mtumishi yeyote atakayebainika ananunua tumbaku kwa njia ya panya nasema akamatwe na vyombo vya sheria kama wanaona biashara ya tumbaku ni nzuri basi waingie kwenye soko la ushindani kupitia vyama vya ushirika, nahitaji wakulima wanufaike, pia taasisi za kifedha ambazo zinawakopesha wakulima nazo zipate faida kwa kurejeshewa madeni yake," alisema Chalamila.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa tumbaku wanaendelea na jitihada za kutafuta soko la uhakika la tumbaku ili kuwanufaisha wakulima kwa kuuza kwa bei nzuri ikilinganishwa na ilivyo sasa.

Alisema katika mazao mengine ikiwamo kakao, wakulima wamenufaika kwa kuwa kilo moja inauzwa kuanzia Sh. 5,000 jambo ambalo limekuwa na tija kwa mkulima kuendesha maisha yake.

Aliwashauri wakulima wa tumbaku wilayani Chunya kuzingatia kanuni bora za kilimo kuanzia kupanda mpaka kuvuna, ili mazao yao yaendane na soko la ushindani.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, aliwataka wakulima wa tumbuka kuendelea kuuza zao hilo kwa pamoja kupitia vyama vya ushirika.

Risala ya Chama cha Wakulima wa Tumbaku (Chutcu), ambayo ilisomwa na Daniel Mpigasupi, kimelalamikia ucheleweshwaji wa pembejeo za kilimo usioenda sambamba na msimu wa zao.

Alisema kucheleweshwa kwa pembejeo za kilimo kunakwamisha wakulima wa tumbaku kulima kwa wakati na matokeo yake hulima msimu ambao hauna mavuno mazuri.

Mrajisi wa vyama vya ushirika Mkoa wa Mbeya, Angela Maganga, alisema serikali inaendelea na jitihada za kuwaunganisha wakulima kupitia vyama vya ushirika ili kupanga bei na kuuza mazao yao kwa pamoja.

Alisema Mkoa wa Mbeya una vyama vya ushirika zaidi ya 17 na lengo ni kuhakikisha wakulima wote wanaunganishwa na vyama hivyo ili waendelee kunufaika na mazao yao, aliwataka viongozi wa vyama vya ushirika kuwa waadilifu.

# 'Mifumo ya tozo za kodi imepitwa na wakati'

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema ipo haja kwa serikali kufanya Marekebisho ya Sheria za tozo za kodi kwa wafanyabiashara na wakulima ili kuongeza tija na faida katika shughuli zao.

Chalamila alitoa rai hiyo jana Jijini Mbeya, wakati wa mkutano wa majadiliano ya namna ya kuboresha biashara kupitia mijadala ya pamoja baina ya sekta binafsi na watendaji wa serikali wakiwamo wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, wenyeviti wa halmashauri, maofisa biashara kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, chini ya Mpango wa Kuendeleza Mifumo ya Kimasoko ya Kilimo nchini (AMDT).

Alisema mazingira ya kibiashara nchini yanakwenda sambamba na mifumo ya maboresho ya kodi na kwamba ya sasa bado ni ile ya miaka 1990 na imepitwa na wakati.

"Mifumo ya maboresho ya kodi haikwepeki, tusikwepe kuzungumzia maboresho ya mifumo ya kodi ili kuleta tija nina amini tukifanya maboresho ya mifumo ya sheria za kodi zetu kutoka mifumo ya zamani na kuanzisha mipya itaondoa manung'uniko," alisema Chalamila.

Alisema kuwa bado kuna kasumba ya watu kuzungumza zaidi kuliko vitendo kwenye masuala ya msingi jambo ambalo linakwamisha juhudi za wananchi kama vile wakulima kuhamasisha kulima kwa wingi, lakini wanakosa masoko na mazao yao kuharibika.

Chalamila alisema viongozi wanaohamasisha wakulima kulima kwa wingi lazima wawaandalie na masoko ya uhakika ili wayauze mazao.


Mtaalamu wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara wa chini ya Mpango wa Kuendeleza Mifumo ya kimasoko ya Kilimo nchini (AMDT), Tertula Swai, alisema lengo ni kuongeza kipato na fursa za ajira kwa Watanzania wa rika zote hususani walioko maeneo ya vijijini.

Alisema kupitia programu hiyo wanakwenda kutengeneza mifumo ya masoko, uzalishaji mbegu na uuzaji pembejeo pamoja na mfumo wa utoaji huduma.

"Mpango huo una vipengele viwili ambavyo ni kuboresha mnyororo wa thamani kwa mazao ya mahindi, mikunde na alizeti na kuboresha mazingira ya biashara," alisema Swai.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Steven Mhapa, alisema mabaraza ya biashara yanawasaidia zaidi madiwani kuwajengea uelewa na kusababisha elimu kwa wakulima maeneo ya vijijini.

Alisema mijadala inayoandaliwa na AMDT iwafikie na wakulima huko vijijini ambao wanahangaika na masuala ya masoko licha ya kuwa wanazalisha kwa wingi.





## Watakiwa kutumia umeme kujikwamua kiuchumi

**Na Renatha Msungu,** MPWAPWA

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amewataka wananchi waishio vijijini ambao wameshafikiwa na huduma ya umeme, kutumia kuendeleza biashara zao ili waweze kujiinua kiuchumi.

Mgalu alitoa kauli hiyo juzi, wakati akiwasha umeme katika Kijiji cha Chibwegere kilichopo wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma.

Subira alisema kwa sasa hakuna sababu ya wao kushindwa kufanya biashara zao kutokana na kijiji hicho kuunganishwa umeme.

"Naomba wananchi muendelee kuunganisha umeme lengo kila nyumba iwe na umeme," alisema Mgalu.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni kila mmoja kutafuta hela ya kuunganisha umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na biashara zao.

Aliagiza Shirika la Umeme nchini (Tanesco), wilayani humo kuhakikisha wanagawa kifaa cha Umeme Tayari (UMETA) kwa wananchi wa eneo hilo ili iwe rahisi kuunganisha katika nyumba zao.

Alisema UMETA inasaidia hususan kwa wale wenye ujenzi wa nyumba ndogo ambazo ni rahisi kwao kuwashiwa.

Alisema kama serikali wanahitaji hadi kufikia Desemba mwaka huu vijiji vyote viwe na umeme.

"Tunahitaji kuona vijiji vyetu vinakuwa na umeme, lengo ni nchi nzima," alisema Mgalu.

Naye Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, George Simbachawene, aliishukuru serikali kwa kuweka umeme takribani vijiji vyote vya jimbo lake.

Alisema awali wananchi wa Chibwegere walikuwa wakipiga kelele kutaka umeme, lakini kwa sasa ana imani biashara ya samaki na vinywaji zitakuwa bora kuliko ilivyokuwa awali.

# Neema kwa wasichana shuleni, mtaani

**Na Paul Mabeja,** BAHI

ILI kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24, serikali imezindua mradi wa kuwawezesha wasichana wenye rika hilo waliopo shuleni na mitaani.

Mradi huo wa miaka mitatu wa timiza malengo, unalenga kuwafikia wasichana waliopo shuleni 15,954 ambao watanufaika kwa kupata fedha Sh. 25,000 kila mwezi.

Aidha, upande wa wanawake vijana waliopo mitaani 14,295 watanufaika kwa kufundishwa stadi za maisha ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa biashara ndogondogo. Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo jana uliofanyika katika kijiji cha Chikola wilayani Bahi, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi nchini (Tacaids) Dk. Leonard Maboko, alisema mradi huo ni wa majaribio katika mikoa mitatu na halmashauri 10 nchini.

Alisema, mradi huo umekuja kutokana na takwimu kuonyesha maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi kwa vijana wa umri huo kuwa ni asilimia 40, huku kati yao wasichana ni asilima 80 ya maambukizi yote.

Alibainisha kuwa lengo la mradi huo ni kuwawezesha wasichana walio katika rika la balehe shuleni pamoja na wanawake vijana waliopo mitaani ili waweze kuondokana na vishawishi vitakavyowasababishia kupata maambukizi.

Dk. Maboko alisema fedha watakazopatiwa wasichana wa shuleni zitawasaidia kujikimu katika mahitaji mbalimbali ikiwamo kujinunulia taulo za kike.

"Hawa walengwa wa shuleni watapata Sh. 25,000 kila mwezi kwa miaka mitatu ambazo zitawasaidia kujikimu katika mahitaji mbalimbali kwa kununua taulo za kike na mahitaji mengine ya shule," alisema.

Alifafanua kuwa kwa upande wa wanawake vijana waliopo nje ya mfumo wa shule wao watanufaika kwa kufundishwa stadi za maisha kwa kutengeneza mpango wa biashara.

"Wanafundishwa na kuandaa mpango wa biashara kwa kusaidiwa na maofisa ugavi na akiwasilisha huo mpango anapatiwa asilimia 60 ya fedha kwa ajili ya kuanza biashara na baadaye atafuatiliwa akionekana anafanya vizuri anamaliziwa asilimia 40 iliyobaki, na kama mpango wake utakubalika anapata fedha isiyozidi Sh. 400,000 ambacho siyo haba katika mtaji wa biashara kwa kuwa kuna watu walianza na Sh. 10,000," alisema.

Naye, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko, aliwataka walengwa katika mradi huo kuitumia fursa hiyo kikamilifu.

"Mliopo shuleni mtumie mradi huu kikamilifu ili muweze kufikia malengo yenu katika elimu, lakini kwa wale wa mitaani mnatakiwa kutumia vipaji vyenu mlivyojaliwa ili muweze kujishughulisha katika kuanzisha biashara ili mjikimu kimaisha," alisema.

Mmoja wa wanafunzi ya Shule ya Msingi Chikola, Maria Severin, alisema tangu kuanza kwa mradi huo umewezesha kuongeza mahudhurio shuleni kutokana na kupata mahitaji yote.

Alisema fedha hizo zimewasaidia kununua sare za shule, madaftari pamoja na taulo za kike ambazo awali zilikuwa zinachangia wao kukosa vipindi kila mwezi.

"Hivi sasa tunashiriki vipindi vyote shuleni kutokana na kupatiwa fedha kiasi cha Sh. 25,000 kila mwezi ambazo tunazitumia kununua mahitaji yetu mbalimbali na imetusaidia kujiepusha na vishawishi mitaani," alisema.

Mradi huo unatekelezwa katika mikoa ya Dodoma, Singida na Morogoro katika halmashauri za Bahi, Kongwa, Mpwapwa, Ulanga, Malinyi, Singida Dc, Iramba, Kilombero na Kondoa Mjini,




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Albert Jonkergouw, katika futari iliyoandaliwa na Benki ya NMB kwa masheikh wa mikoa ya kanda ya kati, wazee wa Dodoma, wabunge, viongozi wa dini, wananchi, wawakilishi wa taasisi mbalimbali na wafanyakazi wa NMB kwenye hoteli ya Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jafo asisitiza utoaji wa asilimia 10 ya mapato

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amezitaka halmashauri nchini kuhakikisha asilimia 10 ya mapato yao ya ndani inapelekwa moja kwa moja kwenye vikundi vya wanawake na vijana na watu wenye ulemavu ili kuwainua kiuchumi.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki katika hafla ya kukabidhi hundi ya Sh. bilioni 1.06 kutoka katika mapato ya ndani ya Jiji la Dodoma kwa mwaka wa fedha 2018/19 kwa vikundi 201.

Alisema kuwa jiji hilo linafanya vizuri katika utoaji wa fedha hizo na kuzitaka halmashauri zingine zihakikishe zinatoa fedha hizo kwa wakati kwa vikundi hivyo.

"Jiji la Dodoma limekuwa la mfano katika mambo mengi kuanzia ukusanyaji wa mapato wameongoza katika pato ghafi na leo hii wametekeleza kwa vitendo Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura Na, 290, kifungu 37A na kanuni zake za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2019," alisema.


Aliutaka uongozi wa jiji hilo kukaa pamoja na wadau kubuni na kuanzisha mradi mkubwa ambao utaweza kuwanufaisha makundi maalumu ambao utatekelezwa kwa kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani. "Unajua wananchi wetu wanataka kufanikiwa katika biashara na pia wanapendelea biashara kubwa, hivyo mkibuni mradi mkawatengenezea vizuri kisha mkawakabidhi kama sehemu ya mkopo itawajenga na kubadilisha maisha yao kuliko kila siku kuwapa fedha ni vyema wakati mwingine mkawapa vitega uchumi," alisema.

Naye, Meya wa jiji hilo, Prof. Davis Mwamfupe, alisema pamoja na jiji kutoa mikopo hiyo pia wameanza kutafuta vyuo vya kutoa ujuzi na maarifa zaidi kwa wanufaika wa mikopo ili iweze kuwa na tija zaidi.

Awali, Mkurugenzi wa jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 2.6 zilitengwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 na kwamba Sh. bilioni 1.79 kimeshatolea katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2018.

"Fedha za vikundi unazokabidhi leo kiasi cha shilingi 1,062,500,000 zinaifanya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa mwaka wa fedha 2018/19 kutoa mikopo ya jumla ya Sh. bilioni 2.8 sawa na asilimia 109.6 ya malengo tuliyojiwekea," alisema Kunambi.

Alieleza kuanzia mwaka 2015/16 mpaka sasa ni vikundi 1,020 vyenye jumla ya wanachama 10,200 vimenufaika vikiwa na mzunguko wa jumla ya Sh. bilioni 3.4.





Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na Kati wa Benki ya Exim Tanzania, Andrew Lyimo (kulia), akizungumza na baadhi ya wateja wa benki hiyo pamoja na wageni waalikwa wakiwamo Waziri wa Habari, Michezo, Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Mahamoud Thabit Kombo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi, wakati wa hafla ya futari mwishoni mwa wiki kwa ajili ya wateja wa benki hiyo Zanzibar. **MPIGAPICHA WETU**

# WB yafurahishwa utekelezaji miradi ya Tasaf

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya Dunia (WB) imeridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo Tasaf visiwani Zanzibar na kujionea maendeleo yaliyopatikana kwa walengwa wa mradi huo.

Akizungumza baada ya kuwatembelea walengwa wa mradi huo katika Kijiji cha Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja, Mwakilishi wa benki hiyo Muderius Abdillah, alisema amefurahishwa kuona fedha zilizotolewa zimetumika kama ilivyokusudiwa.

Alisema amefurahishwa kuona jinsi walengwa wa mradi huo walivyopiga hatua kimaendeleo kwa kujikomboa kiuchumi na kupunguza hali ya umaskini.

"Kwa kweli nimefurahi sana nimewaona walengwa jinsi walivyoanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo hongereni sana," alisema.

Mwakilishi huyo akiwa ameambatana na wenzie kutoka Benki ya Dunia, alisema hivi sasa wapo katika mkakati wa kuhakikisha benki hiyo inatoa fedha nyingine ili kuendelea na Tasaf kwa awamu ya pili.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed, alisema kuna mafanikio makubwa katika kaya zinazonufaika na mfuko wa miradi ya maendeleo kwa jamii Tasaf chini ya ufadhili wa benki hiyo, Zanzibar.

Alisema kwa kipindi kirefu baadhi ya wananchi katika maeneo ya visiwani Zanzibar walikuwa katika hali duni ya umaskini, lakini baada ya uwapo wa miradi hiyo maisha yao yamebadilika kutoka hali duni na kuwa wenye kujiweza.

Aboud alisema licha ya maendeleo makubwa kupatikana kwa wananchi, lakini pia kuna idadi kubwa ya baadhi ya watoto walishakataa kwenda shule, lakini kupitia mradi huo watoto hao walifanikiwa kurudi na hadi sasa wapo shuleni wanaendelea na masomo.

"Hivi sasa kinamama wamekuwa wakulima wa mazao pamoja na miti ya biashara sambamba na shughuli tofauti za ujasiriamali na wamekuwa mfano kwenye jamii zetu," alisema.

Aidha, aliuhakikishia ujumbe wa Benki ya Dunia kuwa serikali itaendelea kuwa makini na kuhakikisha kila mradi unaotolewa na Tasaf kwa ufadhili wa benki hiyo unaratibiwa na kufanikiwa ipasavyo kwa lengo la kuwasaidia wengi.

Baadhi ya wanufaika wa miradi hiyo katika shehia ya Kitogani walisema kuna mabadiliko makubwa ya kimaendeleo.

Mmoja wa wanafuaika hao, Mwatima Ameir, alisema licha ya uwapo wa mafanikio hayo, bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika eneo hilo ikiwamo ukosefu wa maji ya uhakika ambayo yangeweza kuwasadia katika kilimo cha umwagiliaji.

Aidha, alisema watahitaji wataalamu wa kilimo ili waweze kupatiwa elimu hasa pale mashamba yao yanaposhambuliwa na wadudu waharibifu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladislaus Mwamanga, alisema kutokana na mafanikio makubwa ya miradi mbalimbali, Benki ya Dunia kwa kushirikiana na serikali zote mbili wamekubali kuendelea na ufadhili wa miradi mingine kwa awamu ya miaka minne ijayo.

Alisema hayo yote yamekuja kutokana na uwajibikaji mkubwa unaofanywa na serikali kwa kuhakikisha wanufaika wa miradi hiyo wanafanya yale yanayotakiwa.

Hata hivyo, aliwataka wanufaika hao ambao tayari wamejiweza kuachia wengine ambao bado hali zao ni duni kimaisha kwa lengo la kutoka kwenye umaskini.

# Tamwa yaomba mashahidi kujitokeza ukatili wa kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania(Tamwa), kimeomba jamii kutoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha mashahidi wa vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake na watoto wanafika katika vyombo vya sheria ili haki iweze kupatikana.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema zaidi ya kesi 17 zimeripotiwa ndani ya miaka mitatu (2016 - 2019) kwa wanawake kufanyiwa ukatili hadi kufa ikiwamo kubakwa, lakini hadi sasa hukumu za kesi hizo hazijatoka kutokana na kile kinachoelezwa kutokujulikana kwa wahalifu.

Alieleza kuwa madai ya kesi ya ubakaji wa kundi iliyotokea Novemba mwaka jana huko Bungi, Mkoa wa Kusini Unguja dhidi ya mwanamke wa miaka 35, imekuwa tofauti baada ya watuhumiwa wapatao watano kushikiliwa na kuwekwa rumande. Alisema hayo ni maendeleo katika utafutaji wa haki na kulinda heshima ya mwanamke na mtoto katika jitihada za kukomesha vitendo vya udhalilishaji.

"La kusikitisha katika kadhia hiyo ni kuwa yule aliyedaiwa kubakwa ameshindwa kuendelea na kesi jambo ambalo linatishia mwendelezo wa kesi hiyo," alisema.

Alieleza kuwa kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari, Mei 8, mwaka huu, wakili wa upande wa utetezi, Juma Kumba, alidai kuwa mwathirika huyo amekuwa akishindwa kufika mahakamani kila tarehe ya kesi na hivyo kuitaka mahakama kutoa hati ya kukamatwa ambaye ndiye shahidi muhimu katika kesi hiyo au kesi iondolewe mahakamani.

Dk. Mzuri alisema endapo kesi hiyo itafungwa itakuwa ni pigo kubwa kwa watetezi wa haki na jamii kwa ujumla kwa vile kutasababisha kutotolewa hukumu stahiki kwa wabakaji na kudumaza jitihada za kuwalinda wasio na nguvu wala hatia wakiwamo wanawake na watoto.

"Ni imani yetu kuwa jamii itafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha kuwa shahidi huyo muhimu katika kesi hii anapatikana na kushauriwa kufika mahakamani hapo, mahakama itakapokaa tena tarehe 27 Mei, mwaka huu," alisema.

Aidha, alisema ni vyema pia vyombo vya sheria ikiwamo mahakama kuelewa kuwa mwathirika wa matendo kama hayo huumia vibaya hadi kisaikolojia, hivyo busara na ushirikiano wa wanajamii na vyombo hivyo yanahitajika ili ku kutoa haki kwa pande zote.

# Balozi Iddi asisitiza jamii kuitunza amani, umoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameitaka jamii kuendeleza kuitunza amani na kudumisha umoja miongoni mwao inayotoa fursa kwao kufanya shughuli zao za kimaisha bila ya wasiwasi.

Alisema mataifa mengine amani imekuwa adimu kuipata kutokana na uhasama usiokwisha.

Alisema taifa limeweza kupiga hatua kubwa katika kuimarisha uchumi na maendeleo ya wananchi wake kulikosababishwa na uwapo wa amani ambayo haikuja bure bali ni jitihada zilizochukuliwa na wananchi wenyewe chini ya usimamizi wa viongozi wao wa kitaifa.

Balozi Iddi aliyasema hayo katika salamu za ukumbusho zilizotolewa kwa niaba yake na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman Abdullah, baada ya futari ya pamoja iliyowajumuisha wawakilishi wa wananchi wa mikoa miwili ya Pemba iliyofanyika Chake Chake, Pemba.

Alisema wapo baadhi ya binadamu wa mataifa tofauti duniani ambao kipindi hiki cha Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan wanafunga na kufutari katika kambi za wakimbizi kufuatia mataifa yao kuyeyuka kwa amani iliyokosekana kutokana na vurugu za kuhatarisha maisha yao.

"Amani lazima iendelee kuwapo nchini kwa vile hakuna jaribio wala mbadala kwenye suala hilo muhimu katika maisha na ustawi wa kila siku wa mwanadamu," alisema Balozi Iddi.

Aidha, alisema kwa vile jamii imekuwa huru na shwari katika harakati zao za kimaisha ndani ya amani iliyopo, aliwahimiza waumini wa dini ya Kiislamu kudumisha suala la ibada kwa vile ni wajibu kwao kufanya hivyo.

Alieleza kuwa mwanadamu uwapo wake ulimwenguni kaumbiwa kwa kazi moja ya kumuabudu mola wake aliyemuumba hivyo mja huyo analazimika kujiwekea malengo imara katika maisha yake ya kudumu atakaporejea katika himaya ya mola wake.

Mkuu wa Mkoa huyo wa Kusini Pemba, aliwapa pole wananchi wenzao wa Unguja waliopatwa na maafa kufuatia mvua kubwa za masika zinazoendelea kunyesha nchini.

Hemed alisema wananchi wa Pemba wanaungana na wenzao wa Unguja waliopatwa na mtihani huo katika kipindi hiki kigumu cha ukosefu wa makazi yao ya kudumu baada ya nyumba zao kujaa maji.

# Viwanja vya ndege watolewa hofu mifuko ya plastiki

**Na Gwamaka Alipipi**

ZIKIWA zimebaki siku tano kuanza kwa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki nchini, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewatoa hofu watumiaji wa viwanja vya ndege nchini, kuna mifuko ambayo itaendelea kutumika katika maeneo hayo.

Taarifa iliyotolewa jana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) ilimnukuu Mwanasheria wa NEMC, Manchare Heche, akieleza kuwa kwa viwanja vya ndege ipo mifuko ambayo itaendelea kutumika kwa mujibu wa Kanuni Namba tisa ya Sheria ya Kuzuia Matumizi ya Mifuko ya Plastiki ya Mwaka 2019.

Alisema baada ya kutumika mifuko hiyo inatakiwa ihifadhiwe sehemu maalum na kupekekwa mahali itakapo teketezwa.

"Katazo linahusu Watanzania wote na wageni, hapa Airport (uwanja wa ndege) wapo wanaotumia nikiwa na maana ya wafanyakazi na wateja wakiwamo abiria, lakini kwenye kanuni ipo mifuko ya vifungashio ambayo haijazuiwa kama ile ya kuhifadhi vyakula, dawa, kilimo na inayohifadhia takataka," alisema Heche na kuongeza:

"Mfano korosho au keki wanazopewa abiria kwenye ndege mfuko wake upo katika kipengele cha chakula, hivyo itaendelea kutumika lakini baada ya matumizi tu itahifadhiwa sehemu iliyoelekezwa tayari kwa kuteketezwa."

Alisema kwa plastiki zinazotumika kufungia mizigo ya abiria wanaosafiri kutoka ndani na nje ya nchi kwa usafiri wa ndege, itatakiwa kuondolewa wakati abiria anapofika nchini, zitakusanywa na kuhifadhiwa maeneo maalum kabla ya kupelekwa eneo lililotengwa kwa ajili ya kuziteketeza.

Alisema matumizi makubwa ya mifuko ya plastiki nchini yamesababisha uharibifu wa mazingira, ikiwamo ya kuziba kwenye mifereji ya maji, kuua wanyama, na kuharibu ardhi.

Kwa mujibu wa Heche, serikali imefuta leseni za viwanda vinavyotengeneza mifuko ya plastiki na kwamba haijatoa tena leseni kwa wale leseni zao zilizomaliza muda.

Aidha, alitoa angalizo kwa wanaohusika na ukamataji wa watumiaji wa mifuko hiyo, kutotumia nguvu ili kuepusha mikwaruzano na kutoelewana.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanadai vitambulisho kwa wale wote watakaofika kwenye maeneo yao kwa ajili ya kukagua mifuko hiyo ya plastiki.

Mkurugenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Paul Rwegasha, alisema TAA, imeshatoa taarifa kwenye vituo vyote vya kimataifa, mashirika ya ndege yanayoleta abiria Tanzania juu ya katazo la mifuko ya plastiki.

"Hii taarifa inajulikana kitaalamu kama 'timatic pre-information' ambayo inatumwa kwenye vituo vyote duniani, ambapo kuna shirika la ndege ambalo linaleta abiria Tanzania itakuwa rahisi wao kupata taarifa ya katazo hilo na kuwafanya wasibebe mifuko hiyo," alisema Rwegasha.

Aidha, aliwataka wadau wote wanaofanya shughuli mbalimbali kwenye viwanja vya ndege kutoa ushirikiano kuwaeleza abiria juu ya katazo hilo.

# Wanafunzi wakosoa mapango ya Amboni

**Na Dege Masoli,** TANGA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya St. Pio iliyopo Kibaigwa mkoani Dodoma, wamekosoa matumizi ya tochi za kuwaongoza wageni wanaotembelea kwenye mapango ya Amboni kwamba mfumo huo unawanyima haki ya msingi watalii kwa kutoona kwa usahihi vivutio hivyo.

Ushauri huo ulitolewa na wanafunzi hao waliyofanya ziara ya kujifunza ambapo walitembelea maeneo mbalimbali ya kihistoria yakiwamo mapango ya Amboni yaliyopo nje kidogo mwa Jiji la Tanga.

Rechel Mtuli, mwanafunzi wa kidato cha nne akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema mfumo wa matumizi ya tochi kwenye mapango hayo unaotumika hivi sasa haufai badala yake alishauri kuwekwa umeme ili kuruhusu mwanga wa kutosha, hivyo watakuwa wamewatendea haki wageni wanaotembelea maeneo hayo.

Mtuli alisema matumizi ya tochi ndani ya mapango hayo yanaweza kuwafanya wengi kutofurahia kile walichoelezwa na wataalamu kabla ya kuingia humo kwa madai ya kuwapo na mwanga hafifu kutokana na udhaifu wa vifaa hivyo vinavyotumika.

"Matumizi ya umeme kutayafanya kuwapo na mwanga wa kutosha ndani ya mapango hayo, hivyo vitu vingi kutoonekana vema na kuwafanya wageni kujionea uhalisia wa maeneo wanayoonyeshwa," alisisitiza Mtuli.

Hata hivyo, alielezea kufurahishwa na mambo ya asili waliyojifunza pamoja na utaalamu wa namna ya kuandaa, kufungasha na kusafirisha maziwa kitaalamu walipokitembelea kiwanda cha maziwa cha Tangafresh kilichopo Jiji la Tanga.

Pierre Samwel wa kidato cha tatu, alieleza kufurahishwa na sanamu za ndege na Bikira Maria alizoziona katika mapango hayo, huku akiutaka uongozi wa kiwanda cha Tangafresh kujitanua ili kukidhi mahitaji ya walaji wengi.

Naye mkuu wa msafara huo, Elia Lesilwa, aliishauri serikali kuimarisha miundombinu mbalimbali ikiwamo barabara katika vivutio hivyo ili yaendane na hadhi na hali halisi ya kihistoria ya eneo hilo. Lesilwa alipendekeza kuwapo usafiri maalumu kama ilivyo katika hifadhi za wanyama.



Kundi la wananchi kutoka katika kata nane za Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, wakisubiri foleni ya kupatiwa huduma za afya bure katika Shule ya Msingi Ngulyati kutoka kwa madaktari zaidi ya 50 waliopelekwa na Kampuni ya Alliance Ginnery wilayani humo, kwa kushirikiana na Taasisi ya kiislamu ya The Islamic Faundation. **PICHA: HAPPY SEVERINE.**

# Mamia wachangamkia matibabu bure

**Na Happy Severine,** SIMIYU

ZAIDI ya wakazi 4,000 kutoka kata nane za Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu wamejitokeza kwa wingi katika Shule ya Msingi Ngulyati kwa ajili ya kupatiwa huduma za afya bure kutoka kwa madaktari bingwa zaidi ya 20.

Wananchi hao wametoka katika kata za Gamboshi, Kilalo, Sakwe, Ngulyati, Mwasubuya, Kasori, Mhango na Itubukilo, ambapo kata zote hizo zipo Wilaya ya Bariadi.

Madaktari waliohusika kutoa huduma kwa siku mbili juzi na jana wametoka Mwanza, Shinyanga na Simiyu kwa ufadhili wa na taasisi ya kiislam ya The Islamic Foundation chini ya uratibu wa kampuni ya pamba ya Alliance Ginnery iliyopo wilayani humo.

Kaimu Mkurugenzi wa The Islamic Foundation, Mubaraka Said, alisema wameamua kutoa huduma hizo kwa wananchi ikiwa ni moja ya malengo yao makuu ya kusaidia jamii kwa kuwaunganisha Watanzania bila kujali dini wala makabila yao.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa huduma hizo kwa miaka minane tangu kuanzishwa kwake na wamekuwa wakifanya hivyo wakati wa kipindi cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kama moja ya nguzo kuu ya dini ya kiislamu.

"Tumekuwa tukitoa huduma hizi bure ambapo kwa upande wa afya tunatoa dawa, vipimo na ushauri bure na tumejikita sana kwa wananchi wa vijijini, ambapo wamekuwa wakijitokeza kwa wingi kupata huduma hizo," alisema Said.

Meneja wa kampuni ya Alliance, Boaz Ogola, alisema wao kama wawekezaji kwenye maeneo ya wananchi wamekuwa wakitoa huduma kwa jamii ikiwa ni moja ya njia ya kudumisha ushirikiano na kurejesha faida kwa jamii inayoipata kampuni.

Naye Christine Magumba, mwananchi ambaye amepata huduma bure kutoka kwa madaktari hao, alisema anashukuru kupatiwa huduma hizo pamoja na dawa bure, huku akiomba huduma hizo kutolewa mara kwa mara.

## HABARI KIMATAIFA

## Chanjo ya ebola yafanyiwa tathmini itumike Afrika Mashariki

**KINSHASA, Congo**

WAKATI timu ya kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa ebola ikiendelea kuhangaika kuudhibiti ugonjwa huo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, mawaziri wa afya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wamesema wanatambua hatari zake na wanatathmini kuanza kutumia chanjo ya ugonjwa huo iliyoko kwenye majaribio.

Katika kipindi cha hivi karibuni, vituo vinavyotibu ebola nchini Congo vimekuwa vikishambuliwa na hivyo wafanyakazi wanaokabiliana na ugonjwa huo kushindwa kufikia maeneo yenye milipuko.

Vyanzo vya habari kutoka Afrika Mashariki vimeripoti kuwa, hivi sasa nchi sita, hasa zile zilizoko mpakani na majimbo ya Kivu Kaskazini na Ituri nchini DRC, ambako milipuko ya ugonjwa huo iliendelea kwa kasi, wanakabiliana na vikwazo vyote kuhakikisha wanaweza kwa ufanisi kufikisha matibabu pale ambapo imethibitishwa ebola ipo.

Uganda, Burundi na Rwanda ni maeneo yaliyo na hatari kubwa ya maambukizi, wakati baadhi ya sehemu za Sudan Kusini na Tanzania ambayo yako karibu na miji iliyoko mpakani yanakabiliwa na hatari ya wastani ya maambukizo hayo.

Gazeti la The East African limemnukuu Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya kwenye Sekretarieti ya EAC Arusha, Dk. Michael Katende, akieleza uamuzi wa kutumia chanjo ya ebola.

Dk. Katende alisema ni jambo la busara kuwakinga wafanyakazi walioko mstari wa mbele kukabiliana na ugonjwa huu pamoja na wilaya zinazokabiliwa na tishio la maambukizi.

Alisema kinga ambayo imeanza kuonyesha matumaini ni bora kuliko ambayo haijaonyesha, ni bora kuwa na kitu ambacho kinakupa kinga kuliko kutokuwa na kinga yoyote kabisa.

*VOA*

# Rwanda, Uganda katika mzozo mwingine

**KAMPALA, Uganda**

NCHI za Uganda na Rwanda zimetupiana maneno baada ya Polisi wa Uganda kuwatuhumu wanajeshi wa Rwanda kuingia kwenye mpaka wa nchi yake na kutekeleza mauaji ya watu wawili, tukio ambalo limezidisha joto la mzozo baina ya nchi hizi mbili.

Hata hivyo, nchi ya Rwanda imekanusha tuhuma hizo na kueleza kuwa tukio hilo liltokea kwenye mpaka wake baada ya maofisa wake kushambuliwa kwa mapanga.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Uganda imesema kuwa: "Serikali ya Uganda inakemea kwa nguvu zote ukiukwaji wa haki za kimipaka na wanajeshi wa Rwanda pamoja na uhalifu, vurugu na mauaji ya raia wasio na hatia."

Uhusiano kati ya Rais wa Rwanda, Paul Kagame na mwenzake wa Uganda, Yoweri Museveni ambao wakati fulani walikuwa washirika wakubwa, umeendelea kufifia tangu mwanzoni mwa mwaka huu, ambapo nchi hizi zinatuhumiana kwa makosa ya uhaini, mauaji ya kisiasa na kuingiliana na masuala ya ndani.

Taarifa ya Jeshi la Polisi la Rwanda imesema kuwa, wanausalama wake walishambuliwa na watu waliokuwa na mapanga baada ya kuisimamisha pikipiki moja waliyohisi ilikuwa imeingiza vitu kimagendo ikitokea Uganda.

"Maofisa wetu waliwapiga watu wawili risasi, mmoja raia wa Rwanda ambaye alikufa papohapo na raia mmoja wa Uganda ambaye naye alifariki baadaye," ilieleza taarifa hiyo.

Awali polisi wa Uganda walieleza tukio hilo lilitokea majira ya saa mbili usiku, siku ya Ijumaa katika kituo cha mpaka kijiji cha Kiruhura kwenye Wilaya ya Rukiga magharibi mwa nchi hiyo.

Nchi ya Rwanda imepunguza uagizaji wa bidhaa kutoka Uganda, ambapo miezi michache iliyopita ilizuia raia wake kusafiri kwenda Uganda.

Hatua hiyo ilisababisha pia Uganda ambayo nayo iliwakataza raia wake kutumia mpaka huo wa Rwanda.

Wataalamu wanaonya kuwa mzozo kati ya Rwanda na Uganda unatishia mustakabali wa ukuaji wa uchumi wa ukanda pamoja na utengamano hasa katika eneo ambalo kwa miongo kadhaa limeshuhudia baadhi ya nchi wanachama zikiwa kwenye vurugu za wenyewe kwa wenyewe.

Rais Museveni amekiri kuwa aliwahi kukutana na wapinzani wa Rais Kagame, lakini amekanusha kuwa hata mara moja hajawahi kutangaza kuunga mkono harakati za urasi dhidi ya Serikali ya Rwanda.

Mzozo huu ulishika kasi mwezi Machi wakati Rwanda ilipoeleza hadharani na kuituhumu Uganda kwa kuwateka raia wake na kuwaunga mkono waasi ambao wanataka kuipindua serikali.

*RFI*



Rais wa Uganda, Yoweri Museveni (kushoto), akiwa na Rais wa Rwanda, Paul Kagame. **PICHA: REUTERS**

# Apigwa faini kwa kosa la kujikuna akiendesha gari

**BEIJING, China**

MWANAUME mmoja kutoka mashariki mwa China amepigwa faini baada ya kamera ya polisi wa usalama barabarani (trafiki) kumwonesha akiwa anajikuna usoni, huku akiendesha gari.

Kwa mujibu wa chapisho la gazeti la Jilu Evening, liliandika kuwa Liu alikuwa anaendesha gari katika Jimbo la Shandong na huku akiwa anajikuna wakati anapita katika kamera ya trafiki.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa, Liu alipokea ujumbe unaomwambia kuwa amevunja sheria barabarani kwa kuendesha gari huku akiwa anajikuna usoni.

Picha ya kosa ambalo alikuwa amelifanya liliambatanishwa katika ujumbe huo wa kuvunja sheria.

Baada ya kutumiwa ujumbe huo, Liu pia aliambiwa kuwa ataondolewa pointi mbili katika leseni yake na vilevile alitakiwa kulipa dola saba kama faini.

"Huwa nawaona watu mitandaoni wakiwa wamekamatwa kwa kosa la kuendesha huku wamewashika wenza wao, lakini mimi nimekamatwa kwa kosa la kujishika mwenyewe ndio nimeonekana kuwa nimevunja sheria, inashangaza!" Alisema Liu. Hata hivyo, Liu alisema atawasiliana na mamlaka husika ili kupata suluhisho ya tatizo lake.

Gazeti la Global Times liliandika kuwa trafiki wamefuta risiti ya makosa waliomwandikia Liu na kumwambia kuwa kamera yao huwa inarekodi mwendo wa dereva moja kwa moja, ndio maana kujikuna kwake usoni kulimweka matatani na kuonekana kama anaongea na simu.

Picha yake ilizua gumzo mtandaoni huku watu wengine wakieleza kuwa mfumo huo unaaibisha sana, watu wanakuwa hawana faragha.

"Je, hakuna umuhimu kwa Wachina kuwa na faragha?" Mtu mmoja alihoji kwenye mtandao wa jamii, akikomenti kwenye picha ya Liu.

Kamera zaidi ya milioni 170 zimefungwa kwenye barabara nchini China na nyingine milioni 400 zinatarajiwa kufungwa mwakani.

Kamera hizo zimewekwa huku zikiwa na teknolojia inayoweza kutambua mwonekano wa watu na kujua umri, jinsia na eneo walilotoka.

*BBC*

# Mkuchika apongeza Tasaf kupata hati safi

Na Elizabeth Zaya

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, ameupongeza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kuendelea kupata hati safi na kuutaka kuendelea kutunza sifa hiyo pamoja na taasisi nyingine zilizo chini yake.

Mkuchika alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam, wakati akizindua kamati mpya ya uongozi ya Taifa ya Tasaf iliyoteuliwa hivi karibuni na Rais John Magufuli, huku akitamba kwamba hiyo ndiyo siri pekee itakayomsaidia pamoja na mambo mengine kuendelea kuaminika katika nafasi hiyo aliyopo kwa kuhakikisha anazisimamia vema taasisi hizo zilizo chini yake.

Mkuchika alisema siri kubwa ambayo imemsaidia aendelee kuaminika katika nafasi za juu za uongozi ni kutokana na kusimamia vema na kuhakikisha taasisi zote anazoziongoza zinafanya kazi kwa weledi na ufanisi na kuhakikisha pamoja na mambo mengine, zinapata hati safi.

"Niipongeze sana Tasaf imefanya kazi nzuri sana na ndiyo maana tunaona maombi ni mengi kwa viongozi, kila mmoja anataka mpango ufike katika mkoa wake. Hii inaonyesha kwamba wanaona katika maeneo yaliyofikiwa imefanya kazi nzuri ingekuwa haijafanya vizuri kusingekuwa na maombi mengi kama ilivyo sasa," alisema Mkuchika na kuongeza:

"Lakini pamoja na hivyo niipongeze kwa sababu miaka yote imekuwa ikipata hati safi, naamini ni kutokana na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi na inawezekana pia ukali kutoka kwa watendaji waliopo nao unachangia. Niiombe Tasaf iendelee kutunza sifa hii pamoja na taasisi nyingine zote zilizo chini yangu."

Mkuchika alisema amekuwa akishuhudia mawaziri wengi katika vipindi tofauti vya uongozi wakilazimika kujiuzulu au kuondolewa katika nafasi zao kutokana na taasisi zao kupata hati chafu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

"Naamini kwamba mafanikio haya yametokana na juhudi kubwa ambayo imekuwa ikifanywa na watendaji wa mfuko na kamati ambayo imemaliza muda wake," alisema Mkuchika.

Alisema alipo na mazuri hapawezi kukosekana na mabaya na hata kama yapo madogo madogo aliomba wapambane nayo na kuyaondoa kabisa hasa kwa kuhakikisha fedha zinazotolewa zinawafikia walengwa. Pia, aliishauri Tasaf kutafuta vyanzo mbadala ambavyo vitasaidia miradi inayoiendesha kuwa endelevu badala ya kutegemea wafadhili pekee.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladislaus Mwamanga, alisema mpango huo umechangia kwa kiwango kikubwa kupunguza umaskini ikiwamo kupambana na tatizo la lishe, kuchangia katika sekta ya elimu na afya.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na kumpongeza Rais Azali Assouman wa Comoro, baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Visiwa vya Comoro jana katika wa uwanja mpya wa Ominisport Malouzini Stadium Comoro. **PICHA: OMR**

# Magufuli, Ramaphosa wazungumza

Na Mwandishi Wetu

RAIS John Magufuli jana alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, Ikulu jijini Pretoria.

Katika mazungumzo hayo, Rais Magufuli alimpongeza Rais Ramaphosa kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Afrika Kusini na amemhakikishia kuwa Tanzania itadumisha uhusiano na ushirikiano wa kidugu na kihistoria na nchi hiyo ulioasisiwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Nelson Mandela kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha ANC (African National Congress).

Rais Magufuli alimshukuru, Rais Ramaphosa kwa kumkaribisha kufanya naye mazungumzo siku moja baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Afrika Kusini na alibainisha kuwa anatarajia uhusiano wa Tanzania na Afrika Kusini utaimarishwa zaidi katika masuala ya uchumi na kukuza lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wake, Rais Ramaphosa alimshukuru Rais Magufuli kwa kuhudhuria sherehe za kuapishwa kwake, na amemhakikishia kuwa Afrika Kusini inatambua mchango mkubwa wa Tanzania katika ukombozi wa Taifa hilo, na kwamba katika kipindi chake cha uongozi wake atauendeleza na kuuza zaidi uhusiano huo.

Rais Ramaphosa amesema kufuatia uamuzi wa Afrika Kusini kuanza kufundisha lugha ya Kiswahili, nchi yake itachukua walimu wa Kiswahili kutoka Tanzania ili watumike kufundisha somo hilo katika shule za msingi na sekondari.

Aidha, Mhe. Rais Ramaphosa aliahidi kufanya ziara rasmi ya kitaifa nchini kabla ya Mkutano wa 39 wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) uliopangwa kufanyika mwezi Agosti 2019 Tanzania. Na pia atahudhuria mkutano huo.

Kabla ya mazungumzo hayo Rais Magufuli ambaye ameongozana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alimkabidhi Rais Ramaphosa zawadi ya vitabu vya kusoma na kufundishia lugha ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Rais Magufuli na Rais Ramaphosa wamefanya mazungumzo hayo ikiwa ni kabla Rais Ramaphosa hajatangaza Baraza lake la Mawaziri.

Rais Magufuli leo ataondoka Afrika Kusini na kuelekea Namibia ambako atafanya ziara ya kitaifa kwa mwaliko wa Rais wa Namibia, Hage Geingob.

## Wanafunzi 300 wapata ujauzito

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

WANAFUNZI 351 mkoani Shinyanga wameripotiwa kukatishwa masomo kutokana na ujauzito, huku 31 wakiolewa ndoa za utotoni.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Katibu Tawala Msaidizi Utumishi na Utawala, mkoani Shinyanga, Amos Machiliwa, kwenye kikao cha mpango mkakati wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto mkoani humo, kilichoandaliwa na Shirika la Kimataifa la ICS linalotetea haki za wanawake na watoto.

Alisema Takwimu za mwaka (2016 –2018) jumla ya wanafunzi 351 mkoani Shinyanga walikatishwa masomo yao kwa sababu ya ujauzito, huku mwaka jana wanafunzi 31 waliolewa ndoa za utotoni.

Aidha, aliyataka mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na watendaji wa serikali wakiwamo maofisa ustawi wa jamii, wanasheria pamoja na mahakimu, kuongeza nguvu za kutokomeza vitendo hivyo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto zikiwamo mimba na ndoa za utotoni pamoja na kuwafunga jela wahusika.

Pia aliwataka washiriki wa kikao hicho waweke vipaumbele vyao katika kusimamia mashauri ya watoto kwa madai ya kukosekana kwa ushahidi, jambo ambalo litasaidia kupunguza ukatili ndani ya jamii zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

"Kwenye mikakati yenu pia mkajikite kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya mimba na ndoa za utotoni, pamoja na kuwaelezea umuhimu wa elimu na kumthamini mtoto wa kike na siyo kuendekeza tamaa ya kupata mifugo na kuzima ndoto za wanafunzi," alisema Machiliwa.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho akiwamo Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Kahama Mji, Ibrahimu Nuru, alisema changamoto wanayokabiliana nayo ni jamii kuendelea kukumbatia masuala ya mila na desturi kandamizi.

**"Kwenye mikakati yenu pia mkajikite kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya mimba na ndoa za utotoni, pamoja na kuwaelezea umuhimu wa elimu na kumthamini mtoto wa kike...**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI,** Tunahitaji Fundi wa COMPUTER na CCTV CAMERA Awe na Uzoefu wa mwaka mmoja Awe na Diploma. Mawasiliano: 0713 164462/ 2110836

**SALES LADY ANAHITAJIKA,** SALES LADY ANAHITAJIKA MWENYE UZOEFU WA COMPUTER, MITANDO YA KIJAMII INSTAGRAM NA FACE BOOK. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: 0715 88 55 33.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

## KUPOTEA KWA KADI

Ingiahed Ernest Mzava anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili wa namba MC653 BTC aina ya TVS.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: KJN/B.I/I/VOL/2003/2019**

115248302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA: 63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya............TANGA**
**Wilaya ya ......TANGA**
**MADAI NAMBARI .....39....ya...2019**
**Mdai ..............FATUMA ALLY SHEMPONDA**
**Mdaiwa .........AHMED ABITALIB**
**Kwa:............AHMED ABITALIB**
**C/o....M/KITI MTAA B/B 11 TANGA**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba eleza hapa habari ya madai

UNADAIWA PESA TASLIM TSHS 4,480,000/=

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Ijumaa Tarehe 31/5/2019 saa 02:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea.

Angalia kama hukudhuria siku iliyotajwa hapo juu,Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shauri hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 21/05/2019

215248102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;115/2019
Ombi la **HUSSEIN HASSAN MWALIKO** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MARIAM CHABAI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/05/2019.

215248002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;114/2019**

**Ombi la SERAPHIA DANIEL MASAOE**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu**
**DANIEL ELIRINGIA MASAOE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 22/05/2019.

115248402

---

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

***KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO***

***Tupigie 0767 223311***

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# RAIS AMTETEA KOCHA BARCA AKIPOTEZA COPA

**SEVILLA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amesema Ernesto Valverde hatakiwi kubeba lawama baada ya kufungwa kwenye fainali ya Kombe la Copa del Rey dhidi ya Valencia, huku kocha huyo akisisitiza anajihisi vizuri licha ya kumaliza msimu vibaya.

Barca walishinda taji lao la nne la ligi ndani ya kipindi cha miaka mitano Aprili mwaka huu, lakini ikajikuta ikipoteza matumaini ya kushinda mataji matatu kwa kipindi cha siku 19.

Walianza kwa kuongoza kwa mabao 3-0 dhidi ya Liverpool kwenye nusu fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Mei 7, na wakapoteza kwa kufungwa mabao 4-0 kwenye mchezo wa pili pale Anfield 4-0, na mwisho wamefungwa na Valencia 2-1 juzi Jumamosi.

Bartomeu na nahodha Lionel Messi walimpa sapoti Valverde baada ya kichapo kutoka kwa Liverpool na rais huyo amesema kwamba klabu yake haitabadilika kufuatia kufungwa kwao na Valencia.

"Valverde ana mkataba, yeye ni kocha," amesema Bartomeu akiiambia televisheni ya Hispania.

"Kipigo cha Valencia si kwa sababu ya makosa ya kocha. Tulikuwa na nafasi nyingi, lakini mpira hakuweza kuzama wavuni. Kuna wakati unatakiwa kukubali kwamba ni makosa yetu."

Valverde alikataa kujibu swali la mwandishi wa habari wakati alipomuuliza kama ataondoka Barca kutokana na matokeo mabaya ya hivi karibuni.

"Najihisi vizuri," alijibu Valverde swali katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Unaposhinda unajisikia vizuri zaidi, lakini inakuwa tofauti pale unapofungwa."





# MAN CITY YAPANGA KUMBAKIZA SANE

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City inapanga kufanya mazungumzo na Leroy Sane ndani ya siku chache zijazo kwa ajili ya kuongeza mkataba wake, huku kukiwa na taarifa za kutakiwa na Bayern Munich, vyanzo zimeuambia mtandao wa ESPN FC.

Sane amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa, lakini kocha Pep Guardiola anataka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kubakia katika klabu hiyo.

Mabingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern wanajaribu kumshawishi mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, huku Rais Uli Hoeness akidai kumtaka mshambuliaji huyo, lakini sasa taarifa zimethibitisha kwamba, City haijapata ofa yoyote kwa ajili ya Sane.

Sane mwaka 2018, alikuwa mchezaji bora kijana wa mwaka, lakini amejikuta akikosa namba kwenye kikosi cha kwanza cha kocha, Guardiola.

Raheem Sterling na Bernardo Silva ndio wamekuwa chaguo la kwanza kama mawinga na Riyad Mahrez alianza kwenye mchezo wa mwisho wa ushindi wa taji la Ligi Kuu dhidi ya Brighton na Kombe la FA dhidi ya Watford.

Guardiola alisisitiza kwamba, anataka Sane abaki baada ya ushindi wa 6-0 kwenye Uwanja wa Wembley na akasema hatamzuia kama akitaka kuondoka kwenda anakokutaka.

# Tuchel aongezewa mwaka mmoja PSG

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, amesaini mkataba wa mwaka mmoja na sasa atadumu hapo Parc des Princes hadi mwaka 2021.

Raia huyo wa Ujerumani awali mkataba wake ulikuwa unamalizika kipindi cha majira ya joto mwakani baada ya kuteuliwa kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini ameongezewa mwaka mmoja, baada ya kuwa na msimu mzuri.

Tuchel mwenye umri wa miaka 45, ameimarisha uhusiano mzuri na nyota kama Neymar na Kylian Mbappe.

Aliiwezesha timu yake kupigana kwa nguvu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi, kabla ya kutolewa na Manchester United kwenye hatua ya mtoano wa timu 16.


Tuchel alisema baada ya kupoteza mchezo wake na United kwamba hana mpango wa kubakia hapo Parc des Princes kwa kipindi kirefu na alibainisha kwamba ataongeza mwaka mmoja tu.

"Nina furaha kubwa kuongeza mkataba na kuendelea na majukumu yangu kwa Klabu ya Paris Saint-Germain," alisema.

"Asante kwa rais na klabu nzima kwa imani mliyonionyesha mimi na benchi langu la ufundi.

"Malengo yangu ni kuendelea kuijenga timu yenye ushindani na yenye nia ya kutwaa mataji mengi zaidi, nafurahia sapoti ya mashabiki pamoja na wachezaji wote wa timu."

Mwenyekiti na Ofisa Mtendaji Mkuu wa PSG, Nasser Al-Khelaifi pia alionyesha kufurahishwa na kazi iiyofanywa na Tuchel na ameonyesha kuridhishwa naye.



## HABARI MICHEZO



# RAMOS ATAKA KUONDOKA REAL

**MADRID, Hispania**

SERGIO Ramos huenda akaondoka Real Madrid kipindi hiki cha majira ya joto baada ya kuitumikia klabu hiyo kwa miaka 14, kwa mujibu wa Sky Sports pamoja na Gazeti la Marca.

Mtandao wa El Chiringuito na Gazeti la Marca limeripoti kuwa nahodha huyo huenda akaondoka ndani ya Bernabeu muda wowote kuanzia sasa.

Ramos amekosa jumla ya mechi saba za msimu siku za hivi karibuni kwa kile kinachodaiwa kusumbuliwa na majeraha na kutarajiwa kurejea Hispania Juni mwaka huu.

Hata hivyo, nyota huyo amekuwa na msimu mbaya huku akikumbana na kifungo alichopata Machi, mwaka huu, kwenye mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ajax.

Huku akiwaudhi mashabiki baada ya kuachia kipande chake cha video ambacho kinaonyesha maisha yake ya soka wakati ambao timu yake inapata kichapo cha mabao 4-1.

Kutokana na vyanzo vya habari kutoka nchini Hispania, vinaeleza kutokuwapo kwa mahusiano mazuri baina ya klabu na mchezaji huyo, Ramos hana furaha kwa kitendo cha Rais wa timu hiyo, Florentino Perez kuwakoromea wachezaji kwenye vyumba vya kubadilishia nguo baada ya kupoteza mchezo.

Ingawa taarifa zaidi zinasema kwamba, kocha Zinedine Zidane bado anamhitaji mchezaji huyo kwenye kikosi chake.

Klabu za Manchester United na PSG ya Ufaransa zimetajwa kuwania saini ya beki huyo wa kimataifa wa Hispania.

## Juventus yajiandaa kumpa mkataba Sarri

**TURIN, Italia**

MAURIZIO Sarri ameendelea kuwa chaguo namba moja kwa 'Kibibi Kizee' cha Turin, Klabu ya Juventus huku miamba hiyo ya soka ya Italia ikitarajia kumpatia mkataba mara baada ya fainali ya Kombe la Ligi ya Europa.

Sarri kwa sasa anakiandaa kikosi chake kuikabili Arsenal huko Baku Jumatano Mei 29, mwaka huu, huku akiwa hana uhakika na maisha yake ndani Stamford Bridge licha ya kuiweka 'The Blues' katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo na kuwa kwenye uwezekano wa kutwaa taji la Europa.

Gazeti maarufu la michezo la Italia, La Gazzetta dello Sport, limeripoti kwamba kocha huyo wa Chelsea ana nafasi kubwa zaidi ya kutua Juventus.

Ukiachia mbali Sarri, klabu ya Juventus pia imeonyesha nia ya kumtaka kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino, lakini mipango hiyo inaonekana kuwa migumu kutokana na raia huyo wa Argentina kuwa na mkataba na timu hiyo ya London Kaskazini.

Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola pia amehusishwa, lakini Sarri ameonekana kuwa ndiyo chaguo kubwa kwa miamba hiyo ya soka kutoka Italia.

Bosi huyo wa zamani wa Napoli, ametokea kwenye kurasa za mbele za gazeti la michezo la La Gazzetta dello Sport kutoka Italia na kuripotiwa kuwa Sarri alikuwa kwenye kikao cha siri na Mkurugenzi wa Juventus, Fabio Paratici.

Hata hivyo, Paratici alifanya ziara yake hadi jijini London kukutana na kaka wa kocha wa Spurs, Pochettino ambaye inadaiwa kuwa ndiye wakala wake ambao wote hawa wanatazamiwa kuchukua mikoba ya Max Allegri.

Sarri anawavutia Juventus kutokana na uwajibikaji wake kwa maendeleo ya wachezaji na aina ya mfumo wake wa uchezaji.

# DE LIGT AKARIBIA KUTUA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Ajax, Matthijs de Ligt 'anakaribia' kusajiliwa na Manchester United, baada ya 'Mashetani Wekundu' hao kutoa ofa nzuri zaidi, kwa mujibu wa miamba hao wa Catalunya.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye ni nahodha wa Ajax kwa sasa ni mmoja wa wachezaji wanaozungumziwa zaidi duniani, akiwa anawaniwa na klabu kadhaa kubwa Ulaya.

Ni wazi kwamba, De Ligt atafuata nyayo za Frenkie de Jong kipindi cha majira ya joto pale Ajax, huku wengi wakiamini kwamba atajiunga na mwenzake pale Barcelona kwa euro milioni 75. Hata hivyo, mazungumzo yanaonekana kusimama pale Camp Noun na sasa Man United inapewa nafasi ya kuipata saini yake.

Taarifa kutoka kwa miamba hao wa Catalunya zinasema kwamba, kwa sasa hawawezi kufikia bei ya kumnunua mchezaji huyo. Hivyo, Manchester United, wanaweza kuwa na nafasi nzuri ya kumsajili kipindi cha majira ya joto hasa wakati huu wakiwa wanapambana kuijenga upya timu yao. Imeripotiwa kwamba, Man United imetoa ofa ya mshahara wa pauni milioni 12.3 kwa mwaka, ambao utamfanya De Ligt kulipwa kiasi cha pauni 238,000 kwa wiki.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# 'ARSENAL ITABEBA EUROPA KWA AJILI YA MKHITARYAN'

Tunawaheshimu wao, lakini tumepanga kucheza mchezo wetu tuliouzoea na staili yetu, mwisho wa siku kushinda...

**BAKU, Azerbaijan**

SOKRATIS Papastathopoulos amewashauri wachezaji wenzake wa Arsenal kupigana kiume kushinda taji la Ligi ya Europa kwa ajili ya mwenzao Henrikh Mkhitaryan ambaye atakosekana katika fainali hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Armenia hajasafiri na kikosi cha Arsenal kwenda mjini Baku kutokana na mahusiano mabaya ya kidiplomasia kati ya nchi yake na Azerbaijan.

Licha ya kuhakikishiwa usalama wake kutoka kwa ubalozi wa Azerbaijan nchini Uingereza, Mkhitaryan aliamua kutosafiri baada ya kujadiliana na familia yake.

Na sasa beki wa Arsenal raia wa Ugiriki, Sokratis amebainisha kwamba watakuwa na pigo kubwa kwa kumkosa mchezaji huyo kuelekea kwenye fainali itakayopigwa Jumatano dhidi ya Chelsea.

"Bila shaka ni pigo kubwa kwa upande wetu. Tuna huzuni na hivyo tunatakiwa kushinda kwa ajili yake," alisema Sokratis.

"Tunatakiwa kuwa pale na kucheza mchezo wetu. Na kuamini kwamba tunaweza kufanya lolote na nafikiri kama tukicheza vizuri kwa asilimia 100 tutakuwa na siku nzuri, na pia kuwa na bahati, kwa sababu katika mchezo mmoja kitu chochote kinaweza kutokea na tunaweza kufanya hivyo."

Aidha, Sokratis amewataka wachezaji wenzake akili yao yote kuielekeza kwenye mchezo huo na kutokuwa na hofu yoyote dhidi ya Chelsea.

"Wana wachezaji wazuri na wana kocha mzuri, lakini hatupaswi kuwahofia," aliongeza kusema Sokratis.

"Tunawaheshimu wao, lakini tumepanga kucheza mchezo wetu tuliouzoea. Kucheza kwa staili yetu, akili yetu kuiwekeza kwenye mchezo huo na kutengeneza nafasi nyingi zaidi pamoja na kujilinda vizuri, naamini tutakuwa na nafasi nzuri ya kufanya vizuri kwenye mchezo huu.

"Kucheza kwa pamoja na mwisho wa siku tutashinda mchezo, sio kitu kigumu kwa upande wetu, lakini pia sio vigumu kwa upande wao."

## KWA UFUPI

### GUARDIOLA AMPELEKA SARRI JUVE

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri amekubali dili la kuinoa Juventus baada ya kocha wa Manchester City, Pep Guardiola kutupilia mbali ofa hiyo. ***(Italian journalist Tancredi Palmeri, via Sunday Mirror)***

### KOULIBALY ANUKIA KUTUA MADRID

BEKI anayewindwa na Manchester United, Kalidou Koulibaly, 27, atajiunga na Real Madrid baada ya mimba hiyo ya La Liga kutoa ofa ya pauni milioni 79 kwa mlinzi huyo wa kati wa Napoli na Senegal. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### MOSES KUMFUATA CONTE INTER

WINGA wa Chelsea, Victor Moses, 28, atakatisha mkataba wake wa mkopo na Fenerbahce. Nyota huyo wa kimataifa wa Nigeria anatumai kujiunga kwa mara nyingine na Antonio Conte wakati kocha wake huyo wa zamani atakapoteuliwa rasmi kuinoa Inter Milan. ***(Football London)***

### DYBALA CHAMBO KWA POGBA

Juventus ipo tayari kumtoa ofa straika Muargentina, Paulo Dybala, 25, na beki wa kushoto Mbrazil, Alex Sandro, 28, ili kubadilishana na Manchester United kwa kiungo wao, Mfaransa Paul Pogba, 26. ***(Sunday Express)***

### DE LIGT AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United "inakaribia kabisa" kumsajili beki wa kati Matthijs de Ligt, 19, kutoka Ajax, licha ya Barcelona kupewa nafasi kubwa ya kuipata saini ya Mholanzi huyo. ***(RAC1, via Metro)***

### SANE AANDALIWA MASHARTI CITY

Manchester City itampa ofa winga wake, Mjerumani Leroy Sane, 23, ya mshahara wa pauni 150,000 kwa wiki ili kujaribu kumshawishi kusaini mkataba mpya, lakini itaweka kipengele cha kuuvunja kwa zaidi ya pauni milioni 100, kwa nyota huyo ambaye anawindwa na Bayern Munich, kama hapatakuwa na makubaliano yaliyofikiwa. ***(Sunday Mirror)***

### REAL YASHUSHA DAU LA HAZARD

Chelsea itaitaka Real Madrid kulipa pauni milioni 130 kwa mshambuliaji wao, Eden Hazard, 28, ingawa mimba hiyo ya Hispania inamthaminisha Mbelgiji huyo na pauni milioni 88. ***(Sky Sports)***

### SILVA KUTAJIRISHWA QATAR

KIUNGO Mhispania David Silva amepewa ofa nono ya mkataba wa miaka miwili na Klabu ya Qatar na anaweza akawa amecheza mechi ya mwisho Manchester City. ***(Sun on Sunday)***

### WENGER ATAKIWA JAPAN

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger ana ofa mkononi ya kurudi mzigoni kufuatia kutakiwa na klabu ya Japan, Vissel Kobe. ***(Goal.com)***

### LAZIO NAYO YAMFUATA WELBECK

Lazio imejiunga katika mbio moja na Everton, Newcastle na West Ham katika kuwania saini ya mshambuliaji aliyetupiwa virago Arsenal, Danny Welbeck, 28. ***(Sun on Sunday)***

### FELIX KUITOA JASHO UNITED

Manchester United itapaswa kulipa zaidi ya pauni milioni 105 kwa Benfica ili kuipata saini ya mshambuliaji Mreno Joao Felix, 19, amesema Meneja Mkuu wa Primeira Liga, Domingos Soares de Oliveira. ***(Sunday Express)***

### MILAN YAMPIGIA HESABU ALLEGRI

MTENDAJI Mkuu wa AC Milan, Ivan Gazidis amewasiliana na Massimiliano Allegri kuona kama anataka kurudi kufanya kazi ya ukocha wakati atakapoondoka kwa mabingwa wa Serie A, Juventus mwishoni mwa msimu. ***(Tuttomercatoweb - in Italian)***

### FEKIR RUKSA KUONDOKA LYON

RAIS wa Lyon, Jean-Michel Aulas amekubali kumruhusu kiungo Mfaransa Nabil Fekir, 25, ambaye alikaribia kujiunga na Liverpool mwaka jana, kuondoka katika klabu hiyo majira haya ya kiangazi. ***(L'Equipe - in French)***

HABARI MICHEZO

# SAMATTA ATUA, AFUNGUKA MAFANIKIO UBINGWA GENK

**Na Somoe Ng'itu**

MSHAMBULIAJI wa Klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji, Mbwana Samatta, amerejea nchini juzi tayari kuingia kambini na kikosi cha Taifa Stars, huku akisema anaamini miaka ijayo Tanzania itakuwa na wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa barani Ulaya.

Taifa Stars ambayo imefuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), inatarajia kuingia kambini Jumamosi Juni Mosi ili kujiwinda na michuano hiyo itakayopigwa Misri baadaye mwaka huu.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alikuwa ni mmoja wa wadau wa michezo ambao walijitokeza kumpokea Samatta ambaye ameisaidia timu yake kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Samatta alisema amefurahishwa na mafanikio aliyoyapata katika msimu wake wa pili akiwa na Genk na anaamini hali hiyo itachochea wachezaji wengine wa hapa nyumbani kujituma na hatimaye kusajiliwa na Klabu za Ulaya.

Alisema anachokifanya anapokuwa Genk ni kupambana ili apate mafanikio kwa sababu anaamini yeye sasa hivi ni mwakilishi wa Tanzania katika medani ya soka kimataifa.

"Najihisi furaha sana, kila mchezaji ndoto yake ni kushiriki mashindano makubwa, ni jambo zuri nimefanikiwa na huko huwa nawawakilisha Watanzania, naamini iko siku tutashuhudia vijana wengi wakicheza soka Ulaya," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa African Lyon, Simba na TP Mazembe ya DRC.

Aliongeza kuwa tuzo aliyopata ya mfungaji bora, mbali na kuzidi kumjenga, lakini imesaidia pia kuipa klabu yake heshima kwa sababu inaonyesha wazi kwamba msimu huu wamepata mafanikio.

"Wote walifurahia mimi kupata tuzo, wanaamini nilistahili, hata hivyo nimetoa changamoto kwa aliyekuwa mfungaji wa msimu uliopita, ingawa yeye alifunga mabao 25, nilijaribu kumvua hiyo historia lakini haikuwa bahati," Samatta aliongeza.

Hii ni mara ya kwanza kwa Samatta kuiongoza Taifa Stars kushiriki fainali hizo ambapo wamepangwa kundi moja pamoja na Algeria, Senegal na Kenya.




Meneja wa La Liga Kanda ya Afrika, Antonio Barradas (kushoto), akimkabidhi tuzo Tarimba Abbas kwa niaba ya SportPesa kwa kufanikisha ujio wa Sevilla nchini Tanzania. **PICHA: SPORTPESA**

## Ushindani mkali kushuka daraja

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya Simba kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara waliokuwa wanaushikilia, Bodi ya Ligi Kuu (TPLB), imesema ushindani sasa umebaki katika kujinasua na janga la kushuka daraja, imeelezwa.

Simba ikiwa imebakiza mchezo mmoja ili kumaliza msimu, tayari ilishatangazwa kuwa bingwa wa msimu huu na juzi ilifikisha pointi 92, huku Yanga inayomfuata ikiwa na pointi 85.

Ofisa Mtendaji wa Bodi ya Ligi, Boniface Wambura, alisema jana kuwa bado mpaka sasa hakuna timu zinazojulikana kwamba zinashuka daraja ukiondoa African Lyon ambayo inaburuza mkia katika ligi hiyo. Wambura alisema "vita" hiyo iliyobakia inaongeza ushindani katika mechi zote zitakazochezwa hapo kesho kwa sababu kila upande unahitaji kushinda ili kujinasua.

Alisema ligi ya msimu huu imekuwa ndefu kutokana na kushirikisha klabu 20, huku pia kalenda ya mashindano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf) ikiingiliana.

"Msimu huu tumeshirikisha timu 20, imefanya ligi imekuwa ndefu, pia tumekuwa na changamoto ya kukosa mdhamini, lakini klabu zimepambana sana ili kuhakikisha zinacheza mpira kama ratiba ilivyokuwa inaonyesha," alisema Wambura.

Timu ambazo ziko katika hatari hiyo ya kushuka daraja na pointi zake ziko kwenye mabano ni Singida United (44), Biashara United (44), JKT Tanzania (44), Stand United (44), Mbao FC (44), Tanzania Prisons (43), Kagera Sugar (43), Ruvu Shooting (42) na Mwadui FC yenye pointi 41.

# Kocha Biashara aishukuru mvua Taifa sare Simba

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kupata sare ya bao 1-1 dhidi ya Simba, Kocha Mkuu wa Biashara United, Amri Said amesema mvua iliyonyesha na kusababisha baadhi ya sehemu Uwanja wa Taifa kutuama maji, kuliwasaidia kupata matokeo hayo na sasa fainali yake ya kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara itakuwa ni kwenye mchezo wa mwisho watakaocheza ugenini dhidi ya Mbeya City.

Biashara United sasa ina pointi 44 na inahitaji ushindi wa aina yoyote ili kujihakikishia kwamba inabaki katika ligi hiyo ya juu kwa upande wa Tanzania Bara.

Said alisema kuwa haikuwa kazi rahisi kwa kikosi chake kugawana pointi dhidi ya mabingwa wa ligi hiyo, lakini hali ya kujiamini waliyokuwa nayo wachezaji wake pamoja na maji kutuama uwanjani ndio imepelekea kugawana pointi.

"Unajua Simba wanacheza pasi fupi fupi za chini, hivyo kutokana na hali ya uwanja walishindwa kupenyeza pasi zao na sisi kutumia faida hiyo kuwadhibiti kwa mipira ya juu," alisema.

Alisema kuwa kila mchezaji wa Biashara United anajua kuwa hawatakiwi kufungwa na hali hiyo inawaongezea umakini kwa sababu wanataka kuona msimu ujao wanaendelea kucheza katika Ligi Kuu licha ya changamoto mbalimbali walizopitia msimu huu.

"Hakuna mechi rahisi, tena hasa kuipata kwenye Uwanja wa Taifa, tunamshukuru Mungu kwa hiki alichotujalia, sasa tunajipanga upya kuwavaa Mbeya City, tukishinda tutakuwa mahali salama bila kujali matokeo ya wengine," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema kuwa bado timu yake ina nafasi ya kubakia katika ligi hiyo licha ya juzi kukubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa JKT Tanzania. "Wenzetu wametengeneza nafasi mbili na wakazitumia vizuri, sisi tumetengeneza nafasi nyingi lakini hatukuzitumia, napenda pia niwape pole wachezaji wangu kwa kupoteza mchezo, lakini niwapongeze kwa kiwango kizuri walichokionyesha licha ya kufungwa, bado tutapambana ingawa najua Mbao ni wagumu wanapokuwa kwao," Maxime alisema.

Mechi nyingine ya ligi hiyo ambayo timu zake zinapambana kujinasua na janga la kushuka daraja itakuwa ni kati ya JKT Tanzania dhidi ya Stand United kutoka mkoani Shinyanga.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.SIMBA | 37 | 29 | 5 | 3 | 77 | 15 | 92 |
| 2.YANGA | 37 | 27 | 5 | 5 | 56 | 25 | 86 |
| 3.AZAM | 37 | 20 | 12 | 5 | 52 | 21 | 72 |
| 4.KINONDONI MC | 37 | 12 | 16 | 9 | 38 | 25 | 52 |
| 5.MTIBWA SUGAR | 37 | 14 | 7 | 16 | 36 | 34 | 49 |
| 6.LIPULI | 37 | 12 | 13 | 12 | 31 | 37 | 49 |
| 7.NDANDA | 37 | 12 | 12 | 13 | 24 | 34 | 48 |
| 8.MBEYA CITY | 37 | 13 | 8 | 16 | 38 | 39 | 47 |
| 9.ALLIANCE | 37 | 12 | 11 | 14 | 33 | 41 | 47 |
| 10.COASTAL UNION | 37 | 11 | 14 | 12 | 32 | 42 | 47 |
| 11.SINGIDA UNITED | 37 | 11 | 12 | 14 | 30 | 39 | 45 |
| 12.BIASHARA UNITED | 37 | 11 | 11 | 15 | 30 | 35 | 44 |
| 13.JKT TANZANIA | 37 | 10 | 14 | 13 | 26 | 34 | 44 |
| 14.STAND UNITED | 37 | 12 | 8 | 17 | 38 | 48 | 44 |
| 15.MBAO | 37 | 11 | 11 | 15 | 26 | 40 | 44 |
| 16.TZ PRISONS | 37 | 10 | 13 | 14 | 27 | 30 | 43 |
| 17.KAGERA SUGAR | 37 | 10 | 13 | 14 | 32 | 42 | 43 |
| 18.RUVU SHOOTING | 37 | 10 | 12 | 15 | 34 | 43 | 42 |
| 19.MWADUI | 37 | 11 | 8 | 18 | 44 | 51 | 41 |
| 20.AFRICAN LYON | 37 | 4 | 11 | 22 | 23 | 52 | 23 |

# Michezo

Jumatatu Mei 27, 2019

Nipashe





‘Arsenal itabeba Europa kwa ajili ya Mkhitaryan’

HABARI UK 30

KAMA KAGERE...



Kevin Gameiro akishangilia kwa kufunga jicho moja kama straika wa Simba, Meddie Kagere, baada ya kuifungia Valencia bao la kwanza wakati wakishinda 2-1 kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa Del Rey'] dhidi ya Barcelona na kulitwaa kombe hilo juzi.

HABARI UK. 28

# SIMBA SC UBINGWA, ZAHERA ATOA KILIO

●●●Morogoro hapatotosha ikiivaa Mtibwa kesho, Aussems aongezwa mwaka, wachezaji Yanga wazidi kumchanganya...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi kamili cha Simba kikitarajia kutua mkoani Morogoro leo kukabidhiwa ubingwa wao, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, analalamika kuwakosa baadhi ya wachezaji wake mazoezini ili kujiandaa na mchezo wao wa mwisho wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kesho.

Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Simba watafunga pazia la ligi hiyo ugenini dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri wakati Yanga na Azam FC zenyewe zitakutana kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Zahera alisema jana kuwa wachezaji wake nyota wameshindwa kuhudhuria katika mazoezi ya juzi na jana kutokana na kuwa wagonjwa, lakini akakasirika na kitendo cha beki wake wa kati, Kelvin Yondani kutojulikana alipo.

“Yondani si mgonjwa na wala hatuna taarifa zake, tunampigia simu hapokei na wala hatujui yupo wapi, anafanya mambo ya ovyo sana! Nimemtuma Cannavaro (Nadir Haroub) aende kwake kumwangalia halafu atanileteа mrejesho, hapo ndipo nitajua nifanye uamuzi gani kuhusu Yondani, “ alisema Zahera.

Kocha huyo aliongeza kuwa anahitaji kumaliza msimu kwa kupata ushindi licha ya kwamba tayari watani zao, Simba wameshafanikiwa kutetea ubingwa waliokuwa wanaushikilia baada ya kufikisha pointi 92 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine msimu huu.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili kuwa wataelekea Morogoro na wachezaji wote kwa sababu ndiko watakapopokea kikombe cha ubingwa na kuvaa medali.

Rweyemamu alisema kuwa licha ya kutetea ubingwa, wamejiandaa kupambana ili kushinda mchezo huo wa mwisho ili wapokee kombe lao kwa furaha kwa sababu hiyo ndio zawadi kubwa kwa mashabiki wao.

“Safari ya Morogoro ni kesho (leo), na mpango wetu ni kwenda na wachezaji wote, tunahitaji kwenda kumaliza msimu kwa kishindo, tunajua Mtibwa Sugar ni timu ngumu na yenye wachezaji wazoefu,” aliongeza meneja huyo.

Bodi ya Ligi (TPLB), ilitangaza kuwa itawakabidhi kikombe chao cha ubingwa kesho baada ya hapo juzi kuahirisha kutokana na aliyekuwa mgeni rasmi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola kupata udhuru.

Ofisa Mtendaji wa bodi hiyo, Boniface Wambura, alisema jana kuwa sherehe zote sasa zitafanyika Morogoro na wanaamini mambo yatakwenda vema kama walivyotarajia.

Kutokana na kutwaa ubingwa huo, Simba ambayo inafundishwa na Mbelgiji Patrick Aussems ambaye jana amesaini mkataba wa mwaka mmoja zaidi wa kuendelea kuinoa klabu hiyo, mwakani itaiongoza tena timu hiyo kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati KMKM yenyewe itapeperusha bendera hiyo kwa upande wa Zanzibar.

## Sevilla, SportPesa zaidi ya mafanikio

**Na Mwandishi Wetu**

UJIO wa mabingwa wa kihistoria wa michuano ya Uefa Europa League, Klabu ya Sevilla nchini kwa ushirikiano mkubwa wa kampuni ya kubashiri matokeo michezoni ya SportPesa na waendeshaji wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga ni zaidi ya mafanikio nchini, imeelezwa.

Mbali ya wachezaji wa Ligi Kuu Tanzania kuonekana duniani kote kutokana na mechi yao ya kirafiki dhidi ya Simba ilimalizika kwa Sevilla kushinda 5-4, kurushwa mubashara na DSTv, ziara hiyo ya Sevilla imefungua ukurasa mpya wa uhusiano wa kimpira kati ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Ligi La Liga.

Kwenye semina elekezi ya masuala ya uongozi wa soka iliyofanyika Uwanja wa Taifa Mei 22, mwaka huu, Rais wa La Liga Kanda ya Afrika, Antonio Barradas, alisema malengo yao ni kufanya miradi mbalimbali nchini yenye lengo la kuendeleza soka kupitia ushirika wao mpya na TFF.

Lakini pia katika semina hiyo, viongozi wa soka nchini katika ngazi za klabu, Shirikisho na taasisi za mpira, waliweza kupewa ‘madini’ kutoka kwa Rais wa Sevilla, Jose Castro Camona pamoja Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Ramon ‘Monchi’ Rodriguez juu ya uendeshaji wa mpira kwa minajili ya kibiashara kama ambavyo klabu kubwa duniani hufanya.

Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema lengo la ziara hiyo limefanikiwa kwani uitikio wa watu ulikuwa mkubwa sana na wachezaji wa Sevilla na viongozi wao wamefarijika na kujifunza mambo mengi japo kwa muda mfupi.

“Wachezaji wameweza kupata mafunzo, ujuzi na mbinu na viongozi vile vile wamepata mafunzo ya uongozi bora na masoko, hii ni faraja kubwa sana kwa SportPesa Tanzania,” alisema Tarimba.

“Tumefarijika sana, Tanzania imefahamika sana kufuatia ujio wa Sevilla na kwa sasa itakuwa rahisi kuleta hata klabu nyingine, Sevilla wamefarijika na wameona utamaduni na mambo kadha wa kadha ya historia ya binadamu,” alisema Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Harrison Mwakyembe


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >